Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Nne - Tarehe 16 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa na:-

**MHE. LEPHY B. GEMBE (k.n.y. MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka 2003.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa Mwaka 2003.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2003.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE (k.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA):**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2003.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa mwaka 2003.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDO MBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Miundo Mbinu kwa mwaka 2003.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 45

### Kutokuwepo Mipango Thabiti ya Uwiano Kwenye Miradi

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi katika sehemu mbalimbali za nchi yetu wamepata hamasa kubwa na hivyo kubuni na kutekeleza miradi mingi ya maendeleo kama vile ya shule na zahanati kwa kasi kubwa na kwa kuwa mara nyingine uzinduzi wa miradi hiyo unakwamishwa na upungufu wa mahitaji muhimu kama vile walimu, wauguzi na *kits* za madawa:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba hali kama hii inatokana na kutokuwepo mipango thabiti ya uwiano kati ya miradi mbalimbali ya jamii inayobuniwa na kutekelezwa katika ngazi za vijiji na wilaya bila kuwepo mipango sambamba kwa ngazi ya Taifa ya kuwezesha kukidhi mahitaji mbalimbali kwa idadi na wakati unaostahili?

(b) Je, ukwamaji huo hauchangii katika kukatisha tamaa wananchi na wahisani?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuepusha hali kama hii isiendelee kuwepo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inalitambua tatizo la upungufu wa mahitaji muhimu kama vile walimu, wauguzi na *kits* za madawa kukidhi mahitaji ya miradi mingi ya maendeleo inayotekelezwa na wananchi huko vijijini na Wilayani. Tatizo hili halitokani na ukosefu wa mipango thabiti ya uwiano, ambayo inaonyeshwa vyema katika mwongozo wa mipango na bajeti unaotolewa kila mwaka. Ipo changamoto moja na tatizo moja. Utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo hivi sasa nchini kwa kutumia nguvu za wananchi, unaendelea ili kuondoa kero zao, hii ni changamoto kwa Serikali. Ukosefu wa

taarifa kamili za miradi inayobuniwa vijijini na uchache wa raslimali ukilinganisha na mahitaji ya Taifa ni tatizo. Mahitaji ya Taifa ni mengi kuliko uwezo. Mfano, mahitaji halisi ya madawa kwa nchi nzima kwa mwaka wa fedha 2003/2004 yaliyakuwa shilingi 34.7 bilioni, wakati fedha zilizotengwa zilikuwa shilingi 23.4 bilioni tu. Changamoto iliyopo kwa Serikali sasa ni je, tuache kujenga majengo ya huduma vijijini tukisubiri uwiano wa huduma au tujenge tusubiri wafanyakazi na madawa?

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la walimu katika shule za msingi, Serikali kwa kipindi cha mwaka 2003 imeajiri walimu 10,719, sawa na asilimia 92 ya lengo la walimu 11,651 na bado ziko nafasi za ajira ya walimu 932. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004, walimu kutoka vyuo vya ualimu waliofaulu wataajiriwa moja kwa moja na hakutakuwa na mwalimu anayesubiri ajira.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Waheshimiwa Wabunge, kuendelea kuhamasisha wananchi katika kuchangia nguvu zao ili kupunguza pengo la majengo kwa ajili ya huduma mbalimbali za jamii na vile vile kuwataka Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, kusaidia wananchi katika kuibua miradi yao hii ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu husika za uanzishaji wa miradi ya jamii. Nina imani taratibu zikifuatwa na wananchi wakaambiwa ukweli juu ya hali halisi ya raslimali nchini, tatizo hili litapungua.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kumekuwepo mara nyingi zahanati, shule au vituo vya afya vinachelewa kufunguliwa kutokana na sababu hizi ambazo zimeelezwa hapo awali. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuchukua hatua thabiti zaidi za kuweza kuoanisha mipango ya Serikali za Vijiji na Serikali za Wilaya pamoja na Serikali Kuu, ili ucheleweshaji huu usiweze kutokea siku zinazofuata? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwandogro kwamba ni vema Serikali ikaangalia utaratibu wa uwiano wa mipango kati ya vijiji, Wilaya, Mkoa na ngazi ya Taifa na hicho ndiyo tunachojaribu kukifanya. Tatizo lililopo ni kwamba, ufinyu wa bajeti ambao umejitokeza kila mara ndiyo unaotufanya tusiweze kukidhi mahitaji yote ambayo yanahitajika katika miradi hii mingi ya maendeleo inayojengwa kwa nguvu za wananchi. Nadhani Mheshimiwa Mwandoro, atakubali kwamba, mpaka sasa hivi bajeti yetu kinchi bado ni tegemezi, tunaweza kutoa bajeti asilimia 42 wakati asilimia 58 bado ni tegemezi. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo itabidi tuendelee kuliangalia jinsi tunavyoendelea.

**MHE. ISMAEL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali na ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hizi shughuli za ujenzi wa huduma kama zahanati zinatia moyo sana kwa wananchi kwamba zitawapunguzia matatizo ya kusafiri mwendo mrefu wa kupata huduma kama hizi; na kwa kuwa tuna upungufu wa madaktari/waganga katika hizi zahanati, lakini wapo watumishi ambao wanapenda kwenda kusoma katika vyuo vya uganga kama vile Bugando, Muhimbili na kadhalika, lakini tatizo wanakosa watu wa kuwalipia ada; na kwa kuwa Halmashauri sasa hivi baada ya kupunguza baadhi ya vyanzo vyenye kuleta kero wamebaki na vyanzo vichache ambavyo havitoshi kukusanya pesa ya kuweza kusomesha watumishi; je, Serikali itakuwa tayari kuangalia upya suala la kusomesha watumishi kama waganga ili waweze kupatikana na kuweza kupelekwa katika hizi zahanati ambazo zinajengwa kwa wingi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Serikali ingependa kuona maeneo yote chini ya huduma za jamii kwa maana ya afya, elimu na maji, yanapata watalaam wote wanaohitajika. Kama nilivyosema hapo awali, tatizo ni ufinyu wa raslimali hasa za kuwasomesha hawa watalaam ambao wangepaswa kuingia katika maeneo hayo. Lakini nakubaliana kwamba, iko haja kwa Serikali kuona ni utaratibu gani utafanyika kama tunavyofanya kwenye sekta ya elimu, kuendeleza elimu katika fani ya udaktari au waganga ambao wanaweza wakatumika katika zahanati zetu.

Na. 46

**Ukuaji wa Uchumi Tanzania**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya mageuzi makubwa ya kiuchumi nchini na kwa kuwa kwa sababu hiyo uchumi wa Tanzania sasa unakua kwa kasi nzuri:-

(a) Je, uchumi huo umekuwa kwa asilimia ngapi kuanzia mwaka 1996 hadi swali hili linapojibiwa na unatarajia kukua hadi asilimia ngapi kufikia Desemba, 2005?

(b) Je, uchumi wa Tanzania unalinganishwa vipi na uchumi wa Kenya na Uganda katika Afrika Mashariki katika kipindi hicho?

(c) Je, ni nini manufaa ya moja kwa moja *(Direct Benefits)* kwa wananchi wa kawaida kijijini yanayotokana na kukua huku kwa uchumi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1996 hadi 2002, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 4.7. Katika mwaka 1996 uchumi ulikua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 6.2 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, taarifa za awali zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2003, uchumi ulikua kwa asilimia 4.7 ukilinganishwa na asilimia 5.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2002. Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2003, uchumi umekadiriwa kukua kwa asilimia 5.7, ukuaji ambao ni pungufu ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.2 mwaka 2002. Kupungua kwa ukuaji wa uchumi mwaka 2003 kumesababishwa na hali ya ukame hali ambayo imeathiri uzalishaji katika sekta kubwa ya kilimo, hasa sekta ndogo ya mazao. Taarifa ya ukuaji halisi katika mwaka 2003 bado zinachambuliwa ili kuweza kubainisha makadirio ya ukuaji wa miaka ya 2004 na 2005. Aidha, makadirio ya awali ya ukuaji katika miaka hiyo ni asilimia 6.3 mwaka 2004 na asilimia 6.5 mwaka 2005.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa nchi za Afrika Mashariki, uchumi wa Tanzania katika mwaka 1996 ulikua kwa asilimia 4.2 ukilinganisha na asilimia 4.6 ya ukuaji wa uchumi wa Kenya na asilimia 4.7 ya ukuaji wa uchumi wa Uganda. Mwaka 2002 ukuaji ulikuwa asilimia 6.2, 1.1 na 5.1 kwa Tanzania Kenya na Uganda kwa mtiririko huo. Takwimu zaidi za kulinganisha ukuaji katika nchi hizi tatu zinaonyeshwa katika kiambatisho tulichokiwasilisha kwa Mheshimiwa Mbunge.

(c) Mheshimiwa Spika, kukua kwa uchumi kunatokana na kwanza, kuongezeka kwa uwekezaji wa ndani na nje, pili, kukua kwa biashara ya ndani na nje, tatu, kuboreshwa kwa huduma za kichumi na kijamii na nne, kuweka mazingira muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na hatimaye kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, sifa zote hizo zimewezesha wananchi wa kawaida vijiji kwa kiwango fulani kupata manufaa ya moja kwa moja. Ukuaji uchumi kupitia uwekezaji umetoa fursa ya jamii kwa jumla kushiriki katika uzalishaji mali, kuongeza ajira, kupanua wigo wa ujasirimali na kuongeza mapato na hatimaye kupunguza kiwango cha umaskini wa kipato. Bidhaa muhimu sasa zinapatikana kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa. Ukuaji wa kiwango cha mapato ya Serikali, umesaidia kupunguza umaskini usio wa kipato kwa wananchi wengi vijijini kupitia maboresho ya barabara, mawasiliano, elimu, afya, maji, ujenzi wa nyumba bora na kadhalika. Aidha, dira ya maendeleo 2025 na mkakati wa kupunguza umaskini, bado ni dhamira kubwa ya Serikali kuhakikisha kuwa, manufaa ya moja kwa moja yanawafikia wananchi wengi vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa sasa wa Serikali wa kuendeleza kwa nguvu sera za uwezeshaji na uwekezaji utasaidia kutoa fursa kubwa na pana zaidi ya kuwasaidia wananchi wa ngazi zote katika kuibua fursa za kujiendeleza kiuchumi. Maendeleo ni mchakato na siyo tukio hivyo, tunawajibika wananchi wote hususan sisi Wabunge, kuhamasisha zaidi nia ya kukuza uchumi wetu kupitia jitihada kubwa za kukuza maendeleo yetu.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na fasaha. Lakini nina maswali maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa takwimu alizozieleza Mheshimiwa Waziri zinaonyesha kuwa kumekuwa na kasi nzuri ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania ukilinganisha na ule wa Kenya, ni sababu ambazo bado zipo sasa zinapelekea kuwa uchumi wa Kenya uwe na nguvu kuliko wa Tanzania na itachukua muda kwa shilingi ya Tanzania kuwa sawa na ile ya Kenya? *(Makofi)*

(b) Serikali inazo taarifa kwamba pamoja kukua kwa kasi kwa uchumi wa Tanzania kuna kundi la Watanzania wanaozidi kuwa maskini sana kiasi cha kwamba hawawezi kumudu mahitaji/maisha ikiwemo wengine wanaopata mlo mara moja kugharamia elimu na afya na mambo mengine muhimu wakati kuna kundi la Watanzania wanaojilimbikizia utajiri kwa fujo na Serikali inafanya nini kuziba pengo hili hatari? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tuna haja ya kuufanya uchumi wetu uwe na nguvu zaidi tukilinganisha na nchi jirani. Siri moja ya kuufanya uchumi wetu uwe na nguvu zaidi ni kukazana zaidi kwanza na kufanya kazi kwa bidii, pili kukazania suala la kuimarisha biashara ya mauzo yetu nje na tatu kama nilivyosema kutumia vigezo mbalimbali vya uchumi kuhakikisha kwamba uchumi wetu unatengemaa. *(Makofi)*

Pili, ni kwamba liko tatizo la umaskini ambalo tunaendelea nalo nchini sasa hivi na ndiyo maana Serikali inatekeleza kwa makusudi kabisa mkakati wa kupunguza umaskini. Kama nilivyosema, suala la kupunguza umaskini linamaanisha maendeleo na maendeleo ni mchakato siyo tukio kwa hiyo itatuchukua muda mpaka tufikie hapo na ndiyo maana Serikali sasa kupitia sekta ya huduma za jamii, tayari imeshapunguza kipato kisicho na umaskini. Tuna hakika kwamba, baada ya kurekebisha miundombinu na kuuza mazao yetu, tutakuwa tumemalizia kufaidisha kipato cha umaskini.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kwa muda mrefu sasa sekta ya kilimo imekuwa haikui na kwa kuwa sekta ya kilimo ndiyo inayoajiri Watanzania wengi, sasa ukuaji huu wa uchumi katika mazingira ya ukuaji wa uchumi wa sasa, mazingira haya yanatumika vipi katika kuiboresha sekta ya kilimo hasa ukizingatia kwamba, bei za wakulima zimekuwa zikipungua hata ukifanya kazi vipi, lakini bado hali yao inaendelea kuwa duni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa uchumi wetu unategemea kukua kwa sekta ya kilimo na ndiyo maana tumekuwa na mkakati maalum wa kuendeleza kilimo *(Agricultural Development Sector Program)* na mkakati huo unagusia maeneo yale ambayo yataweza kupatikana kwa pembejeo, kuboresha masoko na kukuza uzalishaji. Ni kweli kabisa kwa sababu mazao yetu mengi siyo ya kusindika kwa sababu tunazalisha mazao ya mwanzoni

kama pamba, mara nyingi tumekuwa tukichukua bei zilizopo katika soko la dunia. Tunachohitaji sasa ni kuendeleza jitihada yetu kama tulivyofanya kwenye zao la pamba ambayo sasa hivi inasindikwa kwa asilimia 75 sasa baada ya kufufua viwanda vingi vya nguo ili tuweze kuuza mazao yaliyosindikwa badala ya kuuza mazao ghafi. *(Makofi)*

Na. 47

**Marekebisho ya Sheria ya *PPF* Na. 25 ya 2001**

**MHE. HADIJA K. KUSAGA (k.n.y. MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge lilipopitisha marekebisho ya Sheria ya *PPF* Na. 25 ya mwaka 2001 na kuweka umri wa kuanza kulipwa pensheni ya kila mwezi kuwa miaka 55 walitakiwa kuwahusisha wastaafu wale tu wapya kuanzia tarehe ile ambayo Mheshimiwa Rais, alipoweka sahihi ya kuridhia mabadiliko ya sheria hiyo, lakini Bunge lilipotoka pale lilipoidhinisha mabadiliko hayo kutumika hata kwa wale wastaafu waliokuwa wanapata pensheni hiyo *(Retrospective Application): -*

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba *retrospective application* ya sheria inayohusu kuzuia malipo au mapato ya mtu ni kukiuka Katiba ya nchi na inavunja haki za binadamu na kwa kufanya hivyo kunavunja Mikataba halali kati ya Shirika la *PPF* na wale wastaafu waliokuwa tayari wanalipwa pensheni hiyo?

(b) Kwa kuwa wastaafu waliokuwa wanapata pensheni hiyo ambapo wengi wao walikuwa wanapata kati ya Sh. 10,000/= na 20,000/= kwa mwezi walikuwa wamejihakikishia mapato hayo ambayo yalikuwa tegemeo pekee kwao na familia zao. Je, Serikali haioni kuwa hatua hiyo ya Shirika la *PPF* inawanyanyasa na kuwatesa wananchi hao maskini?

(c) Je ni lini Serikali itairudisha Bungeni Sheria hiyo Na. 25 ya mwaka 2001 ili kifungu kipya Na. 26(2)(b) kiweze kufutwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Bunge lako Tukufu mnamo mwaka 2001, lilipitisha marekebisho ya Sheria ya *PPF* Na. 25 ya mwaka 2001 na kuweka umri wa kuanza kulipwa pensheni ya kila mwezi kuwa ni miaka 55 na kwamba mabadiliko haya yalianza kutumika hata kwa wale wastaafu waliokuwa wanapata pensheni hiyo *(Retrospective Application).*

Kwa kawaida matumizi ya sheria yanayorudi nyuma katika utekelezaji wake, hayaruhusiwi isipokuwa pale ambapo sheria inatamka bayana urudishwaji nyuma wa sheria husika. Kifungu Na. 26 (2) cha Sheria ya Pensheni ya Mashirika ya Umma Na. 25 ya mwaka 2001, kinaelekeza matumizi ya kifungu hicho kwa kutoruhusu malipo ya pensheni kwa mtu yeyote ambaye hajafikia umri wa kustaafu wa miaka 55.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 11(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatamka bayana kwamba, mtu atastahili malipo ya hifadhi ya jamii pale ambapo atafikisha umri wa uzee au kukabiliwa na ulemavu au ugonjwa. Marekebisho ya Sheria ya *PPF* Na. 25 ya mwaka 2001 yamezingatia matakwa ya ibara ya 11(1) ya Katiba kwa kuweka umri wa uzee wa kustaafu ambao ni miaka 55. Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana nami kwamba, kuruhusu malipo ya pensheni bila kujali umri wa uzee ni kukiuka matakwa ya Katiba na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, hivi sasa kuna kesi inayoendelea katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Mjini Dar es Salaam (kesi Na. 129/2002 na 75/2002, Nassoro Gogo na wenzake dhidi ya *PPF*) inayohusu uhalali wa Kikatiba wa kusitisha malipo ya pensheni kwa vijana. Hivyo basi, kwa taratibu za kisheria si vyema suala hili kuzungumzwa kwa undani nje ya Mahakama.

Kuhusu Serikali kuwanyanyasa na kuwatesa wastaafu vijana waliokuwa wanapata Shilingi 20,000/= baada ya kusitisha pensheni zao, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali haina nia ya kuwanyanyasa wastaafu hao bali kulinda maslahi yao watakapokuwa wazee ambao hawawezi kuajiriwa wala kujiajiri.

Baada ya maelezo hayo yanayothibitisha kwamba, marekebisho ya Sheria ya Pensheni ya Mashirika ya Umma Na. 14 ya 1978 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 25 ya mwaka 2001, yanazingatia matakwa ya Kikatiba kuhusu haki za binadamu na kwamba Serikali haina mpango wa kuwasilisha Bungeni Sheria Na. 25 ya mwaka 2001 kwa madhumuni ya kufuta kifungu kipya cha 26(2).

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Ni kweli sheria tuliileta na tukabadilisha sisi wenyewe, lakini kwa vile tumegundua kwamba vijana wetu hawa wanateseka sana kutokana na kutopata hizi shilingi 20,000, je, kwa nini Serikali isifikirie kuleta Bungeni, ili tuweze kubadilisha kifungu hiki hatimaye waendelee kunufaika na hela hizi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Bunge ndiyo linatunga sheria hii na Serikali imesikia hilo, italitafakari na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 48

**Ukusanyaji wa Kodi/Mapato**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya makusanyo ya kodi kwa mujibu wa Wizara ya Fedha ni kwamba asilimia 80 hivi ya makusanyo yote Tanzania hupatikana Dar es Salaam kama yanavyokusanywa na Mamlaka ya Mapato *(TRA)* na asilimia iliyobaki ya makusanyo ya kodi/mapato huchangiwa kutoka kwenye eneo lote la nchi yetu, lakini wakazi wa Dar es Salaam ni asilimia 10 tu ya Watanzania wote:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeamua kukusanya kodi/mapato kwa mpangilio huo ambao hauna uwiano mzuri Kitaifa?

(b) Je, ni kiasi gani cha kodi/mapato kinachokusanywa kutoka kwenye maeneo yote ya Mijini/Jijini, kuacha Dar es Salaam na ni kiasi gani cha kodi/mapato kinapatikana kutoka maeneo yote ya vijijini?

(c) Je, kama sehemu zote mbili pia zinaweza zikaonyeshwa kama asilimia ya kodi/mapato yote ya Taifa yanayopatikana kama nilivyoeleza kwa Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stephen M. Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Kodi zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* zinatokana na vyanzo vinavyohusu shughuli za kiuchumi. Vyanzo hivyo ni pamoja na mapato ya biashara, vitega uchumi na ajira, kodi kwenye mauzo ya bidhaa na huduma na uzalishaji wa bidhaa pamoja na ushuru kwenye biashara za Kimataifa ikijumuisha ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani kwenye bidhaa zinazoingizwa kwenye maeneo ambayo shughuli za kiuchumi zinazotoa kodi hufanyika kwa kiasi kikubwa. Kutokana na vyanzo vya kodi vilivyoainishwa hapo juu, shughuli nyingi za kiuchumi hapa nchini hufanyika mijini, hususan Dar es Salaam ambapo pia ndiko kwenye Bandari Kuu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa vinavyotumika kama mlango mkuu wa biashara yetu ya Kimataifa. Ingawa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ni asilimia kumi tu ya Watanzania wote, sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi nchini, hufanyika ama hulipiwa Dar es Salaam. Hali hii inatokana na kuwepo kwa viwanda, Wizara za Serikali, Makao Makuu ya Makampuni makubwa ya ndani na Matawi ya Kimataifa, Mabenki, Makampuni ya Bima, Bandari na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa. Hali hii pia inajitokeza katika miji yetu mingine ambayo ni Makao Makuu ya Mikoa ikilinganishwa na maeneo mengine ya Mikoa husika. Kwa mantiki hii kigezo cha kiasi cha ulipaji au ukusanyaji wa kodi/mapato si idadi ya wakazi wa eneo husika peke yake bali zaidi ni shughuli za

kiuchumi zinazozalisha kodi hizo zinazoendeshwa kwenye maeneo husika pamoja na taratibu za ulipaji kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Stephen Kazi kwamba, kwa wastani asilimia 80 ya makusanyo yote ya kodi Tanzania hupatikana Dar es Salaam na asilimia iliyobaki yaani 20% huchangiwa kutoka kwenye eneo lote lililobaki la nchi yetu, lakini wakazi wa Dar es Salaam ni asilimia 10 tu. Hata hivyo, uwiano huu hautokani na Serikali kuamua kukusanya kodi kwa mpangilio huu bali ni matokeo ya mtandao wa shughuli zetu za kichumi kuwa zaidi mjini ambako wakazi wake ni wachache ukilinganisha na wa vijijini.

Hata hivyo, Serikali inafanya juhudi za makusudi za kuweka mazingira ya kuvutia na kuhamasisha wawekezaji wa nje na ndani ili wawekeze nje ya Dar es Salaam na hata nje ya miji mingine. Waheshimiwa Wabunge, wanaombwa kushawishi Halmashauri zao kutambua na kutenga maeneo ya uwekezaji na kuyatangaza ili kuhamasisha shughuli za kiuchumi na kuboresha maisha ya wakazi wa vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa miaka 2001/2002 na 2002/2003, mchango wa kodi kutoka Mijini na Vijijini ni kama ifuatavyo: Mchango wa kodi ya mapato kutoka mijini ukitoa Dar es Salaam kwa mwaka 2001/2002 ulikuwa Sh. 181.62 bilioni na Sh. 247.68 bilioni kwa mwaka 2002/2003, wakati mchango wa kodi kutoka vijijini ni Sh. 119 milioni kwa mwaka 2001/2002 na Sh. 141.1 milioni kwa mwaka 2002/2003. Kwa mwaka 2001/2002, Dar es Salaam ilichangia shilingi bilioni 759.85 ikilinganishwa na Sh. bilioni 897.9 kwa mwaka 2002/2003.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu hakuna uwiano wa moja kwa moja kati ya idadi ya wakazi wa eneo moja na kiasi cha kodi/mapato yanayokusanywa na *TRA* kama ilivyokuwa kwa kodi ya kichwa. Kutokana na uhaba wa shughuli za kichumi na biashara pamoja na hali duni ya kipato cha watu wanaoishi vijijini, mchango wa wakazi wa vijijini kwenye mapato ya kodi bado ni mdogo sana.

Mchango wao unatarajiwa kukua pale kipato chao kitakapoboreka na huduma zaidi za kiuchumi kufanyika vijijini kwa kiasi cha kuongeza mapato yao na mchango wao kwenye kodi. Hata hivyo, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Serikali kwa ujumla, inachukua hatua madhubuti za kupanua wigo wa kodi kwa kusajili na kutoza kodi wakazi wa miji mingine nje ya Dar es Salaam na maeneo yaliyo nje ya miji.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri niliyoyapata juu ya swali hili, ningependa tu kuelewa Taarifa nyingi za walipa kodi katika maeneo haya ambako wanakusanya kodi maana yake viwango viko juu sana na pia hali ya makusanyo yanakuwa yanawasonga wao peke yao. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati mzuri

kuisambaza hii kodi kwa kusisimua maeneo mengine hasa hasa kutumia mazao yetu ya biashara haya ambayo Serikali inaweza kuyasisimua yakazalishwa kwa wingi na kodi ikapanuka ili wigo upanuke zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba viwango hivi viko juu kwa sasa kwa maana kwamba, walipa kodi ni wachache na hii ni kwa sababu ya *structure* ya uchumi wetu ulivyo. Kilimo kwa kiasi kikubwa hakitozi kodi ambayo ni asilimia kubwa na wakazi wengi wapo vijijini na pia sekta isiyokuwa rasmi ni kubwa kwa hiyo sekta iliyo rasmi na ambayo inaweza kutoza kodi ibidi hawa hawa ndiyo wafuatiliwe kulipa kodi. Sasa hivi mabadiliko ya kiuchumi yanayoendelea hapa yanafanyika katika lengo la kupanua wigo na pia marekebisho ambayo yanafanyika ndani ya *TRA* yanafanya ufanisi uwe mkubwa zaidi na ambayo pia itafanya watu wanaolipa kodi waweze kuongezeka zaidi na tunatumaini kwamba, viwango hivi vitapungua katika kipindi cha miaka michache ijayo na hii pia itasaidia kuisambaza kodi ili walipa kodi watakapokuwa wameongezeka namiini pia viwango vitapungua na kodi inayotozwa kwa ujumla itaweza kuongezeka.

Na. 49

**Kiwanda cha Kusindika Matunda Morogoro**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa mapema mwaka 2001 walijitokeza wawekezaji ambao walianza kujenga kiwanda cha kusindika matunda pale Kingolwira-Mjini Morogoro lakini mradi huo uliolenga kuwakwamua wananchi wetu kwa ajira na uhifadhi wa matunda yanayolimwa kwa msimu na kuharibika umesimama:-

(a) Je, Serikali inaufahamu mradi huo pamoja na matatizo yaliyoukwamisha?

(b) Je, Serikali inatoa msaada gani kuukwamua kwa manufaa na maendeleo ya wakulima wetu wa Morogoro?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Oscar Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, ningependa kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Serikali inafahamu tatizo la uharibifu wa mazao ya shamba hasa matunda na mboga kutokana na kushindwa kwa wakulima kuyavuna na kuyafikisha kwa muda unaotakiwa kwenye masoko yanayohitaji mazao hayo.

Aidha, Serikali inaendelea kuwahimiza wajasiriamali na asasi zenye utalaamu na uwezo wa kuanzisha miradi itakayoweza kupunguza tatizo hili kwa kuwapa mafunzo ya usindikaji wa vyakula na matunda na mboga kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda

Vidogo na Biashara Ndogo Ndogo *(SIDO)* na kuwahamasisha wawekezaji kuwekeza kwenye miradi ya mazao mbalimbali kama vile matunda na mboga. Wajibu wa Serikali katika uwekezaji ni kuwatengenezea mazingira yatakayowawezesha wawekezaji kuanzisha na kuendeleza miradi yao vizuri kwa manufaa yao na Taifa zima kwa ujumla.

Baada ya maelezo haya, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mloka, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inaufahamu Mradi wa Kiwanda cha Kusindika Matunda *(Unnat Fruit Processing Ltd.),* uliobuniwa na kuanzishwa Kingolwira-Morogoro Mjini. Wakurugenzi wa Kampuni hiyo ni Rohit Shah na Nilesh Shah na baada ya kufuata taratibu zinazohusika, walipewa idhini na Serikali ya kuanzisha kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro. Ujenzi wa kiwanda hicho ulianza Oktoba, 2002 na ukasimama Aprili, 2003 kutokana na wawekezaji hao kushindwa kupata mkopo wa *USD* milioni 6 kutoka Benki ya *CRDB* kinyume na matarajio yao. Hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa majengo ya kiwanda, utawala na stoo na mgahawa ya asilimia 60 na 70 ni nzuri. Hivyo, wawekezaji tunawaasa waendelee kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili wakamilishe ujenzi wa kiwanda na kuanza usindikaji wa matunda yanayolimwa katika Tarafa za Mkuyuni na Matombo, Wilaya ya Morogoro Vijijini.

(b) Serikali hatuwezi kutoa msaada wa kifedha wa kuwakwamua hapo ila tunawasaidia kuwakutanisha na Uongozi wa Benki ya Waarabu ya Maendeleo katika Afrika *(BADEA),* ambao wameonyesha nia nzuri ya kusaidia.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Mji wa Morogoro ulibahatika kuwa na viwanda vingi vya umma vilivyojengwa miaka ya mwanzoni mwa 1980 ambavyo vilileta ajira nyingi kwa wakazi wa Mji wa Morogoro lakini ajira hizo zimeyeyuka au viwanda vimefilisika. Sasa wanapojitokeza wawekezaji kama hawa ambapo walitegemea kuajiri wafanyakazi zaidi ya 150, je, Serikali ni vema kuwasaidia kwa namna yoyote ile kuwakwamua ili ajira hizo ziweze kurejeshwa tena kuleta makusudio ambayo yalitazamiwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua umuhimu wa kuanzisha viwanda katika Mkoa wa Morogoro na ndio sababu Serikali imehakikisha kwamba, viwanda vingi vya Mkoa wa Morogoro sasa vimeanza kufanya kazi. Vile vile kiwanda hiki cha *Unnat Processing* tunakithamini sana na Serikali ndiyo iliweka jiwe la msingi pale na sasa hivi mazungumzo kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba, Waziri amejitahidi, amekwenda kuonana na Benki za Kiarabu ili kuweza kuhakikisha kwamba tunaweza kuwasaidia kuwaunganisha na hizo Benki. Kama nilivyosema, tayari mazungumzo yamekwishaanza na nia ni nzuri au matumaini yapo.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Kwa kuwa wawekezaji hawa walihamasisha watu walime sana matunda na wakulima wakaitikia kulima mazao hayo. Sasa Serikali itawasaidia hawa

wafanyabiashara wadogo wadogo kuwakopesha mikopo midogo midogo kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ili wasipate hasara kwa mazao waliyolima?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kabisa kuwasaidia wakulima waliolima matunda au mboga kwa ajili ya kusindika na ninaomba sana Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wa Mkoa wa Morogoro, ambao wako katika eneo lililolimwa matunda, wawasiliane na Meneja wa *SIDO* katika Mkoa wa Morogoro ili kuweza kuhakikisha kwamba, wanapata mikopo midogo midogo ya kusindika matunda na mboga hizo. *(Makofi)*

Na. 50

**Mpango wa *EPZ* - Mkoa wa Kigoma**

**MHE. FRANK M. MUSSATI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma umewekwa katika mpango wa *EPZ,* mara tu baada ya sheria ya kuanzisha maeneo hayo kupitishwa Bungeni karibu miaka miwili iliyopita:-

(a) Je, hadi leo ni wawekezaji wangapi na katika nyanja zipi wameonyesha nia ya kuwekeza katika mkoa huo?

(b) Je, ni matatizo gani yanawazuia wawekezaji mkoani Kigoma na Serikali inachukua hatua gani kuyaondoa matatizo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussati na Mheshimiwa Wegga, wananipa shida kuwaona. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frank Mussati, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa Sheria ya *EPZ* ilipitishwa miaka miwili iliyopita, hata hivyo, utekelezaji wake ulianza rasmi Mei, 2003 mara baada ya shughuli ya kutayarisha kanuni na taratibu za usimamizi wake kukamilika. Ni dhahiri kwamba, kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa sheria hii ni kifupi kuwezesha kufanyika kwa tathmini sahihi kuhusu ufanisi wake kwa nchi nzima.

Kuhusu utekelezaji wa Progrmu ya *EPZ* Mkoani Kigoma, kazi zilizokwisha fanyika mpaka sasa ni pamoja na kubaini maeneo ambayo yangefaa kuendelezwa kwa ajili ya shughuli za *EPZ.* Aidha, uongozi wa mkoa kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali katika kusimamia programu ya *EPZ*, yaani Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* na kampuni mwekezaji na mshauri ya *IPROP* ya Afrika Kusini, wameanza kubainisha fursa za uwekezaji zinazoweza kutangazwa na hivyo kuvutia wawekezaji katika maeneo ya *EPZ* Mkoani Kigoma. Fursa zinazoelekea kuwa msingi wa maeneo ya *EPZ* Mkoani

Kigoma ni pamoja na utajiri mkubwa wa mazao ghafi ya kilimo na biashara ya upitishaji mizigo *(Transit Trade).*

(b) Wapo wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza kwa kuanzisha maeneo ya *EPZ* mjini Ujiji/Kigoma wakilenga masoko ya nchi za Maziwa Makuu ya Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Kaskazini mwa Zambia. Hata hivyo, hadi hivi sasa hakuna mwekezaji yeyote ambaye ameshafikia hatua rasmi ya kuwekeza mkoani humo chini ya mpango wa *EPZ*. Juhudi zinaendelea za kuwawezesha wawekezaji hao kuanzisha uwekezaji katika *EPZ* mjini Ujiji/Kigoma. Aidha, Serikali inaendelea na juhudi za kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu ya uhakika kama kivutio muhimu kwa wawekezaji. Serikali inatoa wito kwa uongozi na wananchi wa Mkoa wa Kigoma, kuandaa warsha juu ya fursa na uwekezaji Mkoani Kigoma kama ile iliyofanyika Moshi, Kilimanjaro.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Nataka kumwuliza swali moja tu, je, yeye Mheshimiwa Waziri anaona inawezekana kuwekeza kwa mpango wa *EPZ* kwenye eneo ambalo halina umeme? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo linahusu Wizara ya Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, umeme ni nyenzo muhimu sana kwa kuleta maendeleo na ni nyenzo muhimu sana kwa ujenzi wa viwanda vyetu. Ni kwa sababu hiyo basi, Serikali imekuwa inafanya kazi ya kuhakikisha kwamba ile Mikoa ambayo haina umeme wa uhakika ukiwemo Mkoa wa Kigoma unapata umeme wa uhakika. Kazi hiyo, tumekuwa tunaifanya na hapa Bungeni nimewahi kutoa taarifa.

Kwa mfano, kwa Mkoa wa Kigoma ambapo hatua ya kwanza muhimu ni ile ya kuhakikisha kwamba njia ya kupelekea umeme inayotoka Tabora hadi Urambo inakuwa ni njia kubwa badala ya njia 33 na hivi tunavyozungumza ni kwamba, majadiliano yanaendelea kuhakikisha kwamba njia hii inakuwa ni kubwa na tunafanya hivyo bila kuathiri kupeleka umeme kule Urambo na Kaliua ili kuhakikisha kwamba Kigoma itakapofika wakati muafaka, ipate umeme na sehemu nyingine zipate umeme.

Mheshimiwa Spika, kuthibitisha juhudi za Serikali, hapo nyuma katika Mikoa hii tumekuwa tukizungumzia pia Mkoa wa Ruvuma. Hivi tunavyozungumza tayari fedha zimeshapatikana za kujengea *Sub-Station* pale Makambako, ambayo ni chanzo muhimu cha kupitishia umeme Mkoa wa Ruvuma. Jitihada hizi hizi ndizo zinazoendelea kwa Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali kuhusu majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Majibu yake ameelezea kwamba, miundombinu bado inaleta matatizo na uwekezaji. Ndiyo sababu mojawapo aliyoielezea hiyo. Je, haoni suala la barabara nalo ni kigezo kibaya zaidi ya alichokisema kwamba kinawakwamisha

wawekezaji kuweza kuleta *investment* kule kwa Mkoa ule ambao tangu zamani tunategemea tu barabara iliyojengwa na Mjerumani; je, unaweza kumwambia Waziri wa Ujenzi ili tupate hiyo barabara ya lami kutoka hapa mpaka Kigoma ili tupate maendeleo kama wengine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo linahusu Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, kweli kabisa miundombinu ni moja ya kigezo muhimu cha kuleta maendeleo mahali popote pale na ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, upo umuhimu wa kupata barabara ya lami kuelekea Kigoma, lakini Mheshimiwa Mbunge anajua jitihada zetu tunazozifanya kwa sababu alikwishafika Ofisini kwangu zaidi ya mara 10 na tumekwishajadiliana na anajua hatua ya Wakandarasi waliopo kule sasa hivi katika barabara ya Manyovu - Mwandiga. Kwa hiyo, ni jitihada ya Wizara ya Ujenzi, kwa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba, mikoa isiyounganishwa kwa barabara za lami inafanyiwa hivyo kabla ya mwaka 2007. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Kwa kuwa tatizo kubwa lililopo ni ule muunganisho wa mikoa na hizo nchi zinazozungumzwa *(linkage)* kati ya Kigoma kuja Tabora, Kigoma kwenda Bukoba na Mwanza na si kutoka Kigoma kwenda Manyovu ambacho ni kibarabara kilichomo ndani ya Mkoa. Je, Wizara hii inasema nini kuhusu kutuletea hiyo *linkage* kati ya Mkoa na Mkoa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishatamka kwamba, Serikali inafanya makusudi kabisa katika Sera ya Barabara na Miundombinu kuunganisha Mikoa yote ya Tanzania ambayo haijaunganishwa kwa lami hivi sasa ifikapo 2007 yote iwe imefanyiwa hivyo.

Na. 51

**Ugawaji wa Viwanja Jijini Dar es Salaam**

**MHE. SOPHIA M. SIMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa viwanja 20,000 vimepimwa na kugawiwa kwa wananchi katika Jiji la Dar es Salaam na kwa kuwa Manispaa za Jiji hilo zina haki ya kujua ni mambo gani yanayofanyika katika maeneo yake:-

(a) Je, Serikali inaweza kusema ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kwa kila Manispaa?

(b) Je, Manispaa tatu za Jiji hilo zimefaidikaje na zoezi zima la upimaji viwanja?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Machi, 2004 jumla ya Sh.15,984,512,000 zimepatikana kutokana na gharama za kulipia viwanja na makusanyo ya ada zilizotokana na kulipia fomu za maombi ya kupewa viwanja.

Kiasi cha fedha kilichokusanywa kwa kila Manispaa ni kama ifuatavyo:-

(i) Mauzo ya viwanja vilivyolipiwa kikamilifu na vinavyoendelea kulipiwa kwa awamu ni jumla ya Sh.15,957,990,000 zilikusanywa. Katika Manispaa ya Kinondoni zilikusanywa Sh.10,685,290,000, Manispaa ya Temeke zilikusanywa Sh.4,872,000 na Manispaa ya Ilala Sh.399,980,000.

(ii) Mauzo ya fomu za maombi ya kugawiwa viwanja ya Sh.2,000 kila fomu, jumla ya zilikusanywa Sh.26,522,000.

(iii) Katika Manispaa ya Kinondoni zilikusanywa Sh.16,078,000, Manispaa ya Temeke zilikusanywa Sh.8,444,000 na Manispaa ya Ilala ni Sh.2,000,000.

Mapato hayo yamewezesha kulipa asilimia 75 ya gharama za mradi, ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 21.5. Fedha hizo zimetumika katika kutekeleza kazi mbalimbali zikiwa ni pamoja na ulipaji wa fidia, ununuzi wa vifaa vya upimaji, upimaji wa viwanja na uchongaji wa barabara.

(b) Mheshimiwa Spika, manufaa yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mradi wa kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam kwa Manispaa zote tatu na kwa wananchi wengine nje ya Jiji ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, jumla ya viwanja 23,000 vya makazi na viwanja 4,000 kwa ajili ya huduma mbalimbali vimezalishwa. Viwanja hivyo, vitakapoendelezwa vitapunguza msongamano wa watu katikati ya Jiji kwa kuwa, huduma zote zimeelekezwa kwenye maeneo ya mradi na ujenzi holela katika maeneo yasiyopimwa utapungua.

Pili, mradi umesaidia kuziba mianya ya rushwa katika utoaji wa viwanja, ulipaji wa fidia na utoaji wa hati kwa kuwa wananchi wanapta viwanja katika utaratibu ulio wazi.

Tatu, mapato ya Serikali yataongezeka kutokana na kukusanya kodi ya pango la ardhi *(Land Rents)* na kodi ya majengo *(Property Tax).*

Nne, mradi umetoa ajira kwa watu wengi, kwa mfano, wakati wa uthamini na upimaji wa viwanja, vijana waliajiriwa kama vibarua ili kuwasaidia wataalam kufyeka misitu, kukata miti na kupima. Mama lishe nao walipata ajira ya kutoa huduma ya chakula kwa watu waliokuwa wanafanya kazi hizo.

Tano, wananchi wenye maeneo yaliyotwaliwa ambayo mengi yao yalikuwa yametelekezwa au yalikuwa hayalimwi kwa faida, wamelipwa fidia itakayowawezesha kuanzisha miradi yenye tija.

Sita, kampuni binafsi za uthamini, wapimaji na wazabuni wa barabara, walipatiwa kazi na kila kampuni imetoa ajira kwa kiwango chake na pia soko la vifaa vya ujenzi limeongezeka na hivyo kuwanufaisha wazalishaji na waagizaji wa vifaa hivyo.

Mwisho, kwa kuwa Wizara yangu imekuwa ikishirikiana kwa karibu sana na Manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam na taarifa hizi zote wanazo, ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenyewe wote wa Dar es Salaam, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na kushauriana na Manispaa zote, jinsi ya kufanikisha zoezi hili kwa manufaa ya wakazi wote wa Jiji la Dar es Salaam na Tanzania nzima kwa jumla.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri ambayo yanazungumzia viwanja 20,000 na nimeridhika. Lakini nina maswali mengine mawili madogo nayo ni:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria Wizara inawajibika kugawa 20% ya *Land Rent;* na kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake zina majengo mengi na wanalipa pesa hizo; na kwa kuwa kwa mara ya mwisho Wizara imelipa mgao huo mwaka 1995; je, Wizara itatuambia ni sababu gani inafanya asilimia hizo zisilipwe kwenye Halmashauri?

La pili, kwa kuwa *Land Rent* ni kianzio kimoja kikubwa katika Manispaa zetu ambazo zina majukumu mengi. Je, Wizara itakuwa tayari kutamka hapa kuwa itafuata utaratibu na hasa ni Sheria ya kulipa 20% zote ambazo zinalipwa za *Land Rent* na hivyo kuisaidia Halmashauri ya Dar es Salaam na Wilaya zake kuweza kutekeleza miradi yake mbalimbali hapo Jijini mojawapo ikiwa ujenzi wa Shule za Sekondari katika Kata mbalimbali zikiwemo Vijibweni, Pemba Mnazi, Somangila...

**SPIKA:** Swali limeeleweka sikiliza majibu sasa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria kweli fedha za kodi ya ardhi, 20% zinarudi kwenye eneo ambako zimekusanywa. Lakini nakuhakikishia kabisa labda hukufuatilia katika Halmashauri, wanalipwa kila mwaka. Wanachukua 20% yao. Labda rekodi za Manispaa hujazikagua. Lakini nakuhakikishia kwamba, kila mwaka wanalipwa na wala siyo Mkoa wa Dar es Salaam peke yake ni nchi nzima. Kukawia kwake ni jinsi tu ya kuleta Wizarani pengine katika kurudisha inaweza kuwa kuna dosari zimefanyika katika mahesabu. Lakini kila mwaka wanatakiwa lazima warudishiwe 20% zao.

Swali la pili kwamba kurudisha kwa haraka juu ya kufanikisha kwa miradi mbalimbali ya Halmashauri na naomba nieleze dhahiri kwamba 20% zinazorudi katika Wilaya si kwa manufaa ya kazi zingine zozote zaidi ya Ofisi ya Ardhi na kama zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari, kukarabati sijui majengo gani, wanakiuka Sheria ambayo imewekwa katika matumizi ya fedha hizi. Kwa hiyo, wale wanaotumia vibaya itabidi wawajibishwe kwa sababu hawaruhusiwi. Zinarudishwa kwa ajili ya ukarabati maeneo ya Ofisi yao, kupata pembejeo, kufanikisha kazi za ardhi na si vinginevyo.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa viwanja vinagawiwa kwa wananchi na wananchi wameshavilipia; na kwa kuwa bomba la maji linapita katika viwanja vichache katika sehemu ile ya Mbweni, Kinondoni; je, Wizara ina mikakati gani kuwaarifu wahusika ili wasijenge na baadaye kuvunjiwa kwa sababu ya bomba hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama kuna maeneo yoyote yamepimwa viwanja sehemu zinapita nyaya za umeme, mabomba ya maji au kuna vifaa maalum pengine vya baruti, mara moja aliyepewa kiwanja atoe taarifa kwa wahusika. Hairuhusiwi kujenga nyumba katika maeneo ambayo kunapita vifaa kama hivi. Kwa hiyo, kama kweli kuna watu wa namna hiyo, waripoti katika Ofisi ya Mipango Miji Wilayani halafu watashughulikiwa, ikishindikana Wizara iko tayari kusaidia.

Na. 52

**Nauli kwa Wanafunzi**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA (k.n.y. MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya sabini, vyombo vyote vya baharini vilikuwa vikitoza nauli nusu kwa wanafunzi. Je, utaratibu huo unaendelea mpaka hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika miaka ya sabini takribani vyombo vyote vya baharini vilikuwa vikitoza nauli nusu kwa mwanafunzi. Vyombo hivyo hasa vilikuwa ni meli za Serikali zilizokuwa zikiendeshwa na Mashirika ya Umma kama vile Kampuni ya Meli ya Mwambao Tanzania *(TACOSHILI),* kwa upande wa usafirishaji baharini na Shirika la Reli Tanzania, kwa upande wa usafirishaji katika Maziwa ya

Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, kwa upande wa Serikai ya Mapinduzi Zanzibar, meli zilizokuwa zikitoa huduma zilikuwa za Shirika la Meli Zanzibar, zikitoa huduma kati ya Zanzibar na Pemba. Hii iliwezekana kwa sababu kwa mujibu wa Sheria zilizounda Mashirika hayo ya Umma, Waziri anayesimamia shughuli za uchukuzi alikuwa na madaraka ya kuelekeza juu ya viwango vya nauli. Kwa mfano, ibara ya 13(1)(b) ya Sheria ya Shirika la Reli Tanzania ya mwaka 1977, inampa Waziri wa Uchukuzi madaraka kama hayo.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Mashirika haya ya Umma ulipoanza kulegalega, Serikali iliingia Mikataba ya utendaji ili kuinua viwango vya ufanisi. Mikataba hiyo inayataka Mashirika husika yajiendeshe kibiashara na wakati huo huo Serikali kutoingilia utendaji wao. Ndani ya Mikataba hiyo, Serikali haitakiwi kuingilia shughuli za kiutendaji. Iwapo itafanya hivyo na kusababisha hasara, basi hasara hiyo inapaswa kufidiwa na Serikali. Pamoja na Serikali kutojihusisha na kupanga bei, matokeo ya biashara ya ushindani yameanza kuleta matumaini mazuri kwa sekta ya uchukuzi. Aidha, hakuna ongezeko kubwa la nauli kwa aina zozote za njia ya uchukuzi na watu binafsi wameendelea kutoza nusu ya nauli ya mtu mzima kwa watoto na wanafunzi, hasa kwa usafiri wa meli kati ya Dar es Salaam na Zanzibar na huduma za usafiri zinazotolewa mijini na mabasi. Hata hivyo, mwanafunzi anapaswa kuonyesha kitambulisho chake ili aweze kupata unafuu huo.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa hata kwenye mabasi ya Daladala Dar es Salaam, Serikali imeingilia na wanafunzi wanalipa nusu nauli kwa nini na kwenye ndege wasiendelee kulipa nusu nauli?

(b) Kwa sababu tatizo mojawapo ambalo hufanya wanafunzi kuchelewa kufika shuleni na wengine kukosa kabisa kwenda shuleni ni nauli, je, Serikali haifikirii njia yoyote ile ya kufuta nauli za wanafunzi ili waweze kusafiri bure hasa kwa wale wanaokwenda mbali?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nauli kwa wasafiri wanafunzi kuna kiwango maalum na miaka maalum, wanaosafiri kwa ndege wanapewa nauli ya nusu na hiyo inafanyika hadi hii leo.

Mheshimiwa Spika, kufuta kabisa nauli kwa wanafunzi sidhani kama litakuwa ni jambo la busara. Tuchukue mfano mdogo tu, tunapokwenda kula hotelini hatusemi huyu ni mwanafunzi alipe robo na wewe ni mtu mzima ulipe *full* na katika ushindani huu wa biashara, nauli inapangwa na soko lakini Serikali inaingilia kati pale hali itakapokuwa haimruhusu.

Mheshimiwa Spika, labda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, shule nyingi hivi sasa baada ya Kamati za Wazee kukaa, wamekubaliana kwamba, wanafunzi

wanawakodishia mabasi yao inakuwa ni *convenient* kwa wanafunzi kufika shuleni kwa haraka zaidi. Niombe tu Kamati za Shule, ziendelee na juhudi hizo na kuwashawishi wananchi waone umuhimu wa kusaidia sekta ya uchukuzi ili mtoaji huduma afaidike na yule ambaye anapewa huduma ile afaidike.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, nina swali la nyongeza. Pamoja na kwamba Serikali haitaki kuingilia utendaji wa vyombo hivi vya binafsi, Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia nini kuhusiana na vyombo tulivyonavyo hivi sasa ambavyo vinachukua watu zaidi ya kiwango kinachotakiwa na tunajipanga katika vyombo vile vinavyokwenda Zanzibar kama tumo katika Daladala?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme ni kinyume cha taratibu tulizoziweka kwa vyombo vya usafiri kupakiza zaidi ya idadi ambayo inapaswa kuchukua. Nachukua nafasi hii kusema kwamba, wasafirishaji wote wanaosafirisha abiria kwa njia ya meli, nawaomba waache kabisa mtindo huo. Kufanya hivyo ni kinyume cha taratibu na ikibainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi tuna *regular reports* ambazo tunapata kutoka kwa wasafirishaji na wasimamiaji wa shughuli hizi za usafiri wa majini na kila wiki tunapewa ripoti hizo, abiria wangapi wamesafiri na kila chombo kinachoondoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Lakini kama hilo linafanyika, tutalishughulikia ipasavyo.

Na. 53

**Tatizo la Mchanga katika Bandari ya Lindi**

**MHE. MOHAMMED A. ABDULAZIZ** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1997, Serikali iliondoa mchanga katika njia ya meli kwenye Bandari ya Lindi lakini bado tatizo hilo linaonekana sasa kwenye eneo la bandari ambapo meli zinashindwa kufunga gati kutokana na kina kidogo cha maji kilichosababishwa na kujaa mchanga kwenye eneo hilo:-

(a) Je, kazi ya kuondoa mchanga kwenye njia ya meli iligharimu fedha kiasi gani na je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa mchanga uliojaa kwenye eneo la maegesho ya meli ili kuziwezesha kufunga gati bila matatizo?

(b) Je, Serikali imeshafanya utafiti wa aina yoyote ili kufahamu sababu za kuongezeka kwa mchanga katika eneo la maegesho ya meli na sababu hizo ni zipi?

(c) Kama jibu katika sehemu (b) ya swali hili ni ‘Hapana” je, Serikali iko tayari kufanya utafiti huo na itafanya hivyo lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuondoa mchanga kwenye njia ya meli hadi kwenye gati ilifanyika mwaka 1998 na iligharimu kiasi cha Sh.1.3 bilioni, hata hivyo, mchanga ulijaa tena.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya kujaa mchanga tena, Serikali inafanya utafiti ili kubaini sababu za mchanga kujaa kwenye gati kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili. Utafiti unafanywa na Timu ya Wataalam wa Mamlaka ya Bandari. Moja ya kazi ya Timu hiyo ni kutayarisha michoro kwa ajili ya kujenga vizuizi vya mchanga kujaa na kazi ya kuondoa mchanga na ujenzi wa vizuizi itaanza mara baada ya kazi hiyo kukamilika.

**MHE. MOHAMMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa ujenzi wa awali wa Bandari ile uliacha nafasi kule chini kuruhusu maji kupita na mwaka 1980 ule uwazi ulizibwa na kuanzia pale ndio tatizo la mchanga likajitokeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubali ushauri wangu kwamba yale mawe yaliyoziba yaondolewe ili kuruhusu maji kupita kama zamani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, labda niseme kwamba, Wataalam niliozungumza nao katika fani hii, niliwauliza swali hilo hilo ambalo wewe umenipa mimi leo na wakaniambia kwa utaalam wao hilo lisingeweza kuwa ni tatizo la kujaa mchanga. Lakini kwa sababu utafiti utafanywa, utagundua chanzo na sababu ya mchanga kujaa katika Bandari ya Lindi. Nikuombe Mheshimiwa Mbunge, uwe na subira na ustahamilivu ili tuwape nafasi wataalam wafanye shughuli hiyo ipasavyo.

Na. 54

**Kituo cha Utafiti wa Mifugo na Mafunzo Kanda ya Kati**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Utafiti wa Mifugo na Mafunzo cha Kanda ya Kati kina vituo vinne yaani Mpwapwa, Kongwa, Hombolo na Makutupora; na kwa kuwa majengo ya Kituo cha Utafiti cha Hombolo yamechakaa na yanahitaji ukarabati mkubwa na kupatiwa vitendea kazi vya kutosha:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyafanyia ukarabati majengo hayo kwa lengo la kuimarisha kituo hicho?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia vitendea kazi vya kutosha kama vile magari, matrekta, pikipiki, kompyuta na kadhalika ili kuboresha shughuli za utafiti katika Chuo cha Hombolo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka simu ili kuboresha mawasiliano katika kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Utafiti wa Kilimo na Mifugo hapa nchini unasimamiwa kwa pamoja na Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo chini ya Mradi wa Utafiti wa Kilimo *(Tanzania Agricultural Research Project Phase II).* Chini ya mradi huo, utafiti umegawanywa katika kanda 7. Mojawapo ya Kanda hizo ni Kanda ya Kati yenye Makao Makuu katika Taasisi ya Utafiti wa Uzalishaji Mifugo Mpwapwa. Vituo vinavyosimamiwa na Mpwapwa ni Kituo cha Utafiti wa Malisho Kongwa, Kituo cha Utafiti Hombolo na kile cha Makutupora.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Hombolo majengo yake ni machakavu, kina uhaba wa vitendea kazi pamoja na ukosefu wa simu. Hali hii pia ipo katika vituo vingine vya utafiti hapa nchini. Ili kuviweka vyuo na taasisi za utafiti katika hali nzuri, Serikali ina mpango unaoendelea wa kufanyia ukarabati majengo katika vituo vyote vya utafiti kikiwemo hiki cha Hombolo. Kasi ya ukarabati wa vituo hivyo inategemea sana na jinsi gani tunapata fedha kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa vitendea kazi katika Vituo vya Utafiti, Serikali kupitia mpango wa *TARP II,* imekipatia Kituo cha Utafiti Hombolo, *computer* 2, pikipiki 2, jenereta 1 na pampu ya maji katika kipindi cha mwaka 2000 na 2003. Serikali pia itaendelea kuvipatia vituo vyake vyote vitendea kazi vya kutosha kulingana na uwezo uliopo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kwa jitihada zake za kuona hali ya Kituo hiki inakuwa nzuri na napenda aendelee kufanya hivyo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza kabisa, napenda niipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri iliyofanyika ya kukarabati Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa pamoja na Chuo cha Mifugo. *(Makofi)*

(a) Pamoja na majibu mazuri kwamba atawapatia vitendea kazi, je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa tayari kuwapatia usafiri kwa sababu vituo hivi vina tatizo la usafiri?

(b) Kwa kuwa Serikali ilikuwa na utaratibu wa kutoa *Field Allowance* kwa Vyuo vya Mifugo na utaratibu huu sijui ukoje kwa vile hivi sasa fedha hizi hazitolewi, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuwapatia fedha za *Field Allowance* kwa ajili ya *field practical* hao Wanachuo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naelewa hamu ya Mbunge na Watanzania wote ni kuona hali ya Vyuo vyetu ikiwa nzuri, juzi na sio leo au kesho. Kwa hiyo, napenda nirudie jibu langu kwamba, fedha tunapozipata ndipo tunapozipeleka ili kupunguza matatizo ambayo yamekuwa ni ya muda mrefu na sasa hivi tuko mbioni kuyarekebisha ili Vyuo vyetu viwe katika hali inayokubalika Kitaifa na Kimataifa. Kwa hiyo, napenda tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge kuona kwamba, tunapata fedha kutoka sehemu mbalimbali ambapo tunaweza ili kusaidia kurekebisha Vyuo hivi.

Na. 55

**Matokeo ya Mitihani ya *Form II* Kucheleweshwa**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA (k.n.y. MHE. ESTHERINA KILASI)** aliuliza:-

Kwa kuwa wanafunzi wa Kidato cha Pili hufanya mitihani ya kuingia Kidato cha Tatu na kwa kuwa matokeo ya mitihani hiyo huchelewa kutoka kwenye baadhi ya Kanda, hali ambayo husababisha wanafunzi kuingia Kidato cha Tatu kabla ya matokeo kutoka.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka utaratibu utakaowezesha kufanya mitihani pamoja na kutoa matokeo kwa wakati mmoja kwa kanda zote kama ilivyo kwenye mitihani ya Kidato cha Nne ili kuondoa usumbufu unaowapata wanafunzi na wazazi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, kabla ya kujibu swali hili, naomba nitambue kuwepo hapa Bungeni na muda mchache uliopita walikuwemo humu ndani, Walimu 40 na Wanafunzi 80 wa Shule za Msingi...

**SPIKA:** Kazi ya kutambua wanaokuja Bungeni ni ya Spika, endelea kujibu swali tu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Naomba radhi.

**SPIKA:** Watanzania hawatambuliwi, ni haki yao kuja hapa Bungeni. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeweka utaratibu wa kuendesha Mtihani wa Kidato cha Pili Kitaifa kwa kupitia Kanda za Ukaguzi wa Shule mwezi wa 11 kila mwaka na matokeo ya mtihani huo yanatakiwa yatolewe kabla ya tarehe 15 Januari ya kila mwaka katika Kanda zote sambamba na tarehe za kufungua shule ili kuweza kubaini wanafunzi watakaoendelea na Kidato cha Tatu na wale watakaolazimika kukariri Kidato cha II. Kwa mwaka huu, hadi tarehe 15 Januari, 2004 Kanda zote zilikuwa zimekwishatoa matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Pili uliofanyika Novemba, 2003 na Shule za Sekondari zilifunguliwa kati ya tarehe 15 Januari, 2004 na 19 Januari, 2004. Kwa hiyo, kasoro ya kuchelewa iliyowahi kutokea imerekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Mitihani wa Kidato cha Pili unalenga kupima kiwango cha Maarifa na ujuzi alioupata mwanafunzi kutokana na masomo aliyojifunza katika miaka miwili ya kwanza ya Elimu ya Sekondari. Katika mitihani huu, kiwango cha kufaulu ni wastani wa asilimia 30. Mwanafunzi anayepata wastani wa alama asilimia 30 au zaidi anaendelea na Kidato cha Tatu na mwanafunzi anayepata chini ya alama hiyo anakariri Kidato cha Pili. Maendeleo ya matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Pili kuanzia mwaka 2001 hadi 2003 ni kama ifuatavyo:-

| **Mwaka** | **Waliofanya** | **Waliofalu** | **Asilimia** | **Alama ya Kufaulu Mtihani** |
|---|---|---|---|---|
| 2001 | 84,781 | 68,000 | 80.3% | 26 |
| 2002 | 105,000 | 72,000 | 71.6% | 30 |
| 2003 | 115,680 | 80,000 | 70% | 30 |

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuhakikisha kuwa utaratibu huu unazingatiwa na matokeo yanatoka katika wakati uliopangwa katika Kanda zote ili kuepukana na uchelewaji uliowahi kutokea na kusababisha Mheshimiwa Mbunge kuuliza swali hili.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa iliwahi kutokea kuchelewesha matokeo na wanafunzi wakaingia Kidato cha Tatu na baadaye baadhi yao kuambiwa hawakupata sifa; na kwa kuwa jambo kama hili linaweza kutokea tena; je, wale wanafunzi ambao wameshalipa ada hurudishiwa na wale waliopata mkasa ule walirudishiwa ada zao?

(b) Kwa kuwa Mitihani ya Kidato cha Pili imekuwa ikiendeshwa kwa muda mrefu, kwa mtazamo wa Serikali kumekuwa na manufaa yoyote katika kuboresha elimu yetu hapa Tanzania?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba yule aliyekwisha kwenda Kidato cha Tatu akalipa ada, je, anarejeshewa? Kusema kweli hakuna sababu ya kurejeshewa kwa sababu kama nilipojibu swali la msingi, yule ambaye hakufaulu anakariri kwa hiyo ile ada aliyolipa kwa ajili ya Kidato cha Tatu itatumika kwa ajili ya mwaka wake wa kukariri katika Kidato cha Pili. Kwa hiyo, halipo tatizo lolote hapo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, kumekuwa na manufaa yoyote kutumia Mtihani wa Kidato cha Pili kukariri? Ukweli ni kwamba manufaa yamejitokeza vizuri sana. Kwanza wanafunzi wameongeza sana jitihada ya kujifunza na Walimu wameongeza sana jitihada ya kufundisha Kidato cha Kwanza na cha Pili badala ya kukaa wakitegea mpaka wanapofika mtihani wa Kidato cha Nne. Kwa wale ambao wamekwenda Kidato cha Tatu kwa kufaulu mtihani wa Kidato cha Pili, manufaa yamejitokeza vizuri sana katika mitihani ya Kidato cha Nne ukilinganisha mwaka jana na mwaka juzi kufaulu katika madaraja III,II na I kumeongezeka kutoka 36% mpaka 45% katika Shule za Serikali. Kwa hiyo, hayo ni manufaa yaliyo dhahiri ambayo yamejitokeza katika matokeo ya mitihani.

Na. 56

**Shule za Sekondari za Kutwa**

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO (k.n.y. MHE. MARIA D. WATONDOHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la kuanzisha Shule za Sekondari za Kutwa ni kusogeza Elimu ya Sekondari kwa wananchi na kuongeza nafasi ya wasichana kupata Elimu ya Sekondari:-

(a) Je, lengo hilo bado lipo; na kama lengo limebadilika, ni sera zipi zilizotumika kubadilisha lengo hilo?

(b) Kama malengo hayajabadilika; je, Serikali itakuwa tayari kuendeleza mpango huo na kuweka mikakati endelevu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha Shule za Kutwa zilizo karibu na wananchi bado halijabadilika na linaendelea kutekelezwa. Aidha, Shule zote za

Sekondari za Kutwa za Serikali zinachukua wanafunzi wasichana na wavulana kwa idadi inayolingana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhimiza ujenzi wa Shule za Sekondari za Kutwa karibu na wananchi kila mahali ambako kuna Shule za Msingi zenye wanafunzi wa kutosha kujaza Shule hizo za Sekondari. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* 2004 -2009 unaotarajiwa kuanza baadaye mwaka huu, utaainisha mikakati, idadi na maeneo ya kujenga shule hizo zinazochukua idadi sawa ya wanafunzi wasichana na wavulana. Aidha, Waraka wa Elimu Na.3 wa mwaka 2002 uliotolewa na Afisa Elimu Kiongozi kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, uliwapongeza wananchi kwa jitihada wanazofanya katika kuanzisha Shule za Sekondari za Kutwa na kuwahimiza waendelee na jitihada hizo. Waraka huu uliwataka Makatibu Tawala wa Mikoa waendelee kuratibu zoezi hilo na kuwasilisha taarifa za idadi ya shule zinazotarajiwa kuanzishwa katika Mkoa mwaka mmoja kabla ya ufunguzi yaani kabla ya tarehe 31 Januari ya mwaka unaotangulia.

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kushauri kila Mkoa na kila Wilaya, waandae mpango wao wa elimu ya sekondari wenye lengo la kupeleka sekondari 50% ya watahiniwa wa Darasa la Saba ifikapo mwaka 2009 kwa usawa baina ya wavulana na wasichana na kwa kujali maeneo mbalimbali katika Wilaya hiyo, chanzo kabisa ikiwa ni ngazi ya Kata.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya swali hilo lakini pamoja na majibu haya nataka kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Ni lini hasa Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari utaanza na kwa namna gani?

(b) Utakumbuka ulitakiwa kufanya ziara Mkoa wa Lindi mwaka jana, je, uko tayari kufanya ziara mwaka huu mapema iwezekanavyo na hususan Liwale?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, lini Mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari 2004 -2009 utaanza? Jibu ni kwamba, mpango huu hasa umeanza mwaka huu kwa maana ya kwamba katika uandikishaji wa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, Wizara yangu ilitoa maelekezo kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kwamba, mwaka huu tuchukue wanafunzi wengi zaidi Kidato cha Kwanza kati ya Januari na Machi hata kama watazidi namba inayohitajika kwa kujua mpango wenyewe hasa kibajeti unakuja kuanzia bajeti inayoanza tarehe 1 Julai, 2004. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba, mpango huu umeanza kwa sababu mwaka huu tumechukua Kidato cha Kwanza 40% zaidi ya wale tuliowachukua mwaka jana na katika bajeti itakuwepo ruzuku ya maendeleo na ruzuku ya uendeshaji wa shule kwa kuwasaidia wananchi ujenzi wa madarasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba mwaka jana niliahidi kwenda Mkoa wa Lindi na hususani Wilaya ya Liwale, nakiri kabisa lakini kutokana na wingi wa

kazi na mipango iliyokuwepo haikuwezekana. Mara moja nilishapanga kwenda kabisa lakini ikabidi kuahirisha kwa sababu kulikuwa na ratiba ya Mheshimiwa Makamu wa Rais kwenda huko nikaona sio vizuri kuwa na ratiba ya Waziri na Makamu wa Rais wakati huo huo. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitatilia maanani suala hili, hili ni deni ambalo nalikubali na napenda kabla ya mwisho wa mwaka huu niwe nimeshatembelea Mikoa yote ikiwemo Mkoa wa Lindi, namshukuru sana kwa kunikumbusha.

**SPIKA:** Kwa kuwa umemaliza maswali yako Mheshimiwa Waziri, naomba nikuombe radhi kwa kukukatisha pale ulipotaka kuwatambulisha Walimu wako. Naomba radhi sana lakini Spika alikuwa na taarifa kwamba, wapo Walimu na Wanafunzi na yupo Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Kurekebisha Sheria kwenye *gallery* kule juu, lakini kama nilivyoeleza, utaratibu wetu huwa tunapenda kuwatambulisha wageni wa Kimataifa wanaoomba ruksa kuja Bungeni na tunawapa ruksa lakini Watanzania hawaombi ruksa wana nafasi ya kuja wakati wowote wanapotaka, ni haki yao. Ndio utaratibu tuliouweka. Kwa hiyo, tunawakaribisha wale wote waliokuja leo na watakaokuja kesho mpaka tutakapomaliza Bunge hili, Watanzania wanaopenda kuja kusikiliza mijadala ya Bunge wanakaribishwa. Naomba radhi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 57

**Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Singida**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Singida tayari imekubali ombi la Wilaya ya Iramba kuwa barabara itokayo Shelui - Mtoa - Mtekente - Urughu mpaka Kibaya na ile itokayo Kiomboi - Kisiriri - Kidaru - Ibaga mpaka Kidarafa ziondolewe kutoka Wilayani ili ziwe barabara za Mkoa kihuduma:-

(a) Je, Serikali ina sababu gani za kucheleweshwa maamuzi ya Bodi ya Barabara Mkoa wa Singida, kwani mpaka sasa Wizara haijaidhinisha maamuzi hayo?

(b) Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Vijiji na Kata ambapo barabara hizo zinapitia kuwa kuanzia bajeti ya 2004/2005 zitaanza kuhudumiwa na Mkoa wa Singida kupitia *TANROAD* Mkoa?

(c) Kwa kuwa barabara hizi mbili zinahudumia maeneo muhimu ya kiuchumi hasa kilimo cha mazao ya chakula na biashara; je, Serikali itakuwa tayari kuwahakikishia wananchi wa vijiji na Kata kuwa barabara hizo zitaanza kukarabatiwa haraka iwezekanavyo kusudi wananchi wahamasike kujipatia maendeleo kwa kuongeza juhudi za kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Mlumba Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya *Highway Ordinance - Cap.167* ya mwaka 1969, Vifungu namba 6 na 7, moja ya majukumu ya Bodi za Barabara ni kumshauri Waziri wa Ujenzi kuhusu masuala ya barabara ikiwa ni pamoja na kupandisha ama kushusha hadhi baadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi inafanya mapitio ya Sheria ya Barabara *(Highway Ordinance),* ambapo barabara zote nchini zitawekwa kwenye madaraja au makundi yanayostahili kulingana na vigezo vilivyokubalika. Katika zoezi hilo, baadhi ya barabara za Wilaya zinazokidhi vigezo vya kupandishwa daraja zitapandishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya awali, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Mlumba Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Singida ya kutaka barabara za Shelui - Mtoa - Mtekente - Urughu mpaka Kibaya na ile itokayo Kiomboi - Kisiriri - Kidaru - Ibaga mpaka Kidarafa zipandishwe daraja kuwa barabara za Mkoa ili zihudumiwe na Wizara ya Ujenzi, yatajibiwa baada ya zoezi la mapitio ya *Highway Ordinance* kukamilika.

Wakati zoezi hili linaendelea, Halmashauri husika inashauriwa kuendelea kuzihudumia barabara hizo ili wananchi wa vijiji na Kata ambapo barabara hizi zinapita, waendelee na shughuli za uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

**SPIKA:** Hatusikii, sogeza *microphone* karibu.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa barabara hizi zinazounganisha vijiji katika maeneo muhimu ya kiuchumi ni mbovu sana, je, Wizara itaona umuhimu wa kuidhinishwa au kutoa fungu kidogo kwa ajili ya matengenezo ya dharura kwa sababu Halmashauri ya Wilayani haina uwezo wa kuzihudumia barabara hizo?

(b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuja kutembelea kuona ubovu wa barabara hizo ninazozizungumzia na hasa ile inayotoka Kisiriri kupita mlimani kwenda Kidaru ambapo kwa miaka mingi sasa haipitiki kwa magari ya aina yoyote ila tu kwa punda na baiskeli na yeye atakuwa tayari akifika pale apande punda tukakague barabara pamoja? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ombi la Wizara ya Ujenzi itoe fungu maalum ili kutengeneza barabara hizi kwa dharura, lazima niseme ukweli, itashindikana. Lakini naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sasa hivi kwa sababu barabara hizi bado zipo chini ya TAMISEMI, ningeomba Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri yake, waandike barua na taarifa rasmi ya ombi rasmi Ofisi ya TAMISEMI wakiwasilisha ombi lao hilo katika aina ya mradi ili waone jinsi gani TAMISEMI inaweza kuwasaidia.

La pili, aliuliza, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kufika na kuona barabara mbovu na apande punda? Kwanza, mimi nawaonea wivu ndugu zangu hawa kwa sababu wao wana punda, mimi Jimboni kwangu ninatembea kwa miguu. Kwa hiyo, nitakuwa radhi kabisa kuja kupanda punda badala ya kutembea kwa miguu. *(Makofi)*

Na. 58

**Barabara ya Kongwa Hadi Mlali**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kongwa - Sagara - Suguta hadi Mlali Wilayani Kongwa imekuwa ni mbovu sana kwa miaka mingi na kwa kuwa juhudi za Serikali za kukarabati barabara hiyo zimekuwa ni za maeneo korofi tu *(Spot Improvement).* Je, Serikali inaahidi nini kwa nia ya kuitengeneza barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kongwa - Sagara - Suguta hadi Mlali, iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, inajumuisha barabara mbili za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kwa kupita Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Dodoma. Sehemu ya Kongwa - Sagara - Suguta yenye urefu wa kilometa 33.1, iko katika barabara ya Mbande - Kongwa - Suguta yenye urefu wa kilometa 49.7 na sehemu ya Suguta -

Mlali yenye kilometa 6.7, iko katika barabara ya Ng'ambi - Mpwapwa - Suguta - Malali - Pandambili yenye urefu wa kilometa 105.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hizi na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Dodoma, imekuwa ikizihudumia barabara hizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, sehemu ya barabara kati ya Kongwa - Sagara - Suguta ilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi ambapo jumla ya makalvati 18 yalijengwa kwa gharama ya shilingi 44.6m/=.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, sehemu ya barabara kati ya Kongwa na Suguta imefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi katika jumla ya kilometa tatu na pia matengenezo ya kawaida katika jumla ya urefu wa kilometa tano kwa gharama ya jumla ya shilingi 39.9m/=.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matengenezo hayo yaliyofanyika, mafuriko makubwa yaliyotokea Wilayani Kongwa mnamo Januari, 2004, yalisababisha sehemu ya Barabara hii kati ya Mang'weta hadi Chamkoroma na Suguta hadi Mlali kutopitika kabisa. Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* Mkoa wa Dodoma, inafanya matengenezo ya dharura kwa kumtumia Mkandarasi *M/S Madanganya Investment Company Limited* kwa gharama ya shilingi 79.4m/=.

Mheshimiwa Spika, matengenezo hayo ya dharura yanafanyika kati ya Mang'weta na Chamkoroma kwenye urefu wa kilometa mbili na kati ya Suguta na Mlali kwenye urefu wa kilometa 6.7. Matengenezo hayo yatahusisha kuinua tuta la barabara, kujenga makalvati na madaraja ya mfuto.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini baada ya matengenezo hayo barabara hii itaendelea kupitika bila tabu.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza kwa sababu ya muda. Kwa kuwa barabara hii imekuwa ni mbovu kwa miaka thelathini sasa na kwa kuwa kwenye barabara hii ya Kongwa - Mlali si mbali sana kutoka hapa Bungeni. Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kati ya kipindi cha sasa na kipindi cha bajeti tuitembelee barabara hii tuikague na aitengee bajeti wakati wa bajeti? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii kwangu siyo ngeni, nimekwishaitembelea zaidi ya mara mbili, ninaifahamu fika na kama Mheshimiwa Mbunge anaona upo umuhimu twende, niko radhi tutakwenda.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika, sasa ni matangazo. Kwanza, kuna tangazo la kikao cha Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Njelu Kasaka, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 16, Kamati itafanya kikao

majira ya saa tisa alasiri, chumba Na. 231. Tangazo la pili linahusu semina ya kesho kama tulivyokwishakuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba, kesho kuna semina inayodhaminiwa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, inahusu matumizi ya maji ya Mto Nile.

Ratiba ya semina inaonyesha kwamba, itakamilika saa saba na kutakuwa na viburudisho kuanzia saa saba hadi saa nane, viburudisho vilivyoandaliwa na Kamati iliyoandaa semina hiyo.

Tangazo la tatu linahusu burudani kwa Waheshimiwa Wabunge kwa wikiendi hii. Burudani ya kwanza nimeombwa na Mheshimiwa Dr. Aman Kabourou, niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, leo jioni siku ya Ijumaa tarehe 16 Aprili, 2004 mara baada ya Bunge kuahirishwa, Waheshimiwa Wabunge wote wanaombwa kuhudhuria tafrija fupi ya kuwashukuru wao itakayofanyika katika Viwanja vya Ofisi ya Bunge, kuwashukuru kama wapiga kura waliowapigia kura Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Ratiba ya sherehe hiyo inaonyesha kwamba, mara baada ya kuahirisha Bunge tutakwenda kule na Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na tutaendelea kama kawaida hadi muziki utakapofunguliwa saa tatu na dakika ishirini na tano usiku, watakaokuwa na ubavu wa kuendelea wataendelea. *(Kicheko)*

Burudani ya pili ni kesho Jumamosi, *Chief Whip* wa Serikali ameniomba niwatangazie Wabunge wote kwamba, wanaalikwa kwenye sherehe ya kuyapongeza makampuni saba ya Biashara ya Kitanzania, ambayo yalitunukiwa tuzo za juu za ubora huko Geneva hivi karibuni. Sherehe itafanyika *Dodoma Hotel* kuanzia saa moja jioni na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Vile vile ratiba inasema kwamba, wageni wengine wanatakiwa wawe wameshakaa ifikapo saa 12.30, lakini Waheshimiwa Wabunge, tunakaribishwa tufike pale saa moja. Halafu baada ya Hotuba ya Waziri Mkuu, ambaye ni mgeni rasmi mnamo saa mbili hivi utafunguliwa muziki, kwa wale wenye kupenda mambo hayo. *(Kicheko)*

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Bidhaa za Maziwa wa Mwaka 2004
### *(The Dairy Industry Bill, 2004)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, namwomba Mheshimiwa Naibu Spika aje anipokee.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyoko mezani ya Muswada wa Maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii, niipongeze Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kuleta Muswada huu ambao ni msingi mzuri kabisa katika vita yetu ya kupambana na umaskini. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Lowassa na timu yake nzima ya wataalam, kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuleta Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutoa mchango wa Muswada huu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengi wameyaeleza maeneo ambayo yangefaa kuboreshwa na kwa hiyo, mimi nitaangalia katika mtazamo wa eneo moja kubwa. Lakini kwanza ningependa nieleze kwamba, maziwa ni chakula kizuri sana na chakula hiki tumekitumia wote katika kuwalisha watoto wetu na kuwapatia chembechembe nzuri za kujenga miili yao na kuilinda isipatwe na magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maziwa pia ni chakula nyeti na muhimu sana cha kuwapatia watu wazima chembechembe nzuri za kujenga mwili na kuulinda mwili na magonjwa ambayo ni mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zilizoendelea, watu wanakunywa maziwa kila wakati wanapokula chakula na maziwa yanatengenezwa na kupelekwa madukani ili watu waweze kuyanunua na kuyanywa moja kwa moja wanapokula chakula. Sasa mimi nadhani kazi kubwa ya Bodi hii ya Maziwa ambayo inaanzishwa ingekuwa ni kupigia debe au kuhamasisha unywaji wa maziwa hapa nchini. Hiyo ndiyo ingekuwa kazi yake kubwa na ya kwanza. Sasa katika mlolongo wa zile kazi ambazo zipo kwenye sheria hii, naona hili halikuelezwa bayana. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba, liwekwe bayana. Kwanza, siyo tu kwa kuwahimiza wananchi wale chakula bora, lakini pia ingekuwa ni chanzo cha soko kubwa la maziwa

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kabisa kwamba, ili tuweze kupiga hatua ya uzalishaji wa maziwa hapa nchini ni lazima tupanue soko na soko kubwa la maziwa liwe ni wananchi wa Tanzania. Hivi leo tunao wananchi wa Tanzania milioni thelathini na tano. Kama kila mmoja angekunywa nusu lita tu ya maziwa kila siku, basi tayari tungekuwa na soko la lita milioni kumi na saba mpaka ishirini hapa nchini. Soko hilo lingeweza kuwaondoa watu wengi sana kwenye umaskini. Kwa hesabu ambazo unaweza kufanya juu ya bahasha, kama tungekuwa na ng'ombe wa maziwa wa kisasa milioni mbili wanaotoa maziwa kiasi cha lita kumi mpaka ishirini kwa siku, tungeweza kulipatia soko hilo la maziwa lita milioni kumi na saba na kwa bei rahisi kabisa ya shilingi mia mbili kwa lita moja, basi kwa mwaka mmoja tungeweza kuwa na biashara ya maziwa inayozidi shilingi bilioni mia moja na ishirini na mchango huu ungeweza kuwaondolea umaskini Watanzania na familia nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili basi tuweze kufika hapa ni lazima tujiandae, kwa hiyo, Muswada huu uwe ni changamoto ya Wizara yetu ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kutayarisha mpango wa Kitaifa wa kuzalisha mitamba na kuisambaza kwa bei rahisi kwa wakulima Vijijini na hata kwenye maeneo yanayozunguka Miji ili basi tuweze kuzalisha maziwa ya kutosha hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni vizuri tukawafundisha wakulima wetu namna ya kulisha na kutunza ng'ombe wa maziwa maana huwezi kuchunga ng'ombe wa maziwa. Ng'ombe wa maziwa anafugwa. Kwa hiyo, tuwafundishe na kuwaeleza ni chakula gani tuwape, tuwape kiasi gani na mara ngapi kwa siku na tuwape maji kiasi gani, maana maziwa sehemu yake kubwa ni maji. Ili ng'ombe waweze kuzalisha lita kumi mpaka kumi na tano au ishirini za maziwa kwa siku moja, lazima walishwe vizuri na wapewe maji ya kunywa ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vema tukaongea juu ya madawa ya mifugo. Madawa ya mifugo ni ghali sana. Mimi nina ng'ombe wachache sana, lakini bajeti yangu ya madawa ni kubwa sana. Sasa mwaka jana tulianza vizuri tukatoa *subsidy* kwenye mbolea. Basi mwaka huu tufanye bidii iwezekanavyo tuweke kutoa ruzuku kwenye madawa ya mifugo, kwa kweli hapa ndipo matatizo yetu ya mifugo yalipo na tusiwe na kigugumizi juu ya hili. Ng'ombe wetu tunaowaona mbavu zao nje nje huko barabarani siyo kwa sababu tu kuwa hawana chakula cha kutosha ni kwa sababu wanaumwa. Kwa hiyo, tufanye juhudi kubwa tuhakikishe madawa ya mifugo yanapatikana na kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha tatu, moja ya chanzo kikuu cha magonjwa mengi sana ya ng'ombe wetu ni kupe. Kupe anasababisha magonjwa mlolongo mzima na lazima tuchukue hatua ya kupambana na kupe. Sasa hili suala la kuongea mambo kwamba ati kwa sababu ya soko huria kila Kijiji kiendeshe majosho yake, hatujafika hapo. Maana kuna watu ambao wameshaelewa kwamba majosho ni muhimu na yanaondoa kupe lakini bado kuna watu wachache hawajaelewa. Katika Kijiji kama watu wote, acha mtu mmoja wamekubali umuhimu wa josho na huyo mtu mmoja hapeleki ng'ombe wake kwenye majosho na wote wanachunga kwenye pori moja, hakuna faida yoyote ya mwanakijiji yeyote kuosha ng'ombe wake. Hii ni kwa sababu ng'ombe waliooshwa wakienda kule kwenye pori kula majani watapata kupe wa mwanakijiji yule mmoja ambaye hapeleki ng'ombe wake kwenye majosho na watapata magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona Serikali bado ifikirie namna ya kuyaendesha na kuyakarabati majosho ambayo yapo nchini ili nchini kwetu tuondokane na adha kubwa ya magonjwa ya kupe. Magonjwa ya kupe ambayo kwa kweli tunayajua na tunaweza kupambana nayo, ndiyo yanayosababisha hali mbaya ya mifugo hapa nchini. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara iendelee kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, tuyafufue majosho ambayo yapo na tushirikiane na Halmashauri kuendelea kutoa ruzuku katika kuyaendesha majosho haya. Hasa Wizara itenge fedha ya kuyapatia dawa majosho yetu.

Baada ya kuchukua hatua hizi, naamini kabisa kwamba, maziwa mengi yatakuwa yanazalishwa na hivyo ingekuwa vizuri tukaanza kufikiria namna ya kuweka vituo vya

kukusanya maziwa katika maeneo ya Vijijini ambapo maziwa mengi yatazalishwa. Wakulima wengi wanashindwa kabisa kupeleka maziwa yao sokoni kwa sababu wao binafsi hawana uwezo wa kuyapeleka maziwa huko. Kwa hiyo, tungefikiria njia ya kuwahimiza wawekezaji kuweka vituo vya kukusanya maziwa katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuhimiza vikundi vidogo viweze kusindika maziwa na hasa kusindika maziwa ambayo yanaweza kunywewa moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuhakikisha kwamba tunajenga utamaduni wa watu wanaokunywa maziwa hasa wakati huu ambapo ugonjwa wa UKIMWI ni tatizo kubwa, basi ni vizuri tungeanza kama Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mbunge wa Kiteto, alivyopendekeza jana kwamba, watoto wetu wa shule za msingi tuwaanzishie programu ya kuwapa maziwa ya kunywa kila siku. Siyo siku moja moja wabebe kikombe, hapana, kila siku tuwape nusu lita ya maziwa watoto wetu wa shule za msingi. Pia watoto wetu wa shule za sekondari siyo wengi, kwa hiyo na wao kila siku tuwape nusu lita ya maziwa ili kujenga afya zao lakini pia kujenga utamaduni wa watu wanaokunywa maziwa na huko mbele kupanua soko la maziwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili mapendekezo yangu yawe na maana na leo tena nisingependa kupata *Parliamentary gymnastics* hapa maana juzi nilipendekeza mabadiliko hapa nikaambiwa hukuleta barua. Sasa leo pia sikuleta barua, lakini nilikuwa napendekeza, katika kifungu cha 10 cha Muswada huu tuongeze kifungu kidogo cha (g) kinachosema: *"To promote the consumption of milk as a daily dietary supplement among all Tanzanians* au kuhamasisha Watanzania wanywe maziwa au watumie maziwa kama sehemu ya mlo wao wa kila siku". Iwe ni sehemu ya kazi ya Bodi hii maana nadhani hiyo haiko *very clear* katika zile kazi za Bodi ya Maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako nimwombe Mheshimiwa Waziri, akubali mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika ku-*promote processing* na *packaging,* ningeomba sana tuweke kifungu (h), kazi moja ya Bodi hii iwe *to promote milk processing and packaging for direct consumption.* Kuyasindika na kuyapaki maziwa ili yaweze kutumiwa moja kwa moja badala ya kupeleka nyumbani kuchemsha ndiyo unywe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kinyume nyume, sehemu ya tisa, ile ya Wajumbe nilikuwa napendekeza waongezeke Wajumbe wengine wawili. Tuongeze sehemu (l) kama Kamati iliyochambua Muswada huu ilivyosema tuongeze *one member from the Ministry or Cooperative and Marketing* na tuweke sehemu nyingine ya (m) ya *one member from the Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture* ili kuweza kuhimiza Watanzania wote kunywa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nilikuwa napendekeza katika sehemu ya tatu ya Muswada huu ya *definitions* kwamba, pale panaposema *"Minister"* mwisho kuwe na neno *"development",* pale inaposema *"livestock". Definition* ya *Minister* pale mwisho wa sentensi ile liwekwe neno *"development".*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, napenda nikuhakikishie kabisa kwamba, mimi na wananchi wote wa Mwanga, tunaunga mkono Muswada huu mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa wasaa wa kuweza kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge hili, ninaomba nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza sana Marais wetu wawili waliochaguliwa kutokana na Bunge letu katika kutuwakilisha kwenye vyombo mbalimbali vya Kitaifa. Ni heshima kubwa ya Bunge letu lakini ni heshima kubwa sana ya nchi ya Tanzania na pia ni heshima kubwa sana kwa wanawake wa Tanzania, kwa chaguo lililofanywa na Bunge la Afrika kwa kumchagua Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ninaomba pia niipongeze sana Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Lowassa, toka ilipoanza kazi kama Askari wa Mwamvuli, kwa kweli tumeona mabadiliko makubwa sana ya sekta ya maji na mifugo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara. Mfano halisi wa maendeleo ya Wizara hiyo uko katika Mkoa wangu wa Ruvuma, Wizara kwa kiasi kikubwa imeweza kutusaidia kutushirikisha na wafadhili na naomba nimwambie Mheshimiwa Lowassa leo kwamba, zile milioni 48 za mradi wetu wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa sasa zimeshaidhinishwa. Tunakushukuru sana na tunaomba ile ahadi ya Wizara utusaidie sasa kuisukuma ili ule mradi wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa kwa wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, uanze kufanya kazi na moja kwa moja wajiunge katika mpango huu wa Bodi mpya inayoanzishwa ili wanawake wa Mkoa wa Ruvuma waweze kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyejua kwamba, maziwa ni ng'ombe na ng'ombe ni maziwa, lakini ng'ombe na maziwa ni afya lakini pia ng'ombe na maziwa ni uboreshaji wa mazingira kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ng'ombe ni utajiri ambao kwa kipindi kirefu na kwa utamaduni wa wananchi wengi wa Tanzania, ulikuwa ni utajiri ambao hauonekani wazi na haujidhihirishi. Lakini ninafikiri sasa kwa kengele hii inayopigwa ya uanzishwaji wa chombo maalum kitakachosimamia suala zima la maziwa ambayo yanatokana na ng'ombe na hasa kwa wafugaji wadogo wadogo, basi nadhani utajiri huu utajidhihirisha wazi na sasa utaweza kuwa ni changio lingine kubwa sana katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa ng'ombe na maziwa ni utajiri lakini pia ng'ombe ni kitu ambatanisho cha msingi kabisa katika Idara nyeti ya Sekta ya Kilimo kama Sekta Kiongozi ya Taifa letu la Watanzania.Tunapozungumzia maziwa, kama nilivyosema mwanzo, tunamzungumzia ng'ombe. Licha ya maziwa kuwa ni chombo kingine ama kitega uchumi kikubwa kinachopatikana kutokana na ng'ombe, lakini kwa ongezeko la ng'ombe hao watakaotoa maziwa kwa ajili ya afya, kwa ajili ya haya mambo yote ambayo nimeyasema hapo mwanzo, lakini ng'ombe wanaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa sana kuboresha Sekta ya Kilimo na kuwaondoa wananchi kutoka katika kutumia jembe la mkono angalau kuingia katika jembe la kukokotwa na ng'ombe hawa ambao watakuwa pia wanatoa maziwa na hivyo kuona kwamba wanaweza kubadilisha sekta ya mapato katika nchi yetu na kuiboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Wizara kwa kuzingatia maombi ya wadau wa Sekta ya Mifugo na hasa wazalishaji wa maziwa na uanzishwaji wa Bodi hiyo ambayo itasimamia maendeleo ya uzalishaji wa maziwa, lakini maendeleo pia ya soko la maziwa ndani na nje ya nchi ya Tanzania. Kwa ujumla Muswada wenyewe umejikamilisha. Labda yapo maeneo machache sana ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge, tunafikiri tunapoishauri Serikali kupitia Muswada huu, basi utekelezaji wake utaweza kuwa yakinifu na hivyo utaleta maendeleo endelevu ambayo yanaweza kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Bodi nyingi zinapoundwa zimekuwa zikiweka Makao Makuu katika maeneo ya Miji na hivyo imekuwa ni vigumu sana habari za utendaji wa Bodi hizo kuwafikia walengwa katika maeneo ya vijijini na hasa vijiji vya mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya pekee, kwa kuwa Bodi hii imeombwa kutokana na matakwa wadau, ni wakati muafaka wa kufanya mabadiliko ya utendaji wa kazi wa Bodi zetu ambazo tumezizoea katika nchi yetu ya Tanzania. Ninaomba Bodi hii kwa kweli iwashirikishe sana wafugaji wadogo wadogo ambao wako katika maeneo ya mbali huko vijijini ili kweli waweze kufaidika na hiki chombo ambacho kinaonyesha kwamba ni ukombozi wao mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati napitia kifungu cha 9 cha Muswada ambapo *composition* ya *Members* wa Bodi, sina tatizo na hiyo *composition.* Lakini nilikuwa nafikiri kwamba, utamkaji wa uwiano wa kijinsia katika uundaji wa vyombo vya namna hii ni jambo la msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaogopa Mheshimiwa Waziri anaweza akateua hawa watu kadri ya utaratibu, lakini akasahau kuwaingiza wanawake ili wawakilishe wanawake wafugaji kwenye maeneo wanayotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni kweli kabisa kanuni yako inatukataza kufanya mabadiliko. Lakini mimi nafikiri kwamba, Mheshimiwa Waziri ananisikia, atakapokuwa anafanya uteuzi kwa sababu kanuni inanikataza kufanya mabadiliko, basi

utekelezaji uwe katika maombi hayo ninayoyaleta kwake kupitia katika mchango wangu hapa. *(Makofi)*

Tumeshuhudia kabisa wanawake ambao ni wafugaji ni kweli kabisa wameweza kuwa watekelezaji wazuri wa mabadiliko ya maisha katika familia na hivyo basi wakitiwa moyo na wakiona kabisa kwamba chombo hiki kinawafikia moja kwa moja inaweza ikasaidia kurahisisha masuala yote ambayo yanaonyesha kwamba yatakuwa yakifanyiwa utekelezaji katika Bodi na Msajili wa Bodi hiyo kama alivyoonyeshwa katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa pia nataka kuendelea kusisitiza utekelezaji wa Bodi ni jambo la msingi, lakini yapo mazoea mengine ambayo tumeyazoea. Bodi itakuwa inafanya kazi na ninaamini kabisa kwamba, itaamua hata kufanya maonyesho ya unywaji wa maziwa kwenye shule za msingi na maeneo mengine tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mazoea yaliyojijenga katika nchi yetu ya Tanzania, maonyesho haya yote yamekuwa yakifanywa katika Makao Makuu ya Miji ya Wilaya na Mikoa. Lakini katika maeneo ya vijijini ambako *population* pia ni kubwa na wazalishaji wapo kule, vitu kama hivi havipelekwi. Sasa nilikuwa nashauri sana katika utekelezaji wa majukumu yake hii Bodi hebu iangalie namna gani inaweza kufanya maonyesho maalum katika maeneo ya vijiji. Aidha, ku-*promote* soko lenyewe la maziwa ama tabia ya kufuga ng'ombe ili kutoa maziwa na hivyo basi tunaweza pia kutumia nafasi hiyo hiyo kuwaonyesha wafugaji kwamba, ng'ombe huyo anaweza kutoa maziwa kama biashara, lakini akatumika katika shughuli za kilimo na kuwakomboa wanawake wengi wanaotumia jembe la mkono wakajifunza kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatutafanya hayo hata mpango wa kuhamasisha watoto wetu wanywe maziwa, hayo maziwa tutayatoa wapi wakati wafugaji bado ni wachache sana katika maeneo mengine ya Tanzania. Tukipitisha huu Mpango kwamba ni lazima watoto wanywe maziwa kule Kusini, sijui kama tutawapa hayo maziwa tutayatoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, aone umuhimu wa kufika katika maeneo ya vijijini ambako kuna wafugaji wadogo wadogo wakahamasishwa vizuri zaidi wakaongeza uzalishaji na hivyo kukawa na uwiano mzuri wa suala zima la ku-*promote* matumizi ya maziwa na ufugaji wa ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba tena niendelee kusisitiza kwamba, upo umuhimu mkubwa wa Bodi hiyo kushirikiana na Asasi nyingine ambazo tayari ziko katika nchi yetu ya Tanzania. Tunasema tunataka kuboresha maziwa, lakini tunasema tunataka kuboresha soko, lakini hatuwezi kuyaboresha maziwa na soko bila kuwa na teknolojia nyepesi zinazoweza kumudu kutumika katika maeneo ya vijijini. Sasa kama Bodi hiyo itajishirikisha na Asasi kama *SIDO* na vyombo vingine, nafikiri tunaweza tukawa na Programu Maalum kabisa ya kutengeneza hizo mashine ndogo ndogo za

kuwasaidia wafugaji kukamua maziwa na kuyasindika na hivyo basi yakaweza kuingia katika soko kulingana na viwango na ubora ambao utakuwa umetengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Wizara ione umuhimu wa kujihusisha na Asasi nyingine ambazo zinaweza kusaidia sana ku-*promote* suala zima hili la maziwa na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado ninaendelea kutatanishwa na ubora wa maziwa kulingana na asili ya ng'ombe ambao wapo. Mimi bibi yangu alikuwa hataki kabisa kunywa maziwa ya ng'ombe wa kisasa, akisema kabisa kwamba yale maziwa utamu wake ni tofauti na maziwa ya ng'ombe wa kienyeji.

Sasa, Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani liko suala lingine la kimsingi la kuangalia kwa kina ni ubora upi ambao ni muhimu katika kuboresha afya, lakini kuingia katika soko la ndani na la nje la maziwa. Uki-*compare* ng'ombe huyo wa kienyeji na ng'ombe wa kisasa nini kifanyike? Mimi nafikiri Wizara inatakiwa pia iwe makini sana katika kuliangalia suala hilo na hivyo basi itasaidia maziwa yatakayokuwa yakitumika katika nchi yetu ya Tanzania kwa Sheria ambayo tunataka kuipitisha leo, basi yatakuwa ni maziwa yenye viwango vya virutubisho vinavyotakiwa Kimataifa na hata katika nchi yetu ya Tanzania ili kweli kuwa na mifugo ambayo inaweza kuleta kitu halisi na kinachotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeelezwa kwamba kutakuwa na Msajili ambaye yeye ndiyo atashughulikia kabisa kusajili vikundi mbalimbali vya wafugaji. Mimi tu nilikuwa naomba sana suala la usajili lisiwe na urasimu, wafugaji hao wadogo wadogo wanapopata hizo taarifa basi mara wanapotaka, wasajiliwe ili kutambulika na kuwasaidiwa na Mfuko huo Maalum wa kuwasaidia kukuza uzalishaji wa maziwa iwe ni rahisi kwao kufikia na yeye awe ni rahisi kuwafikia. Sasa hilo liendane sambamba na suala zima la umuhimu wa kuongeza watumishi wa ugani ambao ni Bwana Mifugo watakaoweza kuwasaidia sana hawa wakulima wetu katika shughuli zao za uzalishaji za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli bado tunapata shida kubwa sana ya watumishi hao wa ugani, siyo katika Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo hata Wizara ya Kilimo na Chakula unaona ni jinsi gani Serikali inavyokuwa na mipango mizuri lakini haitekelezeki kwa kukosa wasimamizi makini ambao wanaweza kufanya kazi na wakulima wetu siku kwa siku na kuwasaidia kuelewa kila linalotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri hataliangalia hili la kiutekelezaji, basi mimi ninaamini kabisa kwa kweli tutakuwa na matatizo makubwa ambayo hayataweza kusaidia kukuza soko hili la maziwa wala kukuza suala zima la ufugaji wa ng'ombe katika nchi yetu ya Tanzania. Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, jana alilia sana na Mikoa ya Kusini, bado Mheshimiwa Waziri tunahitaji kuongezewa mifugo kwa kiasi kikubwa Mikoa ya Kusini. Yeye alizungumzia Lindi na Mtwara lakini mimi Mheshimiwa Waziri ninasema kwamba, Ruvuma bado tunahitaji mifugo, tunahitaji ng'ombe na mbuzi wa maziwa, bado tunahitaji kuongezewa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka na sisi kuondokana na ile historia kwamba sisi siyo wanywaji wa maziwa. Mheshimiwa Waziri siku hizi watoto wetu wanapenda sana maziwa na ukishawazoesha watoto, sisi wazazi tunajua ukishamzoesha mtoto kunywa uji wa maziwa, ukimpa uji usiokuwa na maziwa hawezi kunywa tena. Sasa Mheshimiwa Waziri tunataka na sisi katika Mkoa wetu wa Ruvuma na Mikoa mengine ya Kusini, tujenge hiyo tabia ya kunywa maziwa na watoto wetu wapate hiyo lishe bora katika maeneo tunayotoka. Lakini msaada mkubwa utakuwa ni katika mpango huo maalum labda ule wa kukopa ng'ombe lipa ng'ombe, kopa mbuzi wa maziwa, lipa mbuzi ama utaratibu mwingine wowote ambao utaonekana kwamba ni utaratibu muafaka wa kuweza kuongeza mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanapoendelea kutekelezwa, mimi nilikuwa nashauri Bodi ichukue tahadhari ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Nina uhakika utekelezaji wa majukumu ya Bodi utafanya ongezeko kubwa sana la ufugaji katika maeneo mbalimbali na hatari inayoweza kuja kujitokeza ni ugomvi wa wakulima na wafugaji. Kwa hiyo ni muhimu utekelezaji huu unapoanza pia suala la kuchukua tahadhari ya migogoro hiyo ya wafugaji na wakulima, lipewe kipaumbele kusudi lisiwe tena ni kikwazo kingine kikubwa huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ambao umeletwa na Mheshimiwa Edward Lowassa. Ninaomba na mimi niungane na wenzangu, kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella pamoja na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa nafasi ambazo wamezipata katika Afrika na katika Dunia kwa ujumla. Mimi naamini kabisa kwamba, hii ni sifa kubwa kwa nchi yetu na kwa kweli tunawatakia kila la kheri na fanaka katika majukumu hayo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na Wizara kwa ujumla. Kwa kweli toka Wizara hii ianzishwe mimi ninataka niseme kwamba, kumekuwa na *a lot of seriousness* katika kuona kwamba tunafikia hatua hii ambayo tumeifikia. Kumekuwa na Warsha nyingi na wadau mbalimbali wamekuwa wanakutanishwa kuzungumzia na kuonyesha umuhimu wa maziwa. Kwa kweli *Industry* yote kuna mabadiliko makubwa ambayo yanafanyika na kwa hiyo napenda kuchukua nafasi hii kupongeza sana jitihada ambazo zimeletwa na Wizara. Moja kwa moja kabla sijaingia kwenye *speed,* ninataka nitamke hapa waziwazi kwamba, Muswada huu ninauunga mkono na ninamtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri na fanaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliyesimama hapa ni Kiongozi wa Wamasai na Mheshimiwa Edward Lowassa anafahamu, *fifty percent* ya *voters* wangu ni Wamasai. Kwa hiyo, nikikaa kimya hapa nisizungumze hapa, nitapata mgogoro kule nyumbani na

wale wengine waliobaki wote wale Mheshimiwa Edward Lowassa anafahamu wanafanya *zero grazing*. Wakati wanapozungumza habari hii, tatizo moja linalonipata kubwa na ambalo leo linakuwa *resolved* hapa ni kwamba, nikihimiza wananchi wangu katika Jimbo langu la Siha nikienda pale Karansi, nikienda Lekrimuni, nikienda Ndinyika, nikienda Kandashi pale, nikienda Mae, nikienda Wandri, nikienda Kengia, nikaenda Samakimaini, nikienda Nsherehehe, nikapiga kelele wasiwasi wangu mkubwa ninaoupata mara kwa mara ni kwamba hawa wakitoa maziwa haya, tutayapeleka wapi? Ndiyo tatizo kubwa, kwa hiyo, nanyamaza, nakuwa mwangalifu sana, sipigi kelele sana kwa sababu baadaye wataniambia kwamba haya Mheshimiwa Mbunge, maziwa haya hapa, tuyapeleke wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika na *especially* wakati wa mvua, zikinyesha hivi kidogo, sana sana tunayapeleka pale Arusha kwa akina Ngassa na akina *Northern Creameries,* wakati mwingine wanafunga hauna mahali pa kupeleka maziwa. Kwa hiyo, leo tunauona mkakati wa Wizara ambao unaonyesha namna ambavyo tuta-*process* maziwa na namna ya kufanya *marketing*. *Contradiction* ambayo iko *in silent* katika Wizara kwa maana ya maziwa ni kati ya uzalishaji na soko. Wajapan wale baada ya *Moiji Restoration* walikuwa wanazungumza habari ya *Marketing in strategies* hawakwambii *how much profit have you captured, no* hawazungumzii hiyo. Wanazungumzia *how much market have you captured* hata kama akipeleka kwenye *balance sheet* anaonekana anapata hasara, *it is not an issue.* Ukiwa unafanya *business,* ukipoteza soko ndiyo umepata hasara, kama *profit* hupati kubwa sana unapata kidogo *is not a problem.* Inakuwa ni *problem* kama ulikuwa na soko, kuna watu wanakunywa maziwa hapa wamepotea huna, hapo ndiyo ume-*loose* mzee wangu.

Kinachozungumzwa hapa ni suala la *marketing* ya maziwa. Maziwa ni kitu *delicate* sana, yakishakamuliwa yanakamuliwa karibu mara tatu asubuhi, saa sita na jioni, sisi hapa kwetu Tanzania mara nyingi ni asubuhi na jioni, unazalisha maziwa, unakamua asubuhi na jioni maziwa. Kama huna mfumo mzuri wa kutunza maziwa ukiamka kesho asubuhi yameganda, huwezi kuyatumia tena na utakuwa na maziwa ya mgando mengi hapa, utapeleka watakunywa baada ya hapo utamwaga tu. Unahimiza watu wazalishe maziwa kwa wingi, unajua kabisa hii iki-*take off, problem* utakayokuja kuipata hapa ni kiasi cha maziwa kinachopatikana kitakuwa ni kidogo, kwa hiyo, utakuwa na *process* na vitu vingine, sasa unafanyaje?

Sasa hapa kwetu imezungumzwa na Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up,* nitamwomba atueleze, tulielezwa vizuri hapa, Warsha zikafanyika na hapa ndani, tukaambiwa tuweke utaratibu hapa ikiwezekana, nadhani hata Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wakaanza kupata maelekezo tuhakikishe kwamba, watoto wanapata maziwa pale shuleni, hivi nchi nzuri namna hii! Tanzania hii imefika mahali inaleta mpango kama ule wa MMEM unashindwa nini kutamka pale ndani, unasema hivi mimi nikitaka niondokane na utoro wa watoto shuleni, nataka niweke maziwa pale shuleni, kila siku wapate kikombe kimoja cha maziwa. Kuna mtoto atakwenda shule tu kwa sababu anajua nikienda shule nitapata maziwa inazungumzwa na Mheshimiwa Waziri, uliizungumza vizuri wakati ulipokuja kwenye Jimbo langu la Siha, nakumbuka ulitoa maelekezo na tukai-*take up* sisi tukaanza kuzungumza hii habari kidogo kidogo tunasikia

imefifia. Hivi kweli kwa Tanzania sisi tutafika mahali Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaambiwa unajidai nini? Unasema ninajidai kwa sababu watoto wangu wote shuleni wanapata kikombe kimoja cha maziwa. Unasema ninajidai na hiyo. Imekwenda wapi?

Wachina wanajidai pale tunawaona wanawatishia Marekani wale, moja ya mambo ambayo wanafanya Wachina wanaonekana kwamba wale ni kiboko, ni *internal market*, hapa kwetu tumei-*create* hiyo watu hapa wanakunywa suturungi. Kwa hiyo, mimi nafikiri kuna haja ya kujua vizuri hivi tumefikia wapi kwenye ule mpango? Mpango ule ulioko pale shuleni ni mpango mzuri, huwezi benki nenda kwa Norway, nenda Canada, ukiwaambia hizi fedha naomba kwa ajili ya kuwapa watoto maziwa wataitikia, watatoa watakwambia chukua. Kwa hiyo, ukienda pale ukapiga kelele, ukasema mimi bwana katika huu mpango wa elimu ambao mnanisaidia ndani yake mimi nataka kuwasaidia watoto wapate maziwa pale shuleni. Kwa sababu ndiyo mahali pekee, umuhimu wa maziwa Mungu aliuona yeye mwenyewe na ndiyo maana hata binadamu alimwekea maziwa. Mungu kwa uwezo wake angeweza akaweka soda kwenye matiti ya mama, watoto wakanyonya soda. Lakini hakuweka soda akaweka maziwa, *importance* yake ameiona, Mungu aliuona umuhimu wa maziwa. Akaona hawa walivyokaa kaa namna hii nikiwaacha hivi hata haya ya ng'ombe hawatakunywa, basi ngoja nimwekee mama ili mtoto akizaliwa anywe maziwa. Leo tunataka kukaa hapa tunaumiza vichwa kuhusu habari ya umuhimu wa maziwa.

Mpango huu Mheshimiwa Edward Lowassa, ninaunga mkono. Ni mpango mzuri, lakini ukitaka ku-*resolve* hii *contradiction you go back to history,* hapa siyo kwamba hatukuwa na *dairies,* hapa siyo kwamba hatukuwa na mipango mizuri kama hii inayozungumzwa hapa, ilikuwepo. Kwangu Siha Sanya Juu tulikuwa tuna-*collect* maziwa, ukienda Kibong'oto pale madukani tulikuwa tuna-*collect* maziwa, ukienda Samakimaini pale Sango, Siha Sekondari pale, tulikuwa tuna-*collect* maziwa. Tulikuwa na *Collecting Center* ya maziwa. Sasa turudi pale Sanya Juu, kuna kituo kimekaa pale, Longai walikuwa wanatoa maziwa, Molomo walikuwa wanatoa maziwa, Galalakua walikuwa wanatoa maziwa, mashamba yote Lelongo walikuwa wanatoa maziwa, akina John, waliitwa Bwana John wakati ule, walikuwa wananywesha maziwa Kibong'oto Hospitali. *Industry* hiyo ikaenda ikafa, ikaisha. Sasa tunataka kuirudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamezungumza hapa habari ya *subsidy. Europe* wanampa ng'ombe *dollar* 3 kama *subsidy.* Hapa kwetu Tanzania mtu kima cha chini, ni chini ya *dollar* 1, binadamu. Wao wanaweka *subsidy* wanampa na tukizungumza habari ya *subsidy* hapa najua inaudhi na nini, ina matatizo yake na nini, lakini *it is an objective reality.* Hiki kitu ukikiacha hivi hivi, ukasema tumwachie Mheshimiwa Edward Lowassa pale anafanye hivi, usi-*introduce Government subsidy* kwenye hii *Industry,* hatutafika.

Naipongeza Serikali kwamba, mmeleta hapa mnazungumzia habari ya Mfuko kwamba kutakuwepo na Mfuko. Mfuko utaangalia habari hii na sisi tunaunga mkono jambo hili. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Botswana ile tunavyoiona inajidai pale, *South Africa,* hizi nchi za *Scandinavian,* jeuri yake yote unayoiona pale ni maziwa tu,

kwetu hapa tulikuwa tunazalisha *Tanbond* imekwenda wapi? Wenzetu hapo Kenya nenda kaangalie wanavyofanya pale, wanafanya vizuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuweke msisitizo mkubwa kwenye kutoa *subsidy*. *Extension Services* zetu nazo zitiliwe mkazo, mpaka tunavyozungumza sasa hivi, mimi naandikwa kwenye magazeti, moja linalopigiwa kelele hakuna Afisa Kilimo, hakuna Afisa Mifugo anayetusaidia pale, napiga kelele kila wakati wananiandika Mbunge wetu njoo utusaidie hatuna mtu. Ng'ombe anakufa pale, wanakwenda pale wafanya *vaccine* pale anababuka unakuta hapa shingo yote imeondoka nyama, Mmasai ukimwambia nenda kamuweke tena *vaccine* pale anakwambia *no way,* acha wafe tu. Inabidi niende nikawaelimishe, nikaeleze kwamba hii imefanyika ndiyo na athari zake ni hizo hawaelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majosho, hili la majosho nataka ni-*pre-empt* majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu najua atakavyoniambia, ataniambia wewe na Halmashauri yako mwende mkakae mfanye juu chini mhakikishie kwamba, mnatengeneza majosho. Sasa nataka nitoe haya majibu ili nione atajibu vipi tena huko mbele. Hilo mzee wangu kule Monduli halikuwezekana, halikuwezekana Hai, tumepiga kelele pale, tulikwenda kukodi *Private Sector* tukawaambia hebu saidieni katika Mpango huu wa kuanzisha majosho katika Wilaya ya Hai, halafu ninyi mchukue ile fedha haiwezekani. Mheshimiwa Waziri akisimama anasema Halmashauri ya Wilaya ya Hai ndiyo inayotakiwa yenyewe na Mbunge wao wakae wafikirie namna ya kuweza ku-*revival* yale majosho pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzee wangu Edward Lowassa, nisaidie majosho pale katika Wilaya ya Hai, katika Jimbo langu la Siha, hutaki nirudi tena humu ndani? Unajua majosho yakijengwa yakiwekwa pale Lakelemuni, Ndinyika, Makiwalu, Dunyomoroko na Ngumbaru, wale jamaa wataniambia wewe utakuwa Mbunge milele. Unisaidie mzee wangu, ukisema hapa Halmashauri ipi ya Hai itakayofanya kazi ya kujenga majosho. Ipi inasuasua pale, akinamama pale wameambiwa wapewe mikopo ndiyo hivyo iko hoi. Nisaidieni kidogo. Mtusaidie yapo majosho ambayo yamekufa pale hayafanyi kazi, tuyakarabati halafu tuweze kuanzisha yale mengine ambayo yatatusaidia. Tunazungumza habari ya maziwa hapa, huna majosho, ng'ombe wanatafunwa na kupe, *how?* Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hilo. *(Kicheko)*

Mwisho, mashamba ya *NARCO,* nilikuwa nimeandika kuchangia kwa maandishi, nilifikiri sitapata nafasi ya kuzungumza humu ndani. Habari hii najua inazungumzwa hapa mashamba yale yako katika Jimbo la Siha ni ekari 78,000 ya *ranch*. Mpango umewekwa vizuri na Rais alikuja hapa akaeleza katika hotuba yake, nakumbuka na Mheshimiwa Waziri, *on several occasions* ameeleza utaratibu utakaotumika. Ekari 20,000, ekari 2,000, 2,000 zitagawanywa, zitapatikana *ranch* kama 100 pale. Swali langu tunawasaidiaje wafugaji wadogo wadogo ambao uwezo wao ni mdogo, hawawezi kwenda kununua mashamba yale ya ng'ombe, unawasaidiaje ili na wao waweze kushiriki katika kumiliki yale mashamba? Hili swali mara kwa mara naliuliza hapa ndani.

*(Hapa umeme ulikatika na kuwaka tena baada ya dakika moja)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Kuna haja ya kuwasaidia hawa ukisema kwamba waende pale watakwenda, ekari 78,0000 zote zitaondoka na watu kutoka nje. Wananchi wa kwetu sisi tunataka kuwaondolea umaskini, tunasema tutawapeleka pale, tutawaambia wajaze fomu pale wapeleke na wao waonyeshe kwamba ni kiasi gani wanaweza wakatoa, watashindwa tu mzee wangu wale.

Mimi kazi yangu hapa ni kupiga kelele kwa ajili ya wanyonge, sasa kule kwangu ukiniambia kwamba kule yatauzwa yale mashamba pale yatachukuliwa yote, naangalia tu hivi. Hivi hatuwezi kufika mahali tu-*devise a formular* tuseme je, hawawezi kujiunga katika vikundi vya ushirika wakakaa kwa pamoja tukaangalia kwa namna kama wamejiunga hao, tukasema hao tuwasaidie kwa sababu wanaonekana mtaji wao ni mdogo. Tukawakuza, tukawalealea hivyo, tukawafikisha mahali na wao wakaweza ku-*own* zile *ranch* ndogo ndogo ambazo tunazizungumza pale. Mpango unaokuja wowote hapa kama hauleti manufaa kwa Watanzania hawa wa kawaida hauna maana. Unakuwa na maana tu kama utakwenda chini ukafuata mfugaji mdogo mdogo pale ukamsaidia. Hii ndiyo *concern* yangu, nimeiandika katika karatasi kwa sababu *I was not sure* kama nitapata nafasi. Nitamwomba Waziri anaposimama kuhitimisha hoja yake, naelewa imewekwa vizuri na imeelezwa, lakini atuambie Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inawasaidiaje wafugaji wadogo wadogo katika ku-*own* hizi *ranch* ndogo ndogo ambazo zipo katika nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, napenda kurudia tena kusema mimi naunga mkono jambo hili na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nawaomba hii ni roho yetu, tupitishe haraka haraka wala msiumize vichwa. Hii hapa ni kwa manufaa yetu na maslahi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Kwanza zaidi ya maelezo ya awali ni jambo la masikitiko sana kwamba kilichokuwa Kiwanda cha Maziwa cha Tanga, kimebinafsishwa kwa mwekezaji ambaye ametelekeza kabisa, usindikaji wa maziwa na utengenezaji wa bidhaa za maziwa, badala yake wawekezaji hao wanajishughulisha na biashara ya matrekta ambayo haina uhusiano wa moja kwa moja na uzalishaji na biashara ya bidhaa za maziwa.

Pili, hali hii imerudisha nyuma biashara ya bidhaa za maziwa Mkoani Tanga kinyume cha matarajio ya Muswada tunaoujadili. Napendekeza kwamba, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na wadau wengine, wawashauri wawekezaji hao ama watumie majengo, mitambo na vifaa vingine vilivyopo katika kiwanda cha kutengeneza bidhaa za maziwa kama ilivyokuwa

awali au upya kwa wawekezaji wenye mipango thabiti ya kutengeneza na kuendeleza biashara ya maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni kwa vile Chama Kikuu cha Ushirika wa Maziwa Mkoani Tanga *(TDCU),* wanakosa mtaji, lakini ushirika huo una dhamira kuu na mipango ya kuendeleza utengenezaji na masoko ya bidhaa ya maziwa. Nashauri kwamba, *TDCU* wafikiriwe miongoni mwa wawekezaji wengine wenye nia ya kuendeleza mazao ya maziwa. Ikibidi nashauri Serikali iwawezeshe katika kufanikisha dhamira yao hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, pia napendekeza kwamba, Serikali ifikirie kuwawezesha *Tanga Fresh* kupata mitambo ya ziada na ya kisasa zaidi ili waweze kumudu vema zaidi, kukidhi mahitaji ya bidhaa zao za maziwa ambayo yanakuwa kwa kasi kubwa kuliko uwezo wao halisi walionao sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ningependa kwa mara nyingine, kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pia niwapongeze Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo na Watalaam wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mazingira Duniani.

Kwa kuwa Serikali imeamua kuinua uchumi wa mfugaji wa Kitanzania kwa kufufua soko la maziwa la nje na ndani kwa kuwa viwanda vingi vimefirisika muda mrefu, ni vema vikafanyiwa utafiti wa kina. Mkoa wa Tabora ulikuwa na Kiwanda cha Kusindika Maziwa, Samli na Siagi ambacho mpaka sasa kipo lakini hakifanyi kazi. Mkoa unao wafugaji wengi ambao ni wahamiaji kutoka, Usukumani, Utusi, Wanyamwezi wenyewe kwa mtazamo huo maziwa wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kuwa kwanza, Bodi ifanye utafiti wa kina kwenye maeneo yenye wafugaji wengi ili waweze kushauri wawekezaji. Pili, Bodi ipitie upya kwenye viwanda vilivyo kuwepo awali, iangalie uwezekano wa kuanzisha viwanda vya maziwa kikanda, vikundi vikopeshwe ng'ombe wa maziwa na mbuzi wa maziwa, elimu itumike kwa kutumia vipeperushi, wananchi wajue umuhimu wa viwanda hivyo, Bodi hiyo ipewe vyenzo za kufanyia kazi kwa kujitegemea kama ilivyokuwa upande wa maji taka na maji safi, kwani utaratibu huo ni mzuri.

Nimpongeze kwa kina, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa utaratibu wa suala zima la upatikanaji wa maji mijini, hususan Mkoa wa Tabora, pia nichukue nafasi hii kwa kupitia kwake, nimpongeze Meneja wa Maji Tabora, Ndugu Kalingonji, kwa usimamizi wake mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa maendeleo ya Watanzania kichumi na kiafya.

Kwanza, kufanikisha mradi huu, watakaochaguliwa kwenye Bodi wawe na mwelekeo wa kusaidia wananchi katika mifugo.

Pili, himiza *Councils* zijenge mabwawa, yatasaidia maendeleo ya mifugo na watu. Maziwa yatapatikana na watu watakunywa kuanzia kwenye familia. Tatu, bei ya dawa ni kubwa, punguza kwa njia ya kutoa bei nafuu kwa wananchi wadogo wadogo walioungana, wafundishwe kuzalisha mazao yatokanayo na maziwa kama siagi, jibini, samli na kadhalika. Usindikaji maziwa katika vikundi vidogo ni msaada mkubwa wa wakulima wadogo wadogo.

Nne, Waholanzi walisaidia sana Mkoa wa Kagera kuendeleza mifugo na kutafuta masoko. Baada ya kuondoka ushirika unasuasua, mtaji ni mdogo, naomba uwasaidie wana ushirika wa vikundi vya maziwa Kagera.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja na naipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu, ambao ninaamini utaboresha sana shughuli za maziwa, chakula bora kwa Watanzania wote.

Hii itapunguza umaskini kwa wafugaji wetu. Katika Mkoa wa Shinyanga wakati wa masika kuna maziwa mengi sana na wakati mwingine maziwa haya huharibika. Mkoa wa Shinyanga, ulikuwa umekubaliwa kuwa na Kiwanda cha Maziwa na *UNDP* lakini mikopo ilipositishwa miaka ya 1990, mradi huu haukufanyika na ilifanywa *study* yake na *TANK DAIRY* ya Denmark. Naomba nitafute taarifa hizo halafu nitaziwasilisha Wizarani ili mradi huu uweze kutekelezwa kwa kuwasaidia wakulima wa Mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba suala la majosho liwekewe maanani ili kuboresha afya za mifugo yetu hasa tatizo la kupe. Kwa sasa hivi majosho mengi hayafanyi kazi. Mifugo ni mali Shinyanga, inafanana na nchi ya Botswana. Nchi ya Botswana inao uchumi safi sana na wanayo mifugo na almasi ambazo zimeboresha sana mapato ya nchi hiyo. Shinyanga tunayo almasi pamoja na mifugo. Wafugaji wakisaidiwa viwanda vya maziwa ya ng'ombe maisha yao yatabadilika.

Hapo nyuma nimewahi kuulizia kuhusu suala la Serikali kujiunga tena na *International Office for Animal Health,* Paris Ufaransa, kutoa taarifa za magonjwa ya mifugo yaliyopo Tanzania na jinsi yanavyoshughulikiwa, hii itawezesha mazao ya mifugo yetu kukubalika Kimataifa (Masoko ya Kimataifa na kadhalika). Nitashukuru kupata taarifa jinsi Wizara ilivyoshughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naendelea kuwapongeza kuhusu jinsi Wizara hii inavyoshughulikia utatuzi wa kero za wananchi. Nawatakia utekelezaji mwema wa

majukumu mliyojiwekea katika Muswada huu katika kuboresha maisha ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DANIEL N. YONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la maziwa ni dogo ijapokuwa Watanzania ni wengi. Lazima tujenge soko la walaji maziwa. Njia mojawapo ya kupanua soko ni kutoa ruzuku ya pesa kwa kila mtoto wa shule ya msingi anywe maziwa kila siku. Kila mtoto apate nusu lita kila siku na alipiwe na Serikali. Tukifanya hivyo, tutawapa watoto wetu afya na tutawawezesha wafugaji wazalishe maziwa kwa wingi.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sana kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, pamoja na Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri na Wataalam, kwa kuleta Muswada huu muhimu ambao kwa hakika umechelewa hasa baada ya *DAFCO* kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo hasa sekta ndogo ya maziwa, ina nafasi kubwa ya kuchangia katika vita yetu ya kupambana na umaskini ili mradi hatua thabiti za kudhibiti na kuendeleza sekta ndogo ya maziwa zilizopendekezwa zinaelekezwa kwa dhati na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mkinga ninaloliwakilisha, limepiga hatua nzuri katika jitihada za kupanua na kuendeleza sekta ya mifugo hasa ya ng'ombe wa maziwa. Ushirika wa Wafugaji wa Mkoa wa Tanga *(TDCU)* na pia *TADAT,* wamefanya jitihada kubwa ya kuendeleza ufugaji wa ng'ombe bora na utaratibu mzuri wa kukusanya maziwa na kuyasambaza katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TDCU* na *TADAT* vile vile zimefanya kazi kubwa sana kuwahamasisha wananchi kujiunga katika Vyama vya Ushirika na vikundi vya uzalishaji. Wananchi wengi sana wamehamasika na wanaendelea kuhamasika. Mahitaji ya ufugaji wa uzalishaji maziwa yamekuwa makubwa sana kuliko upatikanaji wa mahitaji. *Tanga Fresh* wameweka msingi mzuri sana wa kusambaza maziwa, kusindika mazao ya maziwa na kuyasambaza nchini, bado kuna nafasi kubwa sana ya kuendeleza usindikaji na usambazaji wa mazao hayo kama si kwa matatizo yanayowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo mengi yanayoikabili sekta ndogo ya maziwa Jimboni Mkinga na Mkoani Tanga kwa ujumla. Baadhi ya matatizo hayo ni pamoja na huduma za ugani hafifu, bei ghali za dawa, ukosefu wa mitaji, soko lisilo la uhakika, upungufu wa vifaa vya kukusanyia, kuhifadhia, kusindika na kusafirisha maziwa na mazao yake. Ukosefu wa malambo nao ni mkubwa sana pengine kutokana na Wizara kutokuzingatia kwamba Tanga ina nafasi kubwa ya kuendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ni matumaini yangu kwamba, Wizara na Bodi zitazingatia nafasi nzuri tuliyonayo Jimboni, kutopuuzia hayo niliyoyataja na kuchukua hatua thabiti kutasaidia *TDCU, TADAT, Tanga Fresh* na wengineo wanaohusika, kupata ufumbuzi wa matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AGGRERY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kuleta Muswada huu katika muda na wakati muafaka. Nina hakika kwamba, ubunifu huu utasaidia sana katika kupatikana kwa masoko ya maziwa ambayo wakati mwingine wafugaji wanalazimika kuyamwaga. Aidha, nachukua fursa hii kukumbushia ombi la wananchi wa Jimbo la Siha la Serikali kuweka utaratibu utakaowawezesha wananchi wenye kipato kidogo waweze kujipatia maeneo ya Ranchi ya *NARCO* iliyopo katika Jimbo la Siha eneo la *West Kilimanjaro*. Najua Serikali imekwisha ainisha namna maeneo hayo yatakavyogawanywa au kuuzwa kupitia hata Hotuba ya Mheshimiwa Rais lakini msisitizo wangu hapa ni *formula* ambayo itawapa fursa wafugaji wadogo wadogo waweze kumiliki Ranchi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, naiomba Wizara isaidie Jimbo langu katika ukarabati wa majosho kwani hali ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai, haiwezeshi ukarabati na ujenzi wa majosho kwa maana ya uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena pongezi zangu kwa Waziri na Naibu Waziri wake.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na wenzangu kwa kusema kuwa, naiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Maafisa wake, kwa kazi nzuri ya kuuleta Muswada huu japo umechelewa. Naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maziwa kwa binadamu ni la msingi na muhimu sana kwa afya bora na lishe hasa kwa watoto na vijana. Napendekeza kama njia mojawapo ya kuwapa motisha wafugaji/wazalishaji wa maziwa, basi watoto wa shule wawe wanapata maziwa. Hii itaongeza soko la maziwa kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya sensa ya mifugo kumalizika, uwepo mpango endelevu wa kuwepo viwanda vya kutengeneza maziwa vidogo, vya kati na vikubwa ili maziwa yasiharibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya riba nafuu ipatikane kwa wale wawekezaji wa ndani, ambao wangependa kuwekeza katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wataalam na utaalam wa ufugaji wa ng’ombe wa maziwa upewe kipaumbele ili kuongeza tija kwa wafugaji ambao kwa sasa wanapata taabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madawa ya mifugo kuwa na gharama kubwa linawavunja moyo sana wafugaji, hivyo mbinu zitafutwe, madawa yapatikane kiurahisi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema tena naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kuniruhusu ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda na mimi kwa sababu ni mara ya kwanza kuongea hapa, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wawili, waliopata nyadhifa mbalimbali katika kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitapenda nijaribu kuchangia kwa kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na nitajaribu kutumia lugha ya kiutendaji zaidi badala ya lugha ya kisiasa nikimaanisha kwamba nitajaribu kwenda moja kwa moja kwenye hoja.

Kwanza, kwa nini tumeleta Muswada huu? Nina hakika wazungumzaji wote hapa wameeleza umuhimu wake na pia napenda tu niwakumbushe kwamba, maziwa bila kudhibitiwa vizuri huwa ni kisababisho cha magonjwa karibu asilimia 30 ya magonjwa ya kila siku ambayo Watanzania na binadamu tunayapata. Kwa hiyo, maziwa yasipowekwa katika utaratibu unaokubalika, kinaweza kuwa chanzo kikubwa sana cha magonjwa ya kutusumbua wananchi.

Pili, kwenye hilo nitaomba sasa niende moja kwa moja kwa mchango uliotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, napenda nimpongeze kwa kuwa na uelewa mkubwa sana wa Sekta yetu, yeye pamoja na Wajumbe wake na kwamba, wamejaribu kuuchambua Muswada vizuri sana na kutupa mawazo ambayo tumeyaingiza kwenye *Amendment* ambazo zimegawiwa.

Kwanza, idadi ya Wajumbe kama ilivyoombwa ukiangalia kwenye hati ya marekebisho sehemu (b) tumeongeza. Kuongeza Mjumbe kwenye bodi kutoka Wizara inayohusika na Masoko, hilo ningependa niwajulishe Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumeangalia uwezekano huo ambao ni mawazo mazuri tu, lakini tunachotaka hii Bodi isirudie makosa yaliyokuwepo huko nyuma. Tunapenda hii Bodi iongozwe na wahusika wenyewe moja kwa moja badala ya kuwa na watendaji wengi kutoka Serikalini. Unapozidisha watendaji wengi kutoka Serikalini, tatizo ambalo jana Mheshimiwa Benedict Losurutia alilizungumza, litajitokeza. Kwa hiyo, tunaomba sana mtuelewe kwamba, tunataka Bodi hii iendeshwe na wenyewe, mbinu zao za jinsi gani waendeshe hii Bodi zitatokana na wahusika moja kwa moja ambao ni wadau.

Kwa hiyo, tunaomba mtuelewe kwamba, tusingependa kuongeza idadi ya Wajumbe wanaotoka nje ya wahusika au ya wadau. Jina la Bodi ambalo alipendekeza kwamba iwe *Tanzania Dairy Development,* mimi nadhani kwamba tukifanya hivyo tutakuwa tunapunguza dhana nzima ambayo inahusisha pia udhibiti. Kama tulivyosema Muswada huu au sheria hii ikipita ina malengo mapana zaidi badala ya *development. Development* baada ya udhibiti, uhamasishaji, kila kitu kwenda vizuri nina hakika kitakachotokea ni *positive effect* ambayo ndiyo maendeleo.

Kwa hiyo, maendeleo yatakuja moja kwa moja. Ugani na huduma za uzalishaji ziboreshwe. Tunalielewa hilo na tulieleza kwenye Kamati kwamba kuna sheria mfano ya *Veterinary* ya mwaka 2003 imelenga hayo hayo. *Animal Disease Act* ya mwaka 2003 imelenga hilo hilo. Pia tunaleta sasa hivi sera ya uzalishaji mifugo inayoandaliwa na baadaye itatungiwa sheria.

Mheshimiwa Abbas Jecha kutoka Kambi ya Upinzani, napenda pia nimshukuru sana na ametuonyesha kwamba sio kwamba dhana inayoeleweka kwa watu kwamba kila Mpinzani kazi yake ni kupinga tu. Lakini ame-*prove* tofauti kwamba mahali penye zuri linahitaji kusifiwa na tunapenda tupokee shukrani zetu kwa dhati kwa kutupongeza.

Uwakilishi aliouomba wa kutoka kwenye vyuo vya mifugo, jibu letu ni hilo hilo kwamba Vyuo vya Mifugo vingi viko *owned* na Serikali, kwa hiyo, tutakuwa tunaongeza idadi ya wafanyakazi au watu wanaotokea Serikalini. Kwa vile tumesema Chuo kikuu ni Taasisi ya Elimu na wengi ya hao wataalamu wametokea Chuo Kikuu nina hakika kwamba tutapata uwakilishi mzuri tu kutoka Chuo Kikuu na tutapata nadharia ya kutosha kusaidia Bodi iendeshe mambo yake vizuri. Ameomba ziandaliwe kanuni maridhawa. Hilo tunalikubali na nina hakika wakati wa kuandaa kanuni tutalizingatia.

Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ameomba kupanua shughuli za ufugaji Mikoa ya Kusini. Napenda nimshukuru kwanza kwa maoni yake hayo. Lakini lazima napenda nimrudishe kwenye historia. Mikoa ya Kusini miaka iliyopita walipelekewa ng’ombe wengi tu, zikatengenezwa njia za kupelekea mifugo, lakini kwa vile dhana hiyo ilikuwa ni ya ku-*impose* tuliwapelekea kitu ambacho hawakuwa tayari. Kilicho tokea ni nini? Mifugo wengi walikufa na walikula ikawa ni kitoweo basi mambo yakaisha. Sasa tunachosema sasa hivi ni kwamba tunawaomba wao wenyewe na kwa taarifa yake Mheshimiwa Namkulala hafahamu mfano Mikindani kuna wafugaji wengi wa *zero grazing* sasa hivi. Maziwa ni mengi sana Mtwara mpaka wanalalamika soko hakuna.

Ukienda Wilaya ya Masasi kuna ng’ombe wengi sana. Sasa hali imebadilika. Lakini inabadilika kwa sababu ni *participatory* ni wao wenyewe wanahitaji wana-*participate* kuwahitaji wale mifugo unlike ilivyokuwa zamani tuliwapelekea. Kwa hiyo, ile dhana ya kuwapelekea tunaheshimu maombi hayo lakini tungeomba sana Waheshimiwa Wabunge watuelewe sio dhana endelevu.

Kwa hiyo, tunaomba wakaribishe wao wenyewe wawe *willing,* wa-*participate* na nina hakika kwamba kutakuwa na uendelevu. Lakini hata hivyo Serikali kama nilivyoeleza tumepeleka mpango wa *HPI* huu wa kopa ng’ombe lipa ng’ombe

unaendelea vizuri Masasi sehemu ambayo nimekwenda mwenyewe sio kuambiwa. *CARITAS* wametusaidia sana kwenye maeneo mengine. Pia wakati huu kwa kuwatumia *Japanese Counterpart Fund* tumepeleka miradi ambayo itakuwa na dhana hiyo hiyo ya kujaribu kuendeleza ufugaji Kusini na shilingi karibu 107 milioni zimepelekwa hivi juzi mkoa wa Lindi na tayari tupo mbioni kutekeleza mipango ambayo iko chini ya hiyo. Pia mradi wa *Tanzania Livestock Marketing* umeanza kazi ya kujenga miundombinu, kuirudishia iliyokuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niombe sana Mikoa ambayo iko Kusini hasa Wilaya ambazo ziko karibu na maeneo ya mifugo hii inakopita kwa sababu ya kudhibiti magonjwa wawe makini sana kutokupitisha mifugo bila ya kuwa na vyeti husika na bila ya kuwadhibiti kana kwamba sio wagonjwa. Kwa sababu tunapenda Kusini wasipate matatizo tuliyonayo Kaskazini ya magonjwa.

Kwa hiyo, tungependa sana hasa wanaosimamia Daraja la Mkapa ambapo mifugo mingi sasa hivi wanapita wajaribu kuwa na udhibiti wa kutosha ili mifugo yote inayopita kwenda Kusini wawe na vyeti vinavyohusika na tuna hakika kwamba hawana matatizo ya magonjwa.

Mheshimiwa Talala Mbise, majukumu ya Bodi ni mengi. Inaeleweka. Bodi ya zamani iliyokuwepo mambo yote walikuwa wanayafanya lakini siku hizi kuna dhana tofauti mahali ambapo shughuli ni nyingi wana *outsource* wanaweza kuajiri *consultant* wa nje akawafanyia. Kwa hiyo, majukumu sasa hivi sio tatizo kwenye Bodi tunazoziunda sasa hivi. Kwa vile ni za wahusika moja kwa moja mahali ambapo uwezo hawana wanaweza ku-*outsource. Unlike* pale zamani ilikuwa kwamba kila kitu lazima Bodi hiyo ifanye, kwa hiyo, hili sio tatizo tena. Wafugaji wanakopwa na kuuza maziwa bila mikataba. Hilo nina hakika tumekubali Muswada tunaopendekeza kwenu Waheshimiwa Wabunge unasema kwamba Bodi hii kazi mojawapo itakuwa ni hiyo wakishirikiana na *Tanzania Food and Drug Agency* ambayo ni Shirika ambalo Waheshimiwa Wabunge walipitisha sheria yake hivi karibuni.

Kituo cha *NAIC* kutokuwa na usafiri wa kutosha. Hilo linaeleweka lakini pia tunaangalia kwamba hii kati ya *artificial insemination* ni vizuri pia isiachwe *NAIC.* Tuna-*invite private sector* wahusike. Nina hakika kwamba ni kazi nzuri na inaweza kulipa.

Kwa hiyo, tutakapopata *private sector* wanahusika kusambaza teknolojia hii au kusambaza mbegu kwa ajili ya uamilishaji nina hakika kwamba tutakuwa na uwezo mkubwa zaidi badala ya kuangalia kituo kimoja *NAIC* kwa nchi nzima. Mradi wa kopa ng'ombe tunakubaliana naye na kawaida huu mradi unaendeshwa na *HPI* ambayo ni *NGO.*

Kwa hiyo, kama una tatizo la kutaka uongezewe kiwango cha mradi ni vizuri zaidi ukawaona wahusika kwenye maeneo na kama mradi wenyewe unaonekana kuwa na manufaa kwenye eneo husika nina hakika kwamba hawawezi kukataa kupanua mradi kwenye eneo hilo.

Tatizo la soko la maziwa, hili limeelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Lakini ndiyo hivyo tumejaribu kwa kiwango kikubwa baada ya udhibiti kuwepo. Programu zote hizi ambazo tumeomba na Waheshimiwa Wabunge wamezizungumzia tutajaribu kushirikiana na Wizara husika kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Utamaduni ili tuone jinsi gani tunaweza kuhamasisha unywaji wa maziwa. Hiyo tuna mfano hatuhitaji kuangalia mbali.

Kenya, Rais Moi wakati ule aliamuru tu siku moja kwamba wanafunzi wote wapewe maziwa na hilo rika la wanafunzi sasa hivi ni watu wazima. Lakini kwa vile wamekuwa wakizoea kunywa maziwa *consumption* ya maziwa Kenya iko juu sana na inatokana na hilo kwamba unawaanzishia kunywa maziwa wakiwa wadogo watakapokuwa inakuwa ni mazoea. Ni kweli kwamba watu wetu hapa sisi kama alivyosema Mheshimiwa Benedict Losurutia jana na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, leo bado kwamba kunywa chai ya rangi au kunywa chai ya suturungi tunavyoijua, inakuwa ni sifa, lakini kwa kweli sio kitu kizuri ni vizuri tujizoeshe kunywa chai ya maziwa, kunywa maziwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maziwa kama ninavyofahamu ukiwa kwenye biashara ya maziwa huwezi ukapoteza. Maziwa yakiwa *fresh* yananyweka kama *fresh.* Maziwa yakianza kuharibika yanatengenezwa *yoghout,* yakionza kabisa yanatengeneza *cheese.* Kwa hiyo, maziwa *literary* hayatupwi ila yanahitaji miundombinu au viwanda na *processors* ambao wataji-*engage* kwenye uzalishaji wa maziwa.

Tatizo la maji kwa mifugo Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Talala Mbise amelizungumzia. Jitihada kama tulivyosema tunajaribu kila siku, tunapeleka fedha kwenye Halmashauri zetu kwa bahati mbaya sana baadhi ya Halmashauri hawatusaidia sana kabla hujawapelekea fedha wanasema tuleteeni fedha. Ukiwapelekea fedha wanasema fedha hazitoshi. Hawa-*attempt* hata kuongeza fedha ambavyo mikataba yetu na wao inavyowahitaji wafanye. Utakuta wakati mwingine maeneo ambayo tumeyasema kwamba tumeyatengea fedha hawana habari kwenye maeneo yale. Ndio maana sasa hivi tumeweka utaratibu fedha hizi tukizipeleka sasa hivi kwenye Wilaya tutajitahidi sana kuwapa nakala Waheshimiwa Wabunge ambao huenda watatusaidia sana katika kuhamasisha tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, amezungumzia na yeye mambo mengi sana ukosefu wa kuendeleza mifugo ambao ni wa asili. Nakubaliana naye ndiyo kazi ambayo tunataka kuifanya na kituo chetu cha Mpwapwa tunataka kuki-*revive* zaidi ili *Mpwapwa Breed* kiweze kufanya kazi hiyo ili kuweza kuzalisha mbegu ambayo inastahimili matatizo ya hali ya hewa ya hapa.

Tafsiri ya maneno ya *diary.* Mheshimiwa Ndugai, sisi tunachofanya hatu-*event a wheel.* Tumechukua *non mancreature* ambayo inatumika kwenye *WTO,* tumetumia *terminology* hiyo hiyo ambayo inatumika kwenye *Internal Trade Centre* na kadhalika. Kwa hiyo, maana ya *diary* kwa mujibu wa Muswada huo ndio tafsiri sahihi kama ilivyowekwa kwenye Muswada.

Pia *designated milk* inamaanisha ni maziwa *rather than* maziwa ya ng'ombe ikimaanisha maziwa ya mbuzi, nyati, ngamia, kondoo na kadhalika. Ndiyo tafsiri iliyoko katika vitabu. Tukitaka tubadilishe tunaweza kuja kukwama kwa sababu tuna-*expect* kwamba *export* ya maziwa hapo baadaye itakuwa kubwa na hivyo lazima *to harmonise terminology* na *classification* ya *tariffs* zetu ili tuweze kuendana na zile za Kimataifa.

Kuhusu usajili hata wa wafugaji wadogo wadogo, nadhani baada ya kupitia nakumbuka ulizungumza jana lakini nadhani baada ya kupitia Muswada zaidi umeangalia kifungu namba 2(2) kinaeleza kabisa kinaweka bayana kwamba: "Muswada huu unahusu wazalishaji kwa ajili ya biashara."

Sasa hawa wengine wadogo wadogo ndio maana tuna-*encourage* kuwa na *cooperatives* ambazo kutakuwepo na mkusanyaji mdogo ambaye sasa atakuwa *registered* kama mfanyabiashara wa maziwa kwa lengo la Muswada huu. Kwa hiyo, hilo nina hakika umeliona Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Anne Makinda, kutokamilika kiwanda cha maziwa cha Njombe. Hiki kiwanda nina hakika hivi karibuni kinaweza kumalizika kwa sababu hakiko chini yetu moja kwa moja, kiko chini ya *Njombe Livestock Farmers Association* kwa kushirikiana na *CEFA,* Shirika lisilo la Kiserikali la Italy. Kiwanda hiki kina uwezo mkubwa kikimalizika, lakini nina hakika huenda wakawa na tatizo la kupata *raw material.* Wenzangu mnafahamu Njombe ng'ombe wapo, lakini wako huru sana *unlike* maeneo mengine.

Kwa hiyo, kuja kuwa *time* wale ng'ombe wapate maziwa ya kutosha kuzalisha lita 40,000 kwa siku nina hakika wana kazi kubwa. Lakini nina hakika Mheshimiwa Mbunge atahamasisha watu wake akishirikiana na uongozi wa Wilaya husika. Matumizi ya samadi, namshukuru sana kama wameliona hilo Njombe. Kwa kweli ni vizuri zaidi kuliko kutumia mbolea ya chumvi chumvi ambayo imesababisha ardhi ya huko Kusini kuwa dumavu kwa sababu bila ya kuitumia hiyo mbolea sasa hivi ni vigumu sana uzalishaji kufanyika.

Mheshimiwa Musa Lupatu, napenda nirudie kwa kumpongeza sana kwa mawazo yake, *very creative* na *very logical* na ametusaidia sana hata kwenye Kamati. Napenda nishukuru kwa mchango ambao ameutoa kwenye Kamati na huu mchango ameutoa hapa. Lakini jibu la tafsiri hii ya *diary* nina hakika amelipata kwenye maelezo yangu yaliyopita.

Mheshimiwa Benedict Losurutia, amesema Bodi isiwe tegemezi. Nadhani nimelieleza hilo kwamba Bodi sio tegemezi kwa sababu haitafanya kazi kama Bodi zilizokuwepo. Bodi hii ni ya wahusika wenyewe na ndiyo maana *majority* ya *Board Members* wanatokana na *council* ambayo ni ya wadau. Unywaji wa maziwa kwa watoto wa shule. Napongeza sana hilo na ninapenda tulifanyie kazi kwa pamoja kwa sababu hiyo inahitaji dhana nzima kubadilisha mtazamo mzima wa kutokea kwa wazazi kwa Wizara husika, Halmashauri zetu na kadhalika. Itakuwa ni rahisi zaidi hata kama tukiomba usaidizi kutoka nje sisi wenyewe tuwe kwanza *ready* kwamba tumeishaanza.

Napenda nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wilaya ya Hai nadhani ndio Jimbo la Siha na Hai. Tulipoomba wafanye hivyo wamefanya hivyo kwa bidii sana na Wilaya moja ya mkoa wa Arusha nadhani Arumeru napenda sana niwapongeze kwa niaba ya Wizara kwamba wameitikia wito huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ubora wa maziwa yanayozalishwa na wafugaji wadogo wadogo. Nina hakika hilo ni wazo zuri lakini pia sasa hivi tulipitisha sheria hapa Bungeni ya *Tanzania Food and Drug* hao wakishirikiana na matokeo ya Bodi hii nina hakika kwamba ubora wa maziwa na bidhaa zetu zitakuwa nzuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, amezungumzia mambo mengi sana. *Importance* ya maziwa kwa *humans.* Umezungumzia juu ya kuongeza *functions* ihusishe *mobilisation* lakini ningependa Mheshimiwa Profesa Maghembe uelewe kwamba ukiusoma Muswada *in totality focus* yake ni kuhamasisha kwa sababu hawa tuseme Bodi au *council* inatokana na wadau wenyewe. Sasa hawa wadau wenyewe *interest* yao wengi wanatoka *private sector. Interest* yao ni ku-*make money.*

Sasa katika ku-*make money definitely* vitu vingi vya zamani tulivyokuwa tukivifanya vilikuwa havina motisha kwa sababu vingi vilikuwa vinafanyika kama kawaida, havikuwa na motisha ule wa kwamba nitengeneze faida au nitengeneze fedha zaidi.

Kwa hiyo, ukiangalia Muswada wenyewe *in totality* una-*mobilise* sekta ndogo ya maziwa ili iwe endelevu. Kwa hiyo, hata tukiweka maneno kama utendaji wa Bodi hii hautakuwa na maana nzima ya Muswada unakolenga itakuwa ni kazi bure. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa kutuomba kutuongeza haya maneno lakini tuangalie totality ya Muswada na wenyewe ume-*focus* kwenye dhana ipi.

Napenda pia nimshukuru sana Profesa Maghembe kwa *calculation* zako. Ni kweli *actually* ulisema 120 bilioni, sio 120 bilioni kwa *calculation* zako kwa hesabu za haraka haraka hii sekta ilitakiwa ku-*generate over 4,000,000,000 shillings* kwa mwaka. Kwa *calculation* ya ng’ombe hao 20,000 uliowasema wakizalisha lita 10 kila siku na kwa bei iliyopo sasa hivi ambayo ni *prevailing* ya *minimum* ya shilingi 200/=. Kwa hiyo, tulitakiwa kuzalisha kuwa na *input* kubwa sana kutoka kwenye zao la maziwa ambalo ingesaidia sana katika kutatua *balance of payments* ya nchi na kupunguza umaskini kwa wafugaji wetu.

Ushirikiano na Halmalshauri umelieleza hilo kwamba ni tatizo lakini kwa sasa hivi baadhi ya Halmashauri zimeanza kubadilika na zinatusaidia sana. Kama unavyofahamu wakati ilipokuwepo kodi ya mifugo ukienda kwenye *full council* wakati watendaji wanaulizwa maswali. Daktari wa Mifugo wa Wilaya akisimama anaulizwa umekusanya kiasi gani badala ya kuulizwa ng’ombe wangapi umechanja mwaka huu au majosho mangapi yamekuwa *repaired.*

Kwa hiyo, fedha zote walikuwa wanachukua kama kodi za mifugo lakini zilikuwa hazirudi. Lakini Wizara imetoa fedha nyingi sana mwaka jana na mwaka huu. Kwanza

kwa kurekebisha majosho, pili kwa ajili ya kuchimba malambo. Kwa hiyo, nina hakika kwamba wale ambao Waheshimiwa Wabunge waliosema kwamba tuongeze nguvu sisi tunaanza kuliona hilo. Mfano *control* ya magonjwa ningependa tu-*focus* Kusini ambako hakujawa na *contamination* kubwa ya matatizo. Tukiweza kufanya Kusini kuwa *Disease Free Zone* wafugaji wa kule nao utatuwezesha hata *export* ya nchi za nje kuwa rahisi zaidi.

Halafu pia majosho na kadhalika tunajaribu kuangalia uwezekano hata tukope fedha Benki *focus a few districts* zilizo na wanyama wengi ili tuwawekee majosho tuunde vyama vya watumiaji kwa sababu kuna sehemu nyingine tumeona vinafanya kazi vizuri sana ili Wilaya hizo tuweze ku-*eradicate* haya matatizo madogo madogo kama yalivyoelezwa ya kupe na kadhalika. Kwa hiyo, ninapenda nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Maghembe, kwa mawazo yake hayo.

*Processing and packaging definitely* ile ni *function* ya *demand* na *supply. Demand* ikawepo *you will definitely improve your processing.* Kwa sababu ya ushindani *definitely* uta-*improve* hata *packaging* ili *the static part* ya *product* yako iwe *attractive compared* na *import* na ushindani. Kwa hiyo, hilo naona ni wazo zuri ambalo pia nina hakika kwamba litasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mchango mwingine wa Mheshimiwa Jenista Mhagama. Tunashukuru kwa pongezi. Mradi wa ng'ombe wa maziwa Kusini. Nina hakika tumeshirikiana naye sana na nina hakika ameanza kuona kwa jinsi gani Wizara inaanza kutazama Kusini kama inavyotazama sehemu nyingine na kwamba ushirikiano wake na Waheshimiwa Wabunge wengine wa Kusini utatuwezesha kwenda *speed* kubwa zaidi kuliko tulivyokwenda *speed* upande wa huku sehemu nyingine ya nchi.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, nashukuru kwa pongezi. Kama nilivyoeleza kwenye maeneo mengi suala la maziwa shuleni tujaribu kushirikiana pamoja ili tuweze kulitatua na kulihamasisha lianzishwe karibu nchi nzima ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea. Maelezo ya Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro ameyatoa kwa maandishi. Ugani hafifu inaeleweka na hilo ni tatizo ambalo limejitokeza kwa kipindi cha miaka mingi sana na nina hakika sasa hivi tumeanza kuona jitihada ambazo tunazifanya kama Wizara.

Kuhusu u-ghali wa madawa ya mifugo, Waheshimiwa Wabunge wengi wamelalamikia juu ya u-ghali wa madawa. Lakini hili tatizo saa nyingine halipo, mimi nadhani kwa madawa tu ya mifugo. Nitawapa mfano mdogo juzi niliuliza bidhaa fulani Dar es Salaam nikaambiwa ni kama shilingi 200,000 na kitu. Nikazunguka *within* Dar es Salaam nikakuta duka moja lingine wanauza *almost half* 140,000. Basi mimi nikaacha nikampigia simu mtu mmoja anatoka Dubai akanunua hicho kitu kwa shilingi 15,000/=.

Sasa utakuta kwamba hizi *price disparity* saa nyingine zinasababishwa na au *demand* ndogo au pia *ignorance.* Pia watu bahati mbaya sana sisi hatujui *window shopping.* Kwa hiyo, tuko *on most cases uninformed* ya hata bei, *uninformed* ya ubora

wa bidhaa. Unakuta kitu ni *counterfeit* lakini unakuta anauziwa kwa bei ya kitu ambacho ni *genuine.*

Kwa hiyo, haya matatizo ni *complex* kidogo huwezi ukaya-*single out* ukaona kwamba ni tatizo tu na kwamba hawa wanaotoa ugani wana nia ya ku-*lip off.* Lakini utagundua kwamba saa nyingine *level* yetu ya *understanding* pia kwa maeneo mengi ambayo yanatuhusu kila siku inakuwa na tatizo kidogo. Kwa hiyo, napenda nimshukuru Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, kwa wazo hilo.

Mheshimiwa Daniel Yona, ameelezea kuhusu maziwa yatolewe shuleni. Tuangalie uwezekano wa kutumia fedha tunayoitenga kwenye *HIPC.* Ni wazo zuri na nina hakika Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia na napenda nimshukuru. Mheshimiwa Remidius Kissasi unywaji wa maziwa mashuleni, ni hilo hilo. Upatikanaji wa madawa nalo ni tatizo. Nina hakika kama nilivyosema *demand* ikiwa kubwa *supply* itakuwa kubwa na *supply* ikiwa kubwa *competition* itakuwepo na *competition* ikiwepo bei zitakwenda chini na *cost* ya *services* zitakwenda chini.

Kwa hiyo, napenda nilisisitize kwamba hali yenyewe ilivyo sasa hivi kwamba *demand* sio kubwa kwa sababu watu wengi hawajahamasishwa. Sasa hivi kutokana na sheria tunazozitunga sasa hivi haitakuwa tena ni hiari. Zamani ninafahamu mliokuwa wafugaji wa miaka mingi ilikuwa sio hiari kuogesha mifugo, ilikuwa ni lazima. Sasa lazima turudishe hiyo kwamba ni lazima kuogesha mifugo.

Mimi siwezi kuogesha mifugo yangu halafu yako hukuogesha, kesho na kesho kutwa wanakwenda kukutana huko kwenye sehemu ya malisho halafu wanaambukizana magonjwa. Kwa hiyo, hizo sheria tutazifufua na tutazisimamia na nina hakika Halmashauri watatusaidia kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu na nina hakika kwamba maeneo ambayo sikuyagusa Mheshimiwa mtoa hoja ataweza kuyaelezea. Baada ya kusema hayo naomba kuunga hoja mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunikaribisha tena nihitimishe hoja niliyoitoa jana jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima nikiri kwamba kwa kweli kazi ya kujibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge ameifanya vizuri sana Mheshimiwa Anthony Diallo, napenda kumshukuru sana. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge wataridhika na majibu yake tuliyoyatoa na mimi nitapitia maeneo machache sana kwa kweli kuyawekea umuhimu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na mimi nianze kama wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa

kuwa Marais. Wamelijengea heshima Bunge letu na nchi yetu, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, toka jana mimi nimefarijika sana vitu viwili. Kwanza Muswada huu walioandaa ni wadau wenyewe zaidi. Wadau ndio wameleta mapendekezo yao sisi tume-*facilitate.* Tumewezesha tu kuleta Bungeni lakini kazi kubwa ni ya wadau wenyewe. Kwa hiyo, imenipa faraja kwamba watu wetu wenyewe sasa wanashiriki na wanafanya mambo yao katika sekta ya mifugo. Lakini la pili angalau Bunge sasa linazungumza habari ya maendeleo ya mfugaji. Inatia faraja kubwa sana kwamba Bunge hili linazungumza habari ya maendeleo ya wafugaji inatia faraja kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu upeo na uelewa wa Waheshimiwa Wabunge katika masuala haya ni mkubwa sana, nawapongeza sana wale waliochangia. Sasa ningeomba kuwatambua wale waliochangia kama ifuatavyo: Mheshimiwa Eliachim Simpassa, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Anthony Diallo. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Daniel Yona, Mheshimiwa Remidius Kissasi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Mwanne Mchemba na Mwalimu wangu Mheshimiwa Rhoda Kahatano. Ninawashukuru hata wale ambao wamekaa kimya na kutuunga mkono katika suala hili. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja tulizungumza wote tunakiri ni suala la unywaji wa maziwa. Namshukuru sana Profesa Maghembe amelieleza hapa vizuri sana na Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Daniel Yona katika maelezo yake. Tatizo la msingi kwanza Watanzania hatunywi maziwa ndiyo tatizo la msingi.

Waheshimiwa Wabunge, sio utani nitatoa takwimu. Kwa mwaka Waingereza wanakunywa lita 123 kwa mtu. Wa-Swedish wanakunywa lita 157, Waholanzi wanakunywa lita 111 kwa mwaka, mtaniambia ni Ulaya. Twende Kenya lita 84 kwa mwaka, Uganda wanakunywa lita 40 kwa mwaka, Tanzania lita 33 kwa mwaka.

Kwa hiyo, tuna tatizo la msingi la kwanza la Watanzania kutokuwa na utamaduni wa kunywa maziwa. Kwa hiyo, nakubaliana sana na wale wenzangu waliosema tuujenge utamaduni wa kunywa maziwa. Hilo ni muhimu sana na ndiyo maana nakubaliana na mapendekezo mengi kidogo ya kwamba tuanzie shuleni kama alivyosema Mheshimiwa Anthony Diallo na Waheshimiwa Wabunge wengine. Tuanze shuleni kwa kuwapa watoto maziwa na ni heshima kwa nchi yetu. Kwamba watoto wetu wanakunywa maziwa. *(Makofi)*

Kama alivyosema Mheshimiwa Benedict Losurutia maziwa yanasaidia kidogo kuongeza akili kwa hiyo, inafaa sana tuwapatie watoto wetu. Tumejaribu jitihada hizi hasa katika Wiki ya Maziwa. Tuliandika barua kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya nchi

nzima kujaribu kulihimiza jambo hili. Kama alivyosema Mheshimiwa Anthony Diallo, kuna Mikoa inafanya vizuri Arusha hasa Wilaya ya Arumeru wanafanya vizuri na Arusha Mjini nawapongeza sana. Kilimanjaro wanafanya vizuri hasa Wilaya ya Hai kwa Mheshimiwa Aggrey Mwanri wanafanya vizuri sana na Dar es Salaam wameanza, lakini rafiki zangu wa Pwani, Lindi na Mtwara hali ni mbaya sana, mbaya kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema kwa kweli tuanze jitihada hizo za kuhimiza watoto wetu wanywe maziwa ili tujenge utamaduni wa kunywa maziwa na watu wazima pia. Tumezoea sana sisi kunywa soda hizi, sasa daktari hayupo leo hakutuambia kwa nini Wabunge wengi tunapata kisukari, lakini nadhani pamoja na kutofanya mazoezi, aina ya vyakula tunavyokula vinachangia kupata magonjwa hayo. Sasa ukinywa maziwa badala ya soda nina hakika utapunguza kasi ya maradhi kuliko ambavyo ungeongeza. Kwa hiyo, naomba kwa kweli tujenge utamaduni wa kunywa maziwa na tuhimizane kunywa maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo limezungumzwa kwa ufasaha mkubwa sana na nawashukuru sana Wabunge wote waliochangia ambao ni Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Anne Makinda na wote waliochangia eneo hilo la magonjwa ya mifugo nawashukuru sana. Tena uchambuzi wenu ni sahihi kwamba Tanzania kinachoua mifugo mingi hapa ni magonjwa ya kupe (Ndigana). Leo tukiweza ku-*control* magonjwa ya kupe tuna hakika tutaongeza mifugo mara mbili, mara tatu na mnajua pia kwamba dawa ya hakika ya magonjwa ya kupe ni kuogesha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Mheshimiwa Anthony Diallo hapa, wakati wa mkoloni ilikuwepo sheria kwamba ni lazima uogeshe mifugo, usipoogesha mifugo faini. Tulipopata Uhuru nadhani tukafutafuta hilo. Botswana leo iko sheria, ng’ombe wako akikutwa na kupe, kila kupe kwa wakati ule adhabu yake ilikuwa ni kama shilingi 5,000/=. Kwa hiyo, sheria zimebana wafugaji waogeshe mifugo.

Waheshimiwa Wabunge, nakubaliana nanyi kwamba madawa bei ni juu. Moja ya maelekezo ya Rais alipozungumza kule Arusha alisema tuangalie uwezekano wa kupunguza bei ya dawa za mifugo. Tunazungumza na Wizara ya Fedha tuangalie uwezekano wa ile ruzuku mliyokuwa mnaisema kama tunaweza kuelekeza kwenye madawa ya majosho. Mazungumzo yanaendelea yakikubalika kwenye bajeti hii nategemea tunaweza kutafuta *formula* ya kusaidia kupunguza gharama ya madawa ya majosho. *(Makofi)*

Lakini kwa sasa ningependa bado kuhimiza kwamba Halmashauri zisimamie kazi hizo na kuhimiza kwamba pale watu binafsi wanapojiweza tafadhali waifanye kazi hii. Kutengeneza josho lako mtu mfugaji si tatizo sana, kwa sababu kwa kweli kutibu siku hizi ni ghali sana. Wanatuambia kuna *Butolex* ile inasaidia kutibu magonjwa ya Ndigana, lakini haisaidii kwa kiasi kikubwa kwani mimi nimejaribu. Wiki mbili zilizopita nimepata *crisis* ya Ndigana kwa sababu vijana wangu wanaohusika na josho walikosea kuchanganya dawa. Nimepata *outbreak* ya Ndigana kubwa sana, nimetumia

*butolex* nyingi tu, lakini ng'ombe wamekufa. Kwa hiyo, bado kuna tatizo kwa kweli la bei ya dawa na uogeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, walisema Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Talala Mbise juu ya kituo cha *NAIC* na ameeleza Mheshimiwa Naibu Waziri hapa kwamba tunatengeneza *National Breeding Policy.* Lakini kwa kweli *National Breeding Policy* hii tumeamua tuitoe ile Sera ya Mifugo ambayo iko kwenye Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1977, tuinyofoe ile Sera ya Mifugo mle tuiimarishe kidogo na mle ndani ndiyo tuweke Sera ya Uzalishaji ambayo ilikuwa hamna. Kwa nini tunafanya hivyo? Tunafanya hivyo kwa sababu hapa nchini sasa hivi kila mtu analeta mbegu yake, kila mtu. Inatoka mbegu Marekani, inatoka mbegu Uingereza inatoka Israel na kila mahali, ziko hapa Dar es Salaam zimejaa nyingi sana. Sasa, hauwezi ukaongoza Sekta ya Mifugo kwa utaratibu huo, hapana, utaleta *confusion* ndani ya mifugo.

Kwa hiyo, tunataka tutengeneze utaratibu ambao utasimamia kisheria uingizaji wa mbegu hizi ili tukubaliane unataka ng'ombe wa aina gani, siyo unakwenda kiholela tu. Sasa kwa sasa hivi kwa kuanzia, kituo chetu cha *NAIC* kinafanya kazi nzuri sana, nzuri sana.

Mheshimiwa Talala Mbise, nilifikiri wewe ungeshukuru kwa sababu kiko karibu na wewe. Wenzako walioko Mtwara kiko mbali nao, lakini kwa watu wa Arumeru najua mnakitumia sana, mnaweza kukitumia vizuri zaidi. Mwaka 2003 tumepeleka dume ambalo lina uwezo wa kutoa ndama akizaa maziwa yake ni lita 35 kwa siku, ndiyo liko pale. Tumetoa kutoka wenyewe wanaita, jina la kitaalam wanaita wataalam wangu aah, sioni ile lugha.

**MBUNGE FULANI:** Hivyo hivyo.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Hivyo hivyo! Lina jina lake. *(Kicheko)*

Ni kwamba ameandaliwa maalum kwa ajili ya mbegu, tumemtoa Afrika Kusini, yuko pale *NAIC* na wafugaji tunawakaribisha sana. Nimepata habari sasa hivi watu wanakwenda kufuata zile mbegu kwa kasi nzuri sana, ili tusaidiane kubadilisha mbegu yetu na kuongeza uzalishaji kama ambavyo Mheshimiwa Job Ndugai unapendekeza ndivyo tunavyofanya. Lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Mpwapwa ndiyo tunafanya kwa ajili ya mifugo wale wengine wa kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa sababu kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri amemaliza hoja nyingi, ningependa kuzungumza kidogo habari ya mifugo Kusini. Sasa rafiki yangu, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala leo hayupo hapa, amenikimbia tena, lakini Mheshimiwa Benedict Losurutia alijibu pale akasema unapokuja kununua mahindi Kiteto chukua na ng'ombe, peleka ng'ombe Kusini. Pia na mimi kwa kweli nawahamasisha hivyo hivyo kwamba kama tunavyofanya biashara ya mahindi tufanye pia biashara ya mifugo, kupeleka mifugo Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna kasi kubwa sana ya Wasukuma, Wamasai, Wabarbaig kuvuka daraja la Mkapa kupeleka mifugo Kusini kwa *speed* kubwa sana. Tumewaambia viongozi wa Mikoa hiyo, pamoja na kwamba tunakubaliana na ninyi mpate mifugo, lakini tungetaka Mikoa ya Kusini ikafuga badala ya kuchunga kama tunavyofanya Kaskazini na kwa hiyo twende kitaalam basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesaidia sana, pale Lindi unapoingia darajani tumeweka kituo cha kuhakikisha kila ng'ombe anayekwenda Kusini amepimwa ili asiende na magonjwa. Tunataka Mikoa ya Kusini iwe ndiyo *DiseaseFree Zones* hakuna magojwa kule, magonjwa yako huku kuliko na mifugo, ili ikiwezekana tutumie bandari ya Mtwara kuuza nyama nje. Lakini tutaweza kama mifugo inayoingia Kusini itafuata utaratibu na hasa viongozi wa Halmashauri na Mikoa kuhakikisha ng'ombe haingii bila cheti cha kuthibitisha kwamba hana magonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiserikali tumeanza kuchanja *CBDP,* hawana *CBDP* lakini tunachanja ili wasiwe nayo, ili tuwe na hakika kwamba Mikoa yetu ya Kusini ni *Disease Free Zone.* Sasa nawaomba viongozi wa Mtwara, Lindi na Ruvuma tusaidiane kuifanya kazi hiyo kitaalam ili watu wa Kusini wafuge badala ya kuchunga na kuchunga maana yake hata huko wanapokwenda lazima waonyeshe maeneo yao na waambiwe kutoka hapa mpaka hapa tu basi, huwezi kwenda zaidi na kutoka hapa mpaka hapa itakuwa mifugo, kutoka hapa mpaka hapa itakuwa kilimo na taratibu ziwekwe na zisimamiwe. Hivyo nina hakika tunaweza kufuga vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama alivyosema Naibu Waziri, kwa Mkoa wa Ruvuma tumewasaidia na tumepeleka shilingi milioni 107 na zile ambazo mchango wetu ulikuwa unatakiwa tumepeleka wiki iliyopita shilingi milioni 13 kuendelea kusaidia jitihada za ufugaji katika Mkoa wa Ruvuma. Tunatafuta fedha kwa Mkoa wa Lindi, tumeahidiwa shilingi milioni 125 na tunategemea hivi karibuni vile vile tutazipeleka huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunasema kwa kweli tungetaka Kusini wafuge badala ya kuchunga. Jitihada zetu ni za kuwasaidia ili mambo yaende vizuri. Muswada huu madhumuni yake ni kuwasaidia basi hao wafugaji ambao wanataka kufanya biashara ya maziwa wafanye biashara hiyo kwa utaratibu muafaka na kwa utaratibu unaokubalika Kitaifa na Kimataifa. Nina hakika kabisa tukiwawekea sheria hii tukawawekea mazingira mazuri wananchi wetu wataondoa umaskini na pato la Taifa litakuwa limeongezeka kutokana na Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwamba Bunge la mwezi wa 10 tutaleta pia Muswada hapa juu ya *beef* (nyama) na yenyewe tuitengenezee utaratibu kama huu wa jinsi ya kushughulikia nyama. Mwezi wa sita tunafungua hapa Dodoma kiwanda cha kisasa kabisa cha kuchinja nyama na tunategemea tutaikaribisha Sekta binafsi. Tumeshajenga sisi, tunataka kuwaalika Sekta binafsi tuwakabidhi wakiendeshe kisasa ili na sisi tufanane na dunia nyingine katika suala zima la uendelezaji mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Waheshimiwa Wabunge wametuunga mkono. Ninapenda kuwashukuru sana na ninategemea tutaendelea kusaidiana ili kwa kweli Sekta ya Mifugo sasa ionekane inakwenda kwa kasi inayopasa kama ambavyo Chama cha Mapinduzi kiliahidi katika Ilani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Bidhaa za Maziwa wa Mwaka 2004**
***(The Diary Industry Bill, 2004)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2

*(Majedwali yalilotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Bidhaa za Maziwa wa Mwaka 2004**
***(The Diary Industry Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa baada ya Kamati ya Bunge Zima kuupitia Muswada wa Sheria uitwao *The Diary Industry Act, 2004* kifungu kwa kifungu pamoja na mabadiliko yake na kuupitisha kama ulivyo, hivyo basi naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa The *Diary Industry Act, 2004* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaarifu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwamba, Muswada wake atausoma jioni. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.19 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Serikali kwa Wanafunzi na Vyuo Vya Elimu ya Juu wa Mwaka 2004,**
***(The Government Students Loan Board Bill, 2004)***

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niseme machache, kabla sijasema hayo machache, kwanza nakushukuru kwa kunipatia muda huu kuweza kuchangia katika hoja hii ambayo imewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Pili na mimi kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza hadharani hapa katika Bunge hili, napenda niwape pongezi wenzetu Wabunge katika Bunge lako Tukufu, ambao wameteuliwa kuwa Marais katika vikao mbalimbali katika Afrika na Dunia. Tumepata Marais wawili katika Bunge hili ila wa watatu mlikuwa hamfahamu kwa sababu hakujitangaza ndiyo huyu aliyesimama mbele yenu ambaye ni Rais wa Mawaziri wote wa Elimu katika Afrika. Niliteuliwa Dar es Salaam mwaka 2002 na nitakuwa Rais kwa muda miaka mitano. Kwa hiyo, nakupa pongezi Mheshimiwa Naibu Spika, una Marais watatu katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme machache kuhusu umuhimu na haja ya kuwa na elimu kwa jamii yoyote, bila ya mtikisiko wowote sisi sote tunatambua kwamba elimu na hasa elimu ya juu ndiyo chanzo cha nguvu kazi inayohitajiwa kwa maendeleo ya jamii yoyote. Viwango vya maendeleo ya jamii, tofauti vinapimwa na vinatofautiana kwa kuangalia viwango vya maendeleo ya elimu katika jamii zinazolinganishwa.

Elimu na hasa elimu ya juu ndiyo inayotoa stadi za kisayansi na kiteknolojia kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Huu ni ukweli usiyokanika, unaobainika siku hadi siku hasa katika zama hizi za utandawazi ambapo jamii yoyote ile yenye elimu duni haina nafasi kabisa katika mapambano ya uzalishaji mali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mpaka kufikia takribani miongo mitatu iliyopita jukumu la kugharamia elimu ya juu katika nchi zote za Afrika lilikuwa ni jukumu la Serikali. Serikali zetu ambazo zilikuwa bado ni changa kwa maana ya kwamba ndiyo kwanza zilikuwa zimetoka katika mapambano ya uhuru, zililipia gharama zote muhimu za elimu ya juu.

Gharama hizo ni pamoja na ada ya masomo *(tuition),* chakula, malazi, vitabu, viandikwa, mahitaji maalum, mafunzo kwa vitendo, utafiti na matibabu. Gharama hizo ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia mojawapo ya kuisaidia Serikali kugharamia elimu ya juu ni ile ambayo imewashirikisha wadau wote wanaonufaika na elimu hiyo kuichangia na vile vile kuitumia vema nafasi za masomo zilizopo ikiwa ni pamoja na fedha chache zinazotokana na kodi za wananchi. Miundo mbinu iliyokwishajengwa katika taasisi za elimu ya juu na vile vile taasisi hizo kujihusisha na uzalishaji mali. Katika kuchangia elimu yao wanafunzi nao hujilipia nauli za kwenda na kurudi vyuoni, ada ya uanachama katika jumuiya zao, fedha za tahadhari, chakula na malazi. Huu ni utaratibu ambao tumekuwa tukiutekeleza awamu tangu mwaka 1994 wakati sera ya uchangiaji elimu ya juu ilipopitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ni lazima tukubali kwamba jitihada za wananchi kuchangia elimu ya juu pamoja na jitihada za Serikali kuendelea kuwadhamini baadhi ya wanafunzi kulingana na uwezo wake hazijaleta manufaa makubwa katika kuwafanya wananchi wanufaike kikamilifu na elimu ya juu kama ilivyotarajiwa. Miaka kumi baada ya kutekeleza utaratibu huo imedhihirika wazi kwamba wanaonufaika ni sehemu ndogo tu ya jamii, hususan wale wenye uwezo kiuchumi. Wazazi wengi hawawezi kuchangia kutokana na kipato kidogo na kwa sababu hiyo hiyo, hawawezi kuwapeleka watoto wao katika taasisi binafsi za elimu ya juu hata kama watoto hao wana uwezo na sifa za kitaaluma zinazotakiwa kujiunga na taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hiyo kunahitajika mbinu mbadala ya kugharamia elimu ya juu, hivyo basi utaratibu wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ni njia muafaka itakayosaidia jitihada za wananchi na za Serikali kuichangia elimu ya juu. Utaratibu wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu unampa kila mwanafunzi mwenye sifa, fursa sawa ya kupata nafasi ya kusoma, unawasaidia wanafunzi vile vile wenye uwezo mdogo kiuchumi, siyo tu kupata nafasi ya kusoma bali pia kusoma masomo wanayotaka au ndoto zao yaani masomo yatakayowawezesha kupata stadi zitakazowaingiza katika zama za utandawazi wakiwa na nguvu za ushindani sawa na mshiriki mwingine yeyote katika harakati za kuleta maendeleo binafsi ya jamii na ya taifa kwa ujumla. Hii ni njia inayotoa fursa kwa taasisi binafsi za elimu ya juu ambazo zimeendelea kuanzishwa kama sera ya elimu ya juu inavyoelekezwa kutumia vema miundo mbinu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa Mataifa mengine unaonyesha kwamba utaratibu wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kama unaendeshwa kwa sheria taratibu na kanuni sahihi, una mafanikio makubwa. Mifano ya utaratibu kama huo katika nchi mbili za Kiafrika inaweza kutusaidia kuliona hilo.

Katika kipindi cha miaka kumi kati ya mwaka 1988/1989 na mwaka 1999/2000 kwa kutumia utaratibu huo wa mikopo kwa wanafunzi, Nchi ya Ghana ilifanikiwa kuongeza idadi ya taasisi za elimu ya juu zilizonufaika na utaratibu huo kutoka 11 hadi kufikia 23. Idadi ya wanafunzi waliopata fursa ya kujiunga na taasisi za elimu ya juu katika nchi hiyo na kwa kutumia utaratibu huo wa mikopo kati ya mwaka 1988/1989 na mwaka 2000/2001 katika Nchi ya Ghana ulipanda kutoka 8,138 hadi 81,401. Katika nchi jirani ya Kenya ambako utaratibu kama huu ulianzishwa tangu mwaka 1995

wanafunzi 50,000 sasa wasio na uwezo kiuchumi hutengewa shilingi bilioni 1 ya shilingi za Kenya kila kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na marejesho ya mikopo hiyo huko Kenya ni shilingi milioni 600 kwa mwaka. Kwa hiyo, kuna mafanikio asilimia 60 ya kurudisha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi na kabla sijawasilisha Muswada huu, kipengele kwa kipengele napenda sasa uniruhusu ninukuu Sera ya Elimu ya Juu, Tolea lake la mwaka 1999 ukurasa wa 19 ambapo inasema: "Kwa kutambua hali duni kiuchumi cha wanafunzi na wazazi, Serikali itatoa msaada wa fedha kwa wanafunzi kwa kuanzisha utaratibu wa mikopo." Kwa hiyo, Muswada huu unaofikishwa mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii ni utekelezaji wa maelekezo wa sera hii.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki na Kamati yake pamoja na wadau mbalimbali kwa maoni na ushauri wao uliotuwezesha kuboresha Muswada huu. Tumefaidika sana na utaratibu wa kusikilizwa na kutoa maoni hadharani *(public hearing)* wa Miswada. Wanafunzi na viongozi wa taasisi zetu za elimu ya juu wamepata fursa ya kutoa maoni yao juu ya Muswada huu mbele ya Kamati pamoja na kwamba walikwishashiriki kikamilifu katika warsha ya wadau kuhusu Muswada huu huko Morogoro mapema mwaka 2003. Matokeo ya juhudi hizi za pamoja ni waraka wa marekebisho wa Muswada huu ambao ninawasilisha pamoja na Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulio mbele yako unadhamiria kutunga sheria itakayoanzisha chombo kitakachohusika na utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa marejesho ya mikopo hiyo kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu. Sheria hiyo itakuwa na sehemu sita.

Sehemu ya kwanza, inayoundwa na ibara ya kwanza, ya pili na ya tatu, inaainisha jina na sheria inayokusudiwa kutungwa tarehe ya kwanza kwa sheria hiyo na eneo la mamlaka ya sheria hiyo. Hali kadhalika sehemu hii inatoa tanibihi ya istilahi zitakazotumika katika sheria hiyo.

Sehemu ya pili, yaani ibara ya 4, 5 na ya 6 inahusu kuanzishwa kwa chombo kitakachoitwa bodi ya mikopo ya wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu *(Higher Education Students Loans Board).* Bodi hii itakuwa na wajumbe wasiopungua 8 na wasiozidi 12. Wajumbe wote wa Bodi watateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya elimu ya juu.

Majukumu ya Bodi yatakuwa ni kuandaa taratibu za kuwatambua wanafunzi wanaostahili kupata mikopo kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu. Pili kufuatilia na kusimamia utoaji wa malipo na marejesho ya mikopo, tatu kuhakikisha kwamba Bodi inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Sehemu ya tatu ya Muswada huu yenye ibara ya 7 mpaka ya 15 inaainisha Mamlaka ya Bodi ambayo ni pamoja na kuchambua na kuweka vigezo na masharti ya utoaji wa mikopo, kupokea na kutafakari maombi yote ya mikopo kwa ajili ya masomo

ya elimu ya juu, kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaostahili, kuamua idadi ya wanafunzi watakaopewa mikopo, kukusanya na kutunza katika benki fedha zote wanazodaiwa wanafunzi wote waliopata mikopo tangu Julai, 1994.

Ibara za 16 hadi 24 ambazo zinaunda sehemu ya nne ya sheria inayopendekezwa zinahusu dhima na wajibu wa wadau mbalimbali watakaohusika na sheria hii. Bodi itawajibika kuhakikisha kwamba mikopo inayotolewa ni kwa ajili ya chakula na malazi, vitabu na viandikwa, mafunzo kwa vitendo, ada, utafiti na mahitaji maalum ya vitivo.

Sehemu hii pia inabainisha masharti ya kupata mikopo, mwombaji lazima awe raia wa Tanzania yaani Mtanzania amepata usaili katika Chuo cha Elimu ya Juu kinachotambulika kisheria *(Accredited Institution).* Mwanafunzi anayeendelea na masomo baada ya kufaulu vema masomo yaliyopita, ameomba mkopo kwa maandishi kwa kutumia fomu maalum, hana chanzo kingine cha fedha kwa masomo hayo ambayo anaomba, ana mdhamini au wadhamini na ana dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusisitiza umuhimu wa kipengele cha dhamana kwa wakopaji kuwa ni utaratibu wa kawaida katika utoaji mikopo mbalimbali. Suala la msingi ni kuwepo aina mbalimbali za dhamana ambazo hata wananchi wa kawaida wanaweza kumudu. Baadhi ya dhamana hizo ukiacha hizo hati, ardhi, shamba, hati ya nyumba, hati ya bima, akaunti ya benki vile vile hati ya utambulisho kutoka kwenye kijiji, kutoka kwenye Wilaya nazo hizo ni dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi husika itaainisha aina mbalimbali za dhamana ili kutoa fursa sawa kwa wote kufikiriwa kwa mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sehemu hii atakayenufaika na mkopo atawajibika kulipa fedha zote alizokopeshwa bila riba isipokuwa pale ambapo ametozwa faini itakanayo kama ni adhabu kwa ukiukaji wa sheria hii. Itakuwa pia ni wajibu wa mnufaika wa mkopo kuandaa taratibu za makato ya marejesho ya mkopo aliouchukua kwa kushirikiana na mwajiri wake au Bodi. Atawajibika pia kuijulisha Bodi mabadiliko yote ya anwani au ajira yake. Ni wajibu wa mwajiri wake naye kwa upande wake kuijulisha bodi juu ya mnufaika na mkopo ambaye amemwajiri nafasi yake katika ajira, mabadiliko ya anwani, au jina la mshahara wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inatambua kwamba ajira za sasa hazitokani na ajira za Serikali peke yake au ajira kwenye *Private Sector Reform* lakini vile vile kwenye *informal sector.* Hali hiyo vile vile tumeizingatia katika sheria. Sehemu hii pia inaainisha adhabu kwa wale ambao hawatatimiza wajibu wao wa kisheria kuhusiana na taratibu na masharti ya mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mdhamini wa mkopaji ambaye hatatimiza wajibu wake atakuwa amefanya kosa na anastahili kufunguliwa mashtaka siyo ya jinai, mashtaka ya madai. Mwajiri ambaye ameshindwa kutekeleza maelekezo ya kifungu cha 20 cha sheria kinachopendekeza atakuwa amefanya kosa na atastahili adhabu ya faini kisichopungua shilingi milioni moja. Kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha sheria hii kutoa taarifa za uongo ni kosa linalostahili adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano ya sheria, inayopendekezwa yaani ibara ya 25 hadi 28 inahusu vyanzo vya fedha vya bodi vinavyokusudiwa kuundwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi, vyanzo hivyo vya fedha ni pamoja na ruzuku kutoka Serikalini, zawadi, ada na malipo mbalimbali na mapato mbalimbali ya mfuko huu kwa kutoa huduma zitakazotolewa na bodi. Sehemu hii pia inaweka bayana taratibu zitakazotumika katika kutayarisha makisio ya mapato na matumizi ya Bodi, maandalizi na matumizi ya vitabu vya hesabu na ukaguzi wa vitabu hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita na ya mwisho ya Muswada huu ambayo inaanzia ibara ya 29 hadi 33 inatoa mapendekezo juu ya mambo mbalimbali yanayohusu Bodi. Mambo hayo ni pamoja na mamlaka ya Bodi na ya yeye waziri anayehusika na chombo hiki kutoa misamaha juu ya masuala mbalimbali chini ya sheria hii, maslahi ya wajumbe wa Bodi, kinga kwa watendaji wa Bodi chini ya sheria hii kutokana na utekelezaji wa majukumu yao na mamlaka ya Waziri, kutengeneza kanuni za utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni ya Kamati na mimi naomba niungane na wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioukwaa Urais. Naomba kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Getrude Mongella, ambaye amekuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika na wa pili vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani, wote nawatakia kila la kheri katika majukumu yao.

Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, nilishampongeza wakati alipochaguliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu wa Afrika, lakini vizuri niendeleze hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii mliyoipa kazi ya kufikiria Muswada wa Sheria ya kuanzisha taasisi na bodi ya kushughulikia mikopo ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ilikutana tarehe 5 hadi 6 Aprili, 2004 Dar es Salaam na kupata muda wa kutosha kufikiria Muswada huo na ilitumia kanuni ya 88 (6) kupata maoni ya wadau mbalimbali wa Muswada kutoka baadhi ya Taasisi na Vyuo vya Elimu ya Juu kama ifuatavyo:-

Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Tiba Muhimbili, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Biashara pamoja na wadau wengine waliotoka

kwenye Taasisi za Fedha kama *CRDB*. Maoni yao yalitolewa na uongozi wa vyuo pamoja na uongozi wa Serikali za Wanafunzi.

Nawashukuru sana wadau wote waliofika mbele ya Kamati kwa jinsi walivyotoa maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali na Kamati wakati wa kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo naomba niseme kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa bahati mbaya maoni yao hayakuwasilishwa rasmi mbele ya Kamati, lakini hata hivyo Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wameleta maoni yao baada ya Kamati kumaliza kazi yake.

Lakini pamoja na hayo baada ya kuwasiliana nao sehemu ya maoni yao yamezingatiwa kwenye maoni ya Kamati. Lakini hata hivyo tunawashauri vile vile Wabunge ambao ni wawakilishi kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka Bunge hili, basi wapate nafasi ya kuwakilisha vile vile maoni ya eneo hilo na vile vile nina hakika Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni sehemu ya jamii, basi Waheshimiwa Wabunge katika michango yenu mnaweza vile vile mkajaza pengo ambalo limetokea kwa wao kutokuwasilisha taarifa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua, ilihoji na kujadili Muswada wa Sheria iliyotajwa hapo juu na kupitia kila kifungu cha Muswada na kupata maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Naibu wake na wataalam mbalimbali, Kamati iliridhika na kuunga mkono hoja na kupendekeza hoja hii iletwe mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili na hatua zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati, pamoja na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo yafuatayo kwa lengo la kuboresha na kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Juu ambaye inalenga kuwa na mbinu mbadala ya kugharamia Elimu ya Juu kwa utaratibu wa mikopo ikiwa ni njia ya pamoja kati ya Serikali na wananchi kuchangia Elimu ya Juu.

Kamati inaunga mkono Serikali kwa kuanzisha sheria inayoweka utaratibu unaotoa fursa sawa kwa kila mwanafunzi mwenye sifa kupata nafasi ya kusoma na kuwasaidia wazazi wa wanafunzi wenye uwezo mdogo kiuchumi ili watoto wao wenye sifa waweze kupata masomo yatakayowawezesha kupata stadi zitakazowaingiza kwenye zama za utandawazi wakiwa na nguvu za ushindani sawa na mshiriki mwingine yeyote katika harakati za kuleta maendeleo binafsi ya jamii na ya taifa kwa ujumla. Aidha, njia hii inatoa fursa kwa Taasisi binafsi za Elimu ya Juu ambazo zinaendelea kuanzishwa kama sera ya elimu ya juu inavyoelekeza katika kutumia vema miundombinu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua madhubuti ya kuanzishwa utaratibu mpya ya kugharamia Elimu ya Juu kwa kuanzisha mfuko wa kugharamia elimu hiyo na bodi itakayosimamia kutoa na kurejesha mikopo ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kwa utaratibu mpya wa kisheria. Ni matazamio ya Kamati

kuwa utaratibu huu utafanikisha azma ya Serikali kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vyote vya Elimu ya Juu vya Umma na vile vya Binafsi na kuongeza watalaalam nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza, jina la sheria, Kamati inapendekeza kuwa badala ya sheria kujulikana kama *Government Students Loans Board,* jina hili linaleta dhana ya kuwa chombo kinachoundwa na sheria hii ni kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi waliopo katika Vyuo vya Umma pekee. Hivyo Kamati inapendekeza sheria ijulikane kwa jina la *The Higher Education Students Loans Board* kwa msingi kuwa mikopo itakuwa wazi kwa wanafunzi waliopo kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma na vile vya binafsi na pendekezo hili pia linazingatia maoni ya wadau. Tunashukuru kwamba Serikali imekubali pendekezo hili. *(Makofi)*

Sehemu ya pili, Wajumbe wa Bodi, ibara ya 5(1) Kamati inapendekeza kuwa katika idadi ya Wajumbe wa Bodi ya mfuko unaoanzishwa na sheria hii pia wawepo wawakilishi kutoka chombo kinachounganisha Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma na vya Binafsi ambao ndiyo walengwa hasa wa mfuko huu. Pia kuwe na wawakilishi wa Vyuo vya Umma na vya Binafsi na mwakilishi kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye schedule of amendments nina hakika kwamba Waheshimiwa Wabunge mtakaposoma pamoja na maoni haya mtaona kwamba mambo mengi yamekwisharekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za bodi utoaji wa mikopo ibara ya 6. Kamati ilitafakari suala hili na kushauri kuwa ni vema Serikali ikatoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu ambao ni raia wa Tanzania tu. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amelisema hilo, aidha, Kamati inashauri kuwa kwa kuwa nchi yetu imekuwa na mwingiliano na watu kutoka Mataifa mbalimbali wakiwemo wakimbizi kutoka nchi jirani zenye matatizo mbalimbali ya kisiasa suala la Serikali kutoa vitambulisho vya uraia *(National Identity Cards)* kwa raia wake lianze kutekelezwa kwa haraka kwa minajili ya kuhakikisha kuwa mikopo itakayotolewa itatolewa kwa walengwa ambao ni raia wa Tanzania tu na pia kurahisisha ufuatiliaji wa urejeshaji wa mikopo hiyo. *(Makofi)*

Sehemu ya tatu, ibara ya 7 urejeshaji wa mikopo. Kamati ilitafakari mapendekezo ya Serikali kuhusu kurejesha mikopo na kuona kuwa masharti yanayowekwa na sheria hii ya kukusanya mikopo iliyotolewa tangu mwaka 1994, hakuna mantiki kwani utawala bora ni pamoja na kuzingatia kanuni na mikataba ya wakati husika. Hivyo Kamati inapendekeza kuwa katika kukusanya mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi tangu mwaka 1994, Serikali izingatie mikataba iliyoingia kati yake na wanafunzi wakati ule ilipotoa mikopo hiyo. Sheria hii itumike kwa wale tu watakaochukua mikopo baada ya sheria hiyo kuanza kutumika kwa misingi ya kulinda haki, maadili na misingi ya uwajibikaji. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali kuondoa kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 4 *eligibility and liability.* Kamati inapendekeza kuwa kiwango cha juu cha umri, *age limit* kilichopendekezwa kwa kupata mikopo kiondolewe kwani ni kinyume na matakwa ya ibara ya 11(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la mwaka 1977 inayompa kila raia haki ya kujielimisha na kuwa huru kutafuta elimu katika fani anayoipenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na staili na uwezo wake. Hivyo kifungu hicho kinaonekana kubagua baadhi ya wanafunzi wanaoamua kujiendeleza wakiwa na umri mkubwa zaidi ya kiwango cha miaka 60 kinachotajwa na Muswada. Mfano halisi ni baadhi ya wanafunzi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambao huchukua masomo ya shahada ya kwanza wakiwa wamepita umri uliotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 16 ambayo Mheshimiwa Waziri ameifafanua inaonekana kwamba wadau wengi hasa wanafunzi wanahitaji ufafanuzi zaidi wa mahitaji ya wanafunzi kukopa kwa mfano ada, malazi, chakula, mazoezi, vitabu na kadhalika katika hali halisi ya kifedha wangependa kujua katika hali halisi ya kifedha kifungu hiki kinakuwa na *impl6ication* ya namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 18 vifung vya 1 na 2 masharti na dhamana ya mkopo. Kamati inatoa maoni kuwa masharti ya dhamana ya mkopo yanayopendekeza katika ibara ya 18 ya Muswada ya kutafuta wadhamini ambao watawajibika iwapo mkopaji atashindwa kutimiza masharti ya dhamani na hivyo mikopo kutolewa kwa watoto na watu wenye uwezo tu. Hivyo Kamati inapendekeza kuwa Serikali iweke masharti nafuu ikiwa ni pamoja na udhamini wa Serikali katika ngazi za kata, kijiji, masharika ya dini, vyama vya hiari, mali, ardhi hata kujidhamini mwenyewe pale itakaposhindikana, vinginevyo kuwawezesha watoto wasio na uwezo kutumia fursa hii sawa na wenye uwezo kupata Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati inapendekeza kuwa masharti ya mikopo yazingatie muda wote ambao mwanafunzi atakuwa chuoni, ikiwa ni pamoja na muda wa ziada kwa wanaolazimika kurudia masomo na mitihani yao. Wale ambao wanafanya *supplementary* na *repeating students* wote kwa kuzingatia taratibu za Vyuo vya Elimu ya Juu.

Aidha, Kamati inapendekeza kuwa Sheria hii iruhusu mikopo kutolewa kwa wanafunzi wanaochukua Shahada za Uzamili na Falsafa. Kamati inapendekeza kuwa mikopo itolewe pia kwa wanaosoma nje ya nchi ili mradi masharti ya udhamini wa mikopo na urejeshaji wake unazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane, ushauri wetu kwenye Ibara ya 18 mpaka 21 na 23 ni kuwa Kamati imepitia vifungu vya adhabu zitakazotolewa kwa wale watakaoshindwa kurejesha mikopo ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua kali waajiri ambao hawatarejesha mikopo ya watumishi wao kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Kamati inashauri kuwa kabla sheria hii haijaanza kutumika ni vema Serikali ikafanya kazi ya kutoa elimu kwa wadau wote juu ya sheria yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wa Huduma za Jamii kwa umakini wao katika kufikiria na kuchambua Muswada wa Sheria hii na kuweza kutoa maoni haya.

Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Naibu wake, Katibu Mkuu na watalaam wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Muswada huu na kukubali kufanya marekebisho muhimu kama tulivyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniruhusu nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa *The Government Students' Loans Board Act, 2004.* Lakini niwashukuru wale waliochaguliwa kuwa Marais wasije wakasema Kambi ya Upinzani haitaki kuwapongeza. Kwa hiyo na sisi tunaungana na wao katika kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, sauti yangu inakwama kwa sababu ratiba ilivyopangwa nimedhulumiwa sikuweza kwenda kula Pasaka na familia yangu na wapiga kura. Kwa hiyo, tunadhani Pasaka kwa sababu inakuwa inaeleweka siku nyingine tuwe tunaachiwa tujumuike na wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati wa Huduma za Jamii ambaye niliujadili na kuuchambua na kupendekeza marekebisho katika Muswada huu kwa kushirikiana na wadau wengine kama Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alivyosema. Lakini vile vile wenzangu wa Kamati ya Upinzani walikuwa nayo maneno mengine na awali ya yote napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Naibu Waziri, Katibu wa Wizara pamoja na watalaam wa Wizara kwa kufanya baadhi ya marekebisho ambayo tuliyapendekeza wakati tulipokutana kwenye Kamati, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu sehemu ya kwanza, mambo ya utangulizi tunakubaliana na Serikali kufuta neno *Government* na kufanya Muswada usomeke *The Government, I mean, The High Education Students' Loan Board.* Hii ni kwa sababu ya kutaka kuondoa dhana kuwa chombo hiki kilianzishwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi walio katika vyuo vya elimu ya juu ambavyo vinamilikiwa na Serikali na hapa tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha chombo ambacho hakitabagua wanafunzi walioko kwenye vyuo vya elimu ya juu vya binafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya kwanza kifungu cha 3 kuhusu tafsiri ya maneno au *interpretation,* Kambi ya Upinzani inapendekeza tafsiri ya neno *student* lisomeke *student means any person admitted to a higher education institution as a candidate to advanced diploma, first degree, master's degree and doctor's of philosophy degree*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa mapendekezo hayo ili iwe wazi kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa kupata uwiano wa wataalam na wasomi wa viwango tofauti katika nchi yetu tunazingatia kwamba kuanzishwa kwa elimu ya msingi kunapelekea kuimarishwa elimu ya sekondari za kati na kuimarishwa kwa elimu za sekondari za kati kunapelekea kuimarishwa kwa elimu ya elimu ya sekondari za juu. Tatu, kuimarishwa kwa elimu ya sekondari ya juu kutapelekea kuimarishwa kwa elimu ya vyuo vya juu na vyuo vikuu.

Basi kwa msingi huo kunahitaji kuwepo kwa uwiano wa wataalam. Mfano kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu kutahitaji ongezeko la walimu na watalaam wenye shahada za Uzamili na Udaktari wa Falsafa. Kwa hiyo ndiyo maana tunapendekeza mkopo huu uwafikie wanaosomea pia Shahada za Uzamili pamoja na shahada za Udaktari wa Falsafa. Hii ni kwa sababu Serikali imekuwa haiwadhamini wanafunzi wa shahada ya uzamili pamoja na ile ya udaktari wa falsafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya pili, kifungu cha 5(1), Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu hicho kisomeke: *"The board established under section 4 shall consists of not less than twelve and not more than fourteen members as follows."*

Mheshimiwa Waziri yeye alikuwa anapendekeza kati ya nane na kumi na mbili na hii ni kwa sababu kwa kuangalia mapendekezo ambayo tuliyatoa ili kuweza kupata wawakilishi kutoka Zanzibar pamoja na Muungano wa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu vya Serikali pamoja na za binafsi.

Kambi ya Upinzani inaona kuna utata na mushkeri katika sehemu ya kifungu sehemu ya tatu kifungu kidogo cha (j) kinachopendekeza kwamba Bodi hii iwape madaraka ya kukusanya fedha za mkopo zilizokopwa na wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu kuanzia Julai, 1994.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea nitangaze maslahi kwamba mimi ni miongoni mwa waliochukua mkopo huo kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, maoni haya yasifanye kana kwamba napinga nisilipe. Kama tutapitisha niko tayari kulipa ama nikiwa Bungeni ama kwangu shambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hiyo, Kambi ya Upinzani haikubaliani moja kwa moja na pendekezo hili kwa sababu, moja, wanafunzi waliochukua mkopo walilazimika kukopa bila ya hiyari yao na mikopo hiyo ilichukuliwa katika hali ya migomo na vurugu kwa wanavyuo hao.

Pili, wanafunzi hao waliambiwa kuwa Serikali ilitaka ionekane inatoa mikopo kwa wanafunzi ili kukidhi masharti ya Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* pamoja na nchi wafadhili.

Tatu, si kawaida kwa mantiki ya kisheria kutunga sheria inayorudi nyuma *(retrospective)* kushughulikia mambo yaliyotokea au kufanyika kabla ya sheria haijatungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo kwa lengo na madhumuni ya kuanzisha Taasisi hii ili kusaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na sisi watunga sheria pengine waliochukua mikopo kuanzia Julai, 1994 na wao walipe. Basi Kambi ya Upinzani inapendekeza tusirudi nyuma mpaka mwaka 1994 bali turudi nyuma mpaka mwaka 1965 ili wale wote ambao walisoma bure kwa fedha za walipa kodi wa Tanzania chini ya sera hii ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya elimu kuwa bure wote na wao walipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wengi wataguna, lakini hiyo ndiyo itakuwa haki kwa wote. Ni ukweli ulio wazi kuwa wale wote waliosoma wakati wa Awamu ya Kwanza na kipindi cha pili cha Serikali ya Tanzania walisoma bure. Kwani hawakulipa karo ya shule za Sekondari. Hawakujigharamia gharama za usafiri wakiwa vyuoni ndani na nje ya nchi hawakugharamia chochote na badala yake walikuwa wanapewa hata posho ya kujikimu. Kwa hiyo, tunapopendekeza kwamba ili tuweze kukusanya fedha nyingi tusiwaonee wale waliochukua hela mwaka 1994 tu tunawataka na wale wote waliosoma bure waweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na kwamba fedha zilizowafikisha hapo zilikuwa zinatokana na kukata ushuru na kodi kwa mazao ya wakulima, wafugaji, wavuvi ambao leo hii ndiyo hao hao ambao watoto wao wachangie elimu ya juu kwa kukopa ili waje walipe. Tunaona ili jamii ya Watanzania, iweze kutuelewa kwamba sisi Wabunge na watumishi wa vyuo vya juu Serikalini tumedhamiria kutenda haki, basi inapendekezwa kiongezwe kipengele cha kutaka tuchangie kisheria katika mfuko wa Bodi ya Mikopo tunayoianzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza katika sehemu ya nne kifungu kidogo cha kwanza, badala ya kipengele (e) kuongezwe kipengele (f) kisomeke na ile inayoonyesha kwamba ni kwa vipengele vipi na kwa mahitaji yepi, kama ni chakula, *tuition fees* basi kiongezwe kipengele (f) ambacho kitaonyesha *travelling costs for students studying abroad.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa nani analipia malipo ya ziada kwa wanafunzi wanaosoma nchi za nje ambao hawalipiwi na Mataifa haya ya nje ambako wanasomea. Kwani gharama za kuwasomesha huko ni karibu mara tatu kwa mwanafunzi anayesoma nje, kuliko yule anayesoma hapa ndani na hii tunajaribu kuiangalia kuwa itakapokuja kwenye makato ama mtakata hela nyingi kwenye mshahara wake au mtamkata kwa murefu na italeta utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza katika kifungu cha 17 (d) kinachosomeka: *"Is a person who has no financial assistance from any other sources to cover the item of cost for which the application is made."*

Tunapendekeza hivyo, kwa sabu Mheshimiwa Naibu Spika, moja, familia moja inayoonekana ina uwezo inaweza kuwa na wanafunzi wengi wanaosoma katika ngazi

tofauti za shule au vyuo hivyo kuhitaji mikopo au msaada wa ziada. Pili, wakati mwingine kuna wazazi ambao pengine labda ana ng'ombe 500 lakini hataki binti yake aende Chuo Kikuu kwa hiyo, angapenda binti yake huyo aolewe ili aweze kuongeza ng'ombe, sasa akiambiwa atoe dhamana anaweza kukataa halafu yule naye atakosa mkopo huo.

Tatu, hata hivyo hizo fedha za mfuko ni kodi inayotokana na watu ambao pengine wana uwezo wanaolipa kodi ya mapato kama ninyi mnajua mnakatwa shilingi ngapi kwenye mishahara yenu, kwa hiyo, tungependekeza mfuko uwe kwa wote. Aidha, tunapendekeza kifungu kinachoitaka Bodi kutowasaidia wanafunzi wanaorudia masomo au mwaka kifutwe. Hii ni kwa sababu mwanafunzi anayerudia masomo mawili kati ya 10 hana dhambi kwani hiyo ndiyo hali ilivyo katika vyuo vya elimu ya juu. Vile vile yule anayerudia mwaka lazima asaidiwe kwani ziko sababu mbalimbali kama za kiafya, kijamii inaweza kumfanya arudie mwaka na tukizingatia utaratibu wa *semister* ambao umeanzishwa kwamba mtu anaweza akaamua kuacha ile *semister* moja halafu akaja kuirudia baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 18 (1), inamtaka mwombaji mkopo atakiwe kuleta dhamana. Yapo maneno kwamba Bodi ita-*demand security.* Ibara hii ifutwe kwani haina maana kwa sababu moja, anayekwenda kukopa anatafuta elimu ambayo tunadhani ndiyo biashara yake na kama akiwa hai tunategemea ataajiriwa au atajiajiri mwenyewe na atalipa mkopo kwa masharti ya sheria hii.

Pili, kwa vile muda wa kusoma, kumaliza na kuajiriwa na kurejesha mkopo ni zaidi ya kumi na mitano, mali hiyo iliyowekwa dhamana haitasaidia katika maendeleo ya familia kwani itakuwa chini ya Bodi ya Mkopo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika na kwa kuzingatia kwamba pengine hamtakubaliana na mawazo yetu mtakubali kwamba wale ambao hawana uwezo ndio walipe, katika nchi yetu uwezo wao ni mashamba ya mahindi wakati wa msimu. Sasa sijui yana thamani kiasi gani ili kugharamia hela hizo ambazo zinahitajika ndiyo maana tunasema apewe mkopo asome, halafu afuatiliwe atakapokuwa hawezi kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukubaliana na ibara ya 18(6), (7) Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali iangalie upya suala la Watanzania waliosoma bure au kwa mkopo na kodi za wananchi halafu akaenda kufanya kazi nchi za nje. Tunapendekeza hivyo kwa sababu, moja, Watanzania hawanufaiki vilivyo na huduma za raia hawa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi. Pili, hata kodi wanazolipa wanaofaidi ni hao watu wa nchi za nje mahala ambako wanafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uko ushahidi kuwa katika nchi za Amerika ya Kusini mapato ya Taifa, nazungumzia mapato ya Mataifa hayo yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na malipo ya raia wanaofanya kazi nje ya nchi. Kwa sababu kuna utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanachangia katika Pato la Taifa.

Kambi ya Upinzani kwa kuzingatia umuhimu wa Tanzania kuzalisha wasomi wengi na kuongeza idadi ya vyuo vya elimu ya juu na wanafunzi wake ili angalau katika kipindi cha miaka 10 ijayo tuweze kuzipita Kenya, Uganda na ikibidi nchi zote za Afrika. Ni vyema ikaanzishwa kodi maalum kwa ajili ya mfuko wa elimu ya juu kama ilivyo kodi ya *VAT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi hii isiwaguse wakulima wadogo na wananchi wa kawaida wasiokuwa na vipato vya kutosha. Iwahusu Mashirika, makampani makubwa na wafanya biashara wakubwa ambao kila kunakokucha wananeemeka na kuonyesha kwamba kuna tofauti kati ya wao na walala hoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni hayo na mapendekezo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuunga mkono Muswada huu kwa matarajio kwamba mabadiliko yatafanyika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Walioomba kuchangia jumla wako tisa na nadhani wote watapata nafasi, kwa sababu kwa maana hiyo, Waziri anaweza aka-*wind up* siku ya Jumatatu. Kwa hiyo, tunayo nafasi, kwa kila mmoja anaweza kuchangia, wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Leonard Derefa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, hao ni wanne wa kwanza.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kwanza napenda niseme naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Kama sote tunavyofahamu wakati tunajitawala tulibaini maadui watatu kwa maendeleo yetu. Mwenyekiti wa maadui hao ni ujinga, anafuatiwa na umaskini na anafuatiwa na maradhi. Hoja iliyo mbele yetu ni hoja nzuri sana ya kujaribu kutibu matatizo haya hasa matatizo makubwa ya ujinga na napenda kweli nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuleta hoja hii kwa sasa. Lakini kama mnavyofahamu elimu ni haki ya msingi ya kila mwananchi.

Mimi bahati nzuri nilibahatika kutembelea nchi ya Ghana na bahati nzuri tukatembelea Wizara mbalimbali na bahati nzuri tukaenda Wizara ya Fedha na katika Wizara ya Fedha kule Ghana Bajeti yao haina *deficit* mara nyingi kuna hela zinabaki na hela hizo zinapobaki nyingi zinapelekwa Wizara ya Elimu na wanao-*operate* elimu ni watu binafsi, Serikali, ziweze kusaidia katika kusomesha.

Kitu kingine tulichojifunza wakati tumekwenda Ghana ni kwamba Serikali ya Ghana inachanga asilimia mbili na nusu zinachangwa na *Revenue Authority of Ghana,* zinapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko wa elimu. Kule Ghana tatizo kama mtu anataka kusoma tatizo lisiwe fedha na mfuko una hela nyingi sana na kwa bahati nzuri Tanzania vile vile tuliishauri Serikali na kwa bahati nzuri wameunda mamlaka ya elimu katika nchi hii na kwa bahati nzuri sisi tumeshauri kwamba Serikali mapato ya ndani yalipwe asiliamia mbili yaende moja kwa moja kwenye ule mfuko.

Bahati nzuri juzi tulikuwa na mkutano kule Shinyanga wa Mamlaka ya Elimu. Tumeuliza kwamba Serikali mpaka sasa hivi inachangia kiasi gani? Mhusika alituambia kwamba wanachangia, *already* sisi kwenye Sheria tuliruhusu kwamba zichangwe asilimia mbili. Lakini kwa bahati mbaya kwa sasa hivi Serikali inatoa asilimia 0.005 hawajafikia hata moja. Ninaamini kabisa kama Serikali wangeweza wakalipa ile asilimia mbili ya ule mfuko wa elimu, tungeweza kuwa na bilioni ukitazama mapato ya ndani sasa hivi inawezekana karibu trilioni 1.6. Kwa hiyo, tungeweza kuwa na *32 billion* ambazo zingeweza kwenda kwenye mfuko ule.

Kwa kuwa elimu *actually* elimu ni mwanga, mtu ambaye hajaenda shule yuko gizani na mimi nilikuwa nasema kwamba sheria hii ni nzuri kwa kuanza nayo lakini nilikuwa napenda niishauri Serikali kama inawezekana watu wetu wasome, mfuko huu tuuboreshe zaidi na ikiwezekana watu waweze kusoma bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mtu akisoma hata kama hajailipa Serikali lakini ili aweze kupata ile *benefit* ya mtu aliyesoma huwezi ukaipata moja kwa moja, mara nyingine utaipata *indirectly* kwa mtu aliyesoma na Watanzania wetu kama wanakuwa na elimu ya kutosha utakuta kwamba lazima mambo mengi ambayo mengi tunakwama katika kuyaboresha ungelikuta *automatically* yangelikuwa yanaondoka.

Naamini kabisa kwamba huko nyuma nilisema kwamba tunao watu wetu ambao wanasoma hapa na kwa bahati mbaya wanapomaliza Serikali haina uwezo wa kuwapa kazi. Bahati nzuri mimi niko kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali *(Public Accounts Committee - PAC).*

Ukitazama huko Serikali *already* imekopesha watu zaidi ya bilioni 27 nafikiri mpaka kuishia mwaka 2002. Gharama ya kuzikusanya zile hela ni kubwa zaidi afadhali zile hela kama inawezekana wamezi-*right off,* kwa sababu watu tuliowasomesha ile *benefit* watakayoipata hapa hatuwezi kuipata *directly* tutaipata *indirecty.*

Mtu akisoma anatoka kwenye giza na mtu akitoka kwenye giza anakuwa kwenye mwanga na hilo linasaidia. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nasema kwamba sheria hii ni nzuri kwa kuanzia lakini tunakokwenda watu wetu lazima tuwape nafasi ya kusoma bure na tunalo tatizo sasa hivi kwa mfano tukijiuliza maswali huyu mtu unayemsomesha sasa hivi ni kwenye digrii kwa mfano digrii ya kwanza ile gharama yake lazima tungekuwa tunaambiwa atatakiwa awe na fedha kiasi gani na lile deni litakuwa ni kiasi gani mpaka apate Digrii ya Kwanza. Lakini kwa kuwa Serikali hatuna uwezo wa kuajiri hawa tunaowasomesha, *how do we get the money?* Tutazipata vipi?

Tungekuwa na uwezo kwa mfano, labda upande wa Walimu napenda labda nitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa kweli kwamba yeye sasa hivi walimu wanakwenda moja kwa moja wale ndiyo ungewakopesha. Kwa kweli hapo ingewezekana sasa hawa wengi hata zile hela ambazo tumekopeshwa huko hazijulikani na watu wala hatuwajui wako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata pamoja na kuanzisha hii Bodi kutakuwa na tatizo moja kubwa ile gharama ya kuwa-*trace* ile *tracing* itakuwa kubwa zaidi kuliko afadhali mtu asome, halafu aende anakotoka lakini kama tumemsomesha mtu mzuri, *he will always remember* atamkumbuka baba yake, atamjengea nyumba, atakumbuka familia yake atawajengea nyumba na mimi niliwahi kuleta hapa hoja moja na bahati nzuri ikatekelezwa kwamba wale watu ambao tunawasomesha na kwa bahati mbaya hatuwezi kuwaajiri lazima tuwe na mahala pa kuwatafutia kazi ili wakipata kazi hata huko nje wataongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba kwa mfano, ukienda katika nchi za Asia utakuta watumishi wengi wanaofanya kazi katika nchi za Uarabuni wanatoka Asia na yale mapato yao ya ile *salary* ya *emoluments* ambazo wanapata pale wakati mwingine ni hela nyingi sana kuzidi hata kuuza pamba na ninashukuru kwamba Serikali, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo walianzisha hiki kitengo karibu na *NSSF,* naamini kabisa kwamba itafika siku moja watatupa taarifa kitengo hicho sasa hivi kimefikia kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri kwamba pamoja na kwamba hatujawa na uwezo wa kuwa na hela za kutosha, nilikuwa nashauri kwamba kama inawezekana sasa hivi tujitahidi kabisa kwamba mfano Kenya, kijana anayemaliza *Form Six* na anayeweza kupata, anapata *the highest grade* za kwenye mitihani kuanzia *point* nane, *point* mpaka kumi ama mpaka 20, yule mmoja *automatically* moja kwa moja anakwenda *University* na anagharamiwa na Serikali. Kwa sababu tusipofanya namna hiyo, tunao vijana wenye akili lakini baba zao hawana uwezo wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kwamba tuweke utaratibu kwamba wale walioko kwenye *Form Six* anaye-*attain the highest grade* yule aende moja kwa moja na Serikali igharamie, kwa sababu kama tutasema sijui mtu aweke dhamana pale kwenye *Part Four,* nimesoma *Part Four* yale masharti yaliyowekwa pale ni masharti kwa kweli, lazima tuseme ule ukweli hayo masharti yaliyowekwa pale kwa watu wetu tunavyowafahamu ni wachache sana wanaoweza kuyamudu.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwamba Mheshimiwa Waziri ameleta hapa hoja nzuri sana na inataka itusaidie tuwe na watu waliosoma. Mimi napenda vile vile nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Mkapa, kwa kuhakikisha kwamba elimu tunaiwekea mikakati kuanzia kwenye elimu ya msingi. Sasa mawazo hayo twende nayo mpaka huko juu ili watu wetu wawe wana elimu ya kutosha. Ninaamini kabisa kwamba sasa hivi tunalalamika hawa watu wetu hawaajiriwi, tatizo moja hatujawaandaa watu wetu.

Mimi nilikuwa na kampuni moja walitaka kuwekeza hapa lakini bahati mbaya ile nafasi wakaipeleka Asia na wazo moja waliniambia kwamba ninyi Watanzania hamjawaandaa na ikibidi nilete kiwanda hapa itabidi nitafute, niajiri *expatriate.*

Mimi nafikiri kwamba katika utandawazi tujaribu kujibana kabisa kwamba tuhakikishe kwamba watu wetu kama inawezekana wasome bure badala ya kusema

kwamba watu walipie. Kwa sababu ninajua kabisa kwamba kwenye *Part 4 condition* zilizowekwa na hii sheria ninavyowafahamu watu wetu kwanza hawana uzoefu wa kukopa, hawana uzoefu wa dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianzisha Benki zetu hapa mliziona ziko wapi na mimi naamini kabisa kwamba hata hii gharama ya kukusanya zile hela ile *cost of recovery* zile hela itakuwa kubwa zaidi kuliko hata ile *benefit,* ninaamini kabisa kwamba hata hii Bodi itakapowekwa wakati mwingine itakuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine nilitaka niseme kwamba mishahara yetu hii tunayowalipa watu hii, je, imewekewa *provision* ya kulipa hii mikopo, sababu mtu anamaliza *University* analipwa laki moja *the living cost in Dar es Salaam* yule kweli atailipa hiyo hela. Sana sana tunatafuta namna ya kuwa-*enslave* watu, *enslavement of our educated people here now.* Kwa sababu hawataweza, vinginevyo nilifikiri kwamba Mheshimiwa Waziri wakati anajibu vile vile lazima haya mapato ya watumishi yaboreshwe, kama hayakuboreshwa pamoja na kwamba watachukua hii mikopo waweze kuwalipa na kwa kuwa hatuna sheria ya kwamba mtu akishindwa kulipa deni huwezi kumchinja. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, lazima kutakuwa na matatizo haya. Nilitaka nifahamu kwamba kumsomesha mtu akapata digrii, *first degree* inagharimu kiasi gani na je, Watanzania wetu waliotuleta hapa wanao uwezo huo wa kulipa kwa mfano unamwambia *off course* ile *guarantee* kwanza, ile *guarantee system* sidhani kama hawa watu, unakuta mtu ana nyumba ya mgongano ama ana nyumba ya tembe, sasa mtoto wake anataka kwenda kusoma itawezekana kum-*guarantee* maana yake hata kama ile *title deed* hana sasa itawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba ni kwamba tunapokuja hapa lazima tuweke vitu ambavyo ni *reality* na siyo kama naponda, sisemi kama kuponda hii. Lakini ninachosema ni kwamba lazima tuwe tunafanya vitu ambavyo *in rea*lity ambavyo vile vile vinaonyesha kabisa kwamba watu wetu wanao ule uwezo vinginevyo tutakuwa tuna-*create a problem* na kama mnavyofahamu elimu ni haki ya binadamu na hata kwenye Umoja wa Mataifa ni haki ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kwa kweli kama tunataka wananchi wetu wawe na elimu ya kutosha tutafute namna gani ya kuwawezesha hawa vijana wetu wasome na tunaamini kabisa kwamba tukiwa na Taifa lenye wasomi matatizo yetu haya ambayo yanatukabili mpaka sasa hivi na umaskini utaisha *automatically.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunisikiliza, naunga mkono, lakini ninaomba mawazo yangu yafikiriwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niseme yangu machache sina mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Pius Ngw'andu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuwa Rais wa Mawaziri wote wa Elimu katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa kuja na Muswada huu. Nasema Muswada huu ni ukombozi kwa watu ambao wanataka kujielimisha lakini wamekuwa na vikwazo vya kupata fedha ya kujiendeleza. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa juhudi ambazo wamezifanya mpaka kuweza kuufikisha Muswada huu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa kwamba 'elimu ni ufunguo wa maisha' na ni kweli kwamba dunia ya leo jambo lolote lile unalotaka kulifanya, ukitaka kupata kazi nzuri duniani bila elimu huwezi kupata, ukitaka kuwa mfanyabiashara mzuri sana bila elimu huwezi kuwa mfanyabiashara mzuri sana, ukitaka kuwa mkulima kama huna elimu nzuri huwezi kuwa mkulima mzuri sana. Kwa hiyo, kwa kila hali, elimu ni ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii lakini nataka niulize pale katika Ibara ya 7(1)(e) anasema: *"On behalf of the Board to demand and receive such fees for services rendered by the officers and other employees of the Board"*. Tunasema tunataka kuundaa hii Bodi pamoja na kazi zake za kutoa mikopo na kufuatilia hiyo mikopo ambayo itakuwa imetolewa kwa watu ambao wameomba kwa ajili ya kujisomesha, inataka kufanya shughuli nyingine ambazo itakuwa inalipwa. Lakini labda hapa naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*windup* atuambie hii Bodi inakusudia kufanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza hivyo kwa sababu suala la mikopo kwa sisi Watanzania kidogo hatuna utamaduni wa kuheshimu wa mikopo, tuna tatizo hilo. Mzungumzaji aliyepita amejaribu kutolea mfano wa vyombo tulivyonavyo ambavyo vimepata matatizo ya watu kutorejesha mikopo, tunayo mifano mingi tuna ile mifuko ya akina mama, tuna mifuko ya vijana, ukijaribu kufuatilia mikopo mingi haijarejeshwa. Mfano mzuri sana tulikuwa na Benki yetu ya *THB* tuliikopa ikaisha ikafika mahali badala ya kuwa *THB* ikawa Tanzania Hatuna Benki. Naomba kutoa wito kwa Watanzania kwamba tumepata hiki chombo ni vizuri tukakiheshimu kikaweza kutusaidia kuweza kuleta elimu kwa Watanzania wetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanzisha mfuko huu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri mwenyewe ili kuwawezesha vijana wetu waweze kupata elimu ili na wao waweze kushiriki katika soko la ajira katika huu utandawazi na katika enzi hizi za soko huria. Lakini vile vile itatusaidia kupata wataalam na tukipata wataalam inatusaidia sisi Watanzania kupata huduma bora kutoka kwao wataalam kama Walimu au Madaktari.

Lakini kama alivyozungumza mzungumzaji aliyepita, naiomba Serikali kwamba pamoja na kuwasomesha hawa wataalam ifike wakati sasa mishahara ya hawa wataalam itazamwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania tumekuwa mahodari sana wa kusomesha wataalam lakini sina uhakika kama wataalam wetu wote tunafaidika nao baada ya kuwasomesha. Siku moja nilikuwa naongea na Daktari mmoja pale Muhimbili akaniambia sisi hapa Madaktari tunapata mshahara wa Sh.135,000/=. Sasa sina uhakika kama hiyo ndiyo mishahara au alikuwa tu ananiambia kwa sababu ya mazungumzo lakini akaniambia nchi za jirani kama Botswana na Zimbabwe Daktari analipwa dola 1,500 ambayo kwa mujibu wa pesa za Tanzania sio chini ya shilingi 1.5 milioni. Sasa hivi Serikali inajitahidi kwa fedha zake zenyewe inasomesha baadhi ya hawa wataalam na leo tunaanzisha mfuko huu kwa ajili ya kuwawezesha vijana waweze kujiendeleza na baadaye kuwa wataalam ili tuweze kufaidika na vijana hawa, naomba Serikali iliangalie suala hilo vinginevyo hawa vijana wanaweza kutorekea nchi za wenzetu ambapo wanalipa mishahara mikubwa. Naomba niwapongeze wale ambao wameamua kubaki hapa kwa sababu ya uzalendo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chukulia mfano wa Madaktari, Madaktari wengi walioko Dar es Salaam unamkuta asubuhi mpaka saa nane yuko Muhimbili, saa nane mpaka saa mbili ya usiku unamkuta labda yuko *Agha Khan* na saa fulani yuko mahali pengine. Sasa hii kwa kweli ni kumwumiza huyu mtu naamini kama angepata mshahara mzuri huyu mtu asingesumbuka afanye kazi mpaka saa nane atoke saa nane aende mahali pengine akafanye kazi atoke hapo aende mahali pengine angefanya kama sisi tukishatoka hapa tunarudi nyumbani. Mtu kama Daktari mgonjwa wake anapokuwa na matatizo anatakiwa amfuate aende kumhudumia sasa unapompa mshahara mdogo ili ajiongezee mapato ameondoka kazini unasema amekwenda nyumba kumbe tena kaenda mahali pengine kwenda kujitafutia kipato kingine mgonjwa ana matatizo wakimfuata nyumbani hapatikani. Naomba Serikali iliangalie suala hili, haiwezekani kweli tukawapandishia mishahara lakini hebu tuwaangalie vizuri ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba nizungumzie pale katika Ibara ya 18 kwamba kijana au mtu anayeomba mkopo anatakiwa awe na wadhamini. Sasa wanasema: ‘kukopa ni harusi, kulipa ni matanga’. Inawezekana wengine inapofika wakati wa kulipa ikawa ni matatizo matokeo yake wadhamini wanaweza kupata taabu kwa sababu ya mtu tu kukwepa kulipa deni la elimu ambapo yeye mwenyewe ndio amefaidika. Nauliza hivi haiwezekani huyu ambaye amechukua huu mkopo moja ya dhamana ikawa ni cheti chake kwamba atakapomaliza kwa sababu hajalipa deni cheti chake kibaki mpaka atakapomaliza ndio apewe? Hivi haitakuwa vizuri kuwaondolea adha hawa wadhamini kama atakuwa ametoroka basi asisumbuliwe na kwa sababu cheti chake kitakuwa kimezuiliwa basi atakuwa hana nafasi ya kutoroka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie katika ile Sehemu ya Sita, kunatolewa msamaha kama mkopaji atakuwa amefariki lakini kuna zile sehemu nyingine zinasema kama mtu atakuwa na matatizo ya kimaisha au atakuwa na ugumu fulani fulani. Sasa hapa sijui ni ugumu wa aina gani labda hapa naomba ufafanuzi kidogo kwa sababu

naogopa hiki kipengele kisije kikatumika kama kisingizio ili kutoa upendeleo kwa baadhi ya watu, naomba suala hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho naomba wakati mfuko huu utakapoanza kufanya kazi badala ya ofisi za kutolea mikopo kuwa mahali pamoja labda mahali kama Dar es Salaam tuangalie uwezekano wa kuwa na ofisi katika Kanda au Mikoa ili kuwapunguzia usumbufu na gharama wale waombaji hasa wanaotoka katika maeneo ya mbali ya nchi yetu. Nafikiri kama tutafanya kitu cha namna hii, tutawasaidia wengi na tutakuwa tumewapunguzia gharama nyingi.

Baada ya kusema hayo, naomba nisipoteze muda, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mawazo yangu katika hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Ngw'andu, kwa kuwa Rais wa Mawaziri wote wa Elimu katika Bara hili lakini vile vile kwa kuleta Muswada huu katika muda muafaka. Shukrani hizo pia naomba zimfikie Naibu Waziri na Katibu Mkuu Mama Mollel, Mama Mollel ni mchapakazi hodari sana ni *asset* kwa Wizara hii, naye ningependa kumpongeza kwa kazi nzuri anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Mkutano huu, napenda kuungana na wenzangu kuwapongeza Wabunge wenzetu ambao katika muda mfupi uliopita wamepewa Urais katika vyombo mbalimbali vya Kimataifa, Mama Mongella na Waziri Ntagazwa, nawapa hongera sana. Wote tunajua kwamba sasa hivi hapa nchini idadi ya Shule za Sekondari imeongezeka na mazingira ya kufundisha na kujifunza pia kwa kiasi kikubwa yameboreshwa matokeo yake ni kwamba wanafunzi wengi wanafaulu na wanapata sifa za kujiunga na Vyuo Vikuu na Vyuo vingine vya Elimu ya Juu na hii ndio ilizaa Sera ya Uchangiaji na vile vile baadhi ya wanafunzi walikopeshwa.

Baada ya miaka kadhaa, Serikali ikashindwa kuwafadhili wanafunzi wote. Nikitoa mfano katika Chuo Kikuu cha Mzumbe mwaka 2003 vijana walioomba nafasi kujiunga na Chuo Kikuu na walikuwa na sifa walikuwa 4,483 lakini Serikali iliweza kuwafadhili wanafunzi 250 tu ambao ni 5.5%. Ni dhahiri kwamba vijana wengi wenye vipaji tuliwapoteza ingawa wengine walipata huku na huku wakajifadhili lakini kwa tarakimu kama hizo inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu zinazotulinganisha sisi Tanzania na majirani zetu, unapata kichefuchefu. Kwa mfano takwimu fulani nilizonazo hapa ni kwamba huu utafiti uliangalia nchi 13 zinazotuzunguka na wakaangalia katika kila wananchi 100,000 ni wahitimu wangapi wanatoka kila mwaka, Tanzania ni 7:100,000, *Mozambique* 10:100,000, Uganda 19:100,000, Botswana 40:100,000, Kenya 41:100,000, Afrika Kusini 244:100,000. Kwa mwendo huu wa kusuasua hatutafika ndio maana naona

Muswada huu utawapa fursa vijana wetu wengi ambao wana alama nzuri waweze kuendelea na masomo ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu tunachotaka kuunda ni Mfuko wa Kukopesha kama jirani yangu alivyosema hapa ni kama mifuko mingine ya kukopesha na kufanikiwa kwa mifuko yoyote ya kukopesha ni kwamba kuwe na utaratibu mzuri wa urejeshaji wa mikopo. Nia ni nzuri tu kwamba pesa iliyokopwa irudishwe katika muda muafaka ili wengine wakopeshwe na wenyewe waendelee na shule.

Kama nilivyosema hapo awali, Serikali sasa hivi inakopesha wanafunzi na Mheshimiwa Mutungirehi anasema ni mmoja wa waliokopa huko nyuma lakini mpaka leo hajarudisha pesa hizo. Kwa hiyo, sio vibaya tukaangalia uzoefu tulio nao ili tuweze kuziba, pale tulishindwa kurejesha pesa sasa hivi tufanye nini. Hoja nyingi za ukaguzi za mahesabu za Wizara hii zinatokana na malimbikizo makubwa ya fedha za mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa bado kwenye mikopo, Sehemu ya Nne katika Muswada huu inashughulikia mambo mengi pamoja na urejeshaji wa mikopo. Nakubaliana na Kamati iliyochambua Muswada huu kuhusu wadhamini kwamba masharti ya wadhamini yapewe urahisi kidogo ili isiwe kikwazo kwa vijana ambao ndio tunawalenga kwamba waweze kupata nafasi ya kwenda katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Lakini nimeangalia Kifungu Na.18(2) ambapo niliona kama kinapishana na Kifungu cha (1) anaposema na nanukuu: *"Where in granting a loan to any students the Board considers it necessary to require a guarantor or guarantors to guarantee any loan granted to a student"*. Sasa hapa tasfiri yake ni kwamba Bodi itaamua mwombaji gani alete mdhamini na yupi apewe mkopo bila mdhamini. Nadhani hiki kifungu kingeangaliwa upya uamuzi ufanyike kuwe na mdhamini au kusiwe na mdhamini kama kutakuwa ana wadhamini basi masharti yapunguzwe. Iwapo tutaona wadhamini ni muhimu basi iwe kwa wakopaji wote vinginevyo wengine watapata mwanya wa kuingia mitini kilaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya nyingi katika Sehemu hii ya Nne zinamhusisha tajiri atakayemwajiri mkopaji pindi atakapomaliza masomo yake na hapa nimetumia neno 'tajiri' nikiwa na maana ya mwajiri. Sehemu mbalimbali wamesema kwamba mkopaji atalazimika kumwarifu mwajiri wake kwamba ana deni na Serikali. Vile vile tunaambiwa mwajiri anatakiwa kuiarifu Bodi kwamba ameajiri kijana ambaye ana deni na Serikali. Mwajiri huyo huyo anahitajika kumkata mshahara na kurejesha makato haya kwenye mfuko na kati yao mwajiri na mwajiriwa asipofanya hivyo atakuwa amevunja sheria ya nchi na adhabu zimeainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikijiuliza kitu gani kitakachomsukuma mkopaji kumwarifu mwajiri kwamba ana deni? Hulka yetu sio kulipa madeni, hulka yetu sio kulipa kodi mpaka ulazimishwe sasa hapa tunasema kwamba huyu kijana amemaliza masomo anakwenda kwa mwajiri anamwambia mimi nina deni kwa hiyo uanze kunikata! Hilo ningependa liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna *mechanism* gani ya kuwafuatilia hawa vijana wetu pindi watakapomaliza masomo yao kwenye Muswada huu haikuainishwa. Halafu kabla ya kumchukulia hatua mwajiri tutakuwa na uhakika gani kwamba amepata taarifa ya deni la mtumishi wake? Kumshtaki mwanafunzi mwenye deni kama atakiuka mkataba ni rahisi kama atapatikana lakini kwa mwajiri ni vigumu labda kiwekwe kipengele katika sheria kitakachomtaka kila tajiri a-*check* na Bodi pale anapotaka kumwajiri mtumishi ili ajue kwamba huyu kijana anayetaka kumwajiri ana deni au vipi hiyo ndio inaweza kumbana kwamba ilikuwaje ukamwajiri kijana bila kuuliza au bila ku-*check* na Bodi, sasa huyu ana deni inabidi ulipe mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nataka kutoa wazo tu kwamba nchi nyingi zina mpango wa *scholarship,* sijui neno sahihi ambalo linaweza kuelezea hii kwamba tunaweza kutambua vijana ambao wana vipaji maalum, wanafaulu vizuri na ambao watakuwa *asset* kwa nchi, hawa wanalipiwa kila kitu na Serikali. Hawa ndio ambao watakuwa watafiti wakubwa, Walimu kwenye Vyuo na tungependa wabaki katika nchi kwa hiyo tukiwapa *scholarship* itakuwa motisha kwa wengine kufanya kazi vizuri ili waweze kupata nafasi ya hiyo ya *scholarship*. Naomba nitoe wazo hilo kwa Mheshimiwa Waziri ili alifikirie ingawa nadhani linaweza kuingia mahali fulani labda kwenye *schedule* hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuitakia Wizara na Bodi utekelezaji mwema wa Muswada huu pindi utakapopitishwa kama sheria. Naunga mkono hoja kwa asilimia zote, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi nami kuungana na wenzangu pamoja na kwamba kina Mheshimiwa Mongella nimeshawapongeza tulipoandaa *party* sisi Kamati ya Ulinzi na Usalama, lakini nataka niungane na wenzangu kuwapongeza Marais wote na kuwatakia mafanikio. Tunafikiria labda faida kubwa ya kuchaguliwa kuwa Marais wa Afrika haikuja tu ni historia labda ya Taifa letu la Tanzania pengine na Miswada kama hii ambayo tunaijadili na kutokana na elimu yao kubwa ambayo Mungu amewabariki. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Muswada huu muhimu kwa Taifa letu la Tanzania na nimtakie mafanikio ambayo kwa kweli yataweza kuikomboa jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonishawishi kusimama kuchangia ni ile dhana iliyomo katika Muswada kama Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha kwamba Muswada huu umekuja kulenga pia kuwawezesha na wale maskini waweze kupata elimu. Nikimnukuu Baba wa Taifa katika moja ya hotuba zake ambazo nimewahi kuzisikia alikuwa akizungumza na vijana, walimwuliza, Mwalimu tufanye nini ili tuwe viongozi bora kama wewe? Akawaambia vijana someni kwanza. Halafu akawaambia kwamba sifa moja ya kuwa kiongozi bora ni kuwajali wanadamu wenzako na sifa hii uwe kiongozi usiwe kiongozi inamstahiki kila binadamu. Kwa hiyo, hapa Serikali, Wizara imefanikisha ile dhana kubwa ambayo Baba wa Taifa aliijenga kwenye jamii ya Taifa la Tanzania, kuwapatia elimu ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichangia tena Muswada kama huu kutoka Wizara hii ya Sayansi na Teknolojia, nilisema kwa mujibu wa taarifa za wataalam duniani zinasema msingi mkuu wa uchumi duniani ni elimu, sayansi na teknolojia ndio msingi mkuu wa elimu wa nchi yoyote ile duniani. Kwa hiyo, mimi sitakuwa na hofu wale ambao watashindwa kurudisha mikopo hii, sina hofu kwa sababu kama Taifa ni lazima watumie haki yao ya nchi yao kuwapatia elimu. Serikali yetu ni suala la utandawazi lazima tuwawezeshe vijana wetu wawe na uwezo wa kufanya kazi popote. Juzi Serikali ya Tanzania imewapokea Madaktari kutoka Cuba na wengine tumewaona jana katika *Television* wamepelekwa Zanzibar na wengine Pemba tunaimani wale wote hawakuajiriwa Serikalini wametokea Vyuoni pengine wamepelekwa *field* kwa ajili ya kusaidia yale Mataifa. Kwa hivyo, huu msingi, tusifanye hofu kwamba labda hawatarejesha mikopo lakini jukumu letu kubwa ni kuwapatia elimu kwa faida ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikinukuu katika Muswada huu Sehemu ya Pili yenye Ibara ya 4-6, inapendekezwa kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo, hadhi ya kisheria ya Bodi hiyo pamoja na majukumu yake. Mheshimiwa Waziri hili uliangalie sana kwa sababu suala lolote ambalo tutaliingiza kwenye masuala ya kisheria linahitaji lifuate utaratibu ule ule ambao tuliuweka kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, kama kutastahiki kupatikana haki iliyostahiki kwa kila Mtanzania, tunaomba Muswada huu utekelezeke na moja ni Bodi ya Mikopo, kwa hiyo kusiwe na upendeleo katika ku-*appoint* Watanzania ambao watastahiki, kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, Bodi hii iratibu kama Muswada ulivyoelekeza kwa faida ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hifadhi ya kisheria ya Bodi hiyo kwa hiyo sheria zitakazokuwa zimeingizwa kwenye Muswada huu zifuatwe na taratibu zote zilizowekwa isije tumika *naizesheni* kwa kuwasaidia watu kutumika labda uenyeji na mambo mengine, napenda kulisisitiza suala hili. Lingine ni majukumu yake ambayo Bodi hiyo imepewa. Kwa hiyo, tunaitaka ifanye kwa mujibu wa majukumu iliyopangiwa kwa sababu kama Bodi hii itafeli kufanikisha Muswada huu, hatutafika pale ambapo tumepakusudia. Mimi sishangai kwa nini tumechelewa au kwa nini nchi yetu inatoa mikopo midogo, kwa kweli historia ya Taifa letu tunajua tulipotoka jamani, tusidanganyane na tusitoe mifano ya Kenya, Afrika Kusini, Uganda sisi tumeanza uchumi kwenye miaka ya 1980 kote huko tulikuwa katika vita katika Bara zima la Afrika. Hata juzi hapa kulikuwa na mmoja alizungumzia kuhusu masuala haya, Mheshimiwa Chubi kwamba kumbe wamekosa kupata umeme kule kwa ajili ya kuisaidia nchi kama ya Msumbiji. Kwa hiyo, kulikuwa na sababu ingekuwa sio matatizo haya tungeshaondoka zamani sana kwa hiyo tuangalie suala hili, tusimamie Muswada huu kulisimamia Taifa ili vijana wetu waweze kufanikiwa yale malengo ambayo tumekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne yenye Ibara 16-24, inapendekeza wajibu na haki za wahusika mbalimbali chini ya utaratibu wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo hiyo. Naomba utaratibu huu uliongizwa kwenye Muswada huu usibakie kwenye Muswada, wahusika wote wajulishwe waelewe utaratibu mzima ambao Serikali ina mipango namna gani inataka kuwasaidia wananchi hawa kwa ajili ya kujitafutia elimu na

kusiwe na *vitiation* wapewe miongozo na mawazo laini ili wawe na imani ya kuweza kuchukua mikopo hii kwa kujiamini kabisa wakijua kwamba wanachukua ni pesa za Taifa leo, kodi za wananchi wao na ambazo Serikali imeamua kwa nia safi sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri eneo hili ninakuomba ulisimamie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu inasema wajibu na haki hizi au nasema mimi, ninaomba ziwafikie walengwa zisije zikabakia katika vitabu. Nasisitiza Mheshimiwa Waziri hapa, isiwe Muswada wa kupitisha tu lakini mara tu Muswada huu ukipata wananchi wote wa Tanzania kupitia vyombo vya habari, kupitia bodi, shule, waelezwe madhumuni ya Muswada huu na wana haki gani ili wananchi wengi waweze kuomba mikopo hii. Kuhusu utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaostahili, nauzingatia kama ulivyoelezwa ndani ya Muswada huu. Kwa hiyo, wale waliolengwa, wanaostahili kupata mikopo hii tuwaangalieni kama ulivyosema kwamba tumeangalia kwamba kuna wanyonge tuliona walikuwa wanakosa elimu kutokana na kufanya hilo zoezi. Kwa hiyo, isije kuwa Bodi hii ikatumia fedha hizi kwa maslahi yao au ikawepo rushwa na kila baada ya muda fulani muwawekee malengo maalum wawe wanatoa taarifa zinazostahiki ili jamii ijue yale masuala yanavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimenukuu ni wajibu wa wahusika kuhusu urejeshaji wa mikopo na hatma ya watakaoshindwa kurejesha mikopo yao pamoja na kwamba yapo mambo ambayo yamefafanuliwa katika Muswada huu. Lakini zuri zaidi ni kwa Bodi hii kuwa karibu sana na wahusika kwa muda wote. Hili naliomba sana. Hii Bodi iwe karibu isiwe imeshatoa mikopo inasubiri vijana wetu washindwe waanze kuwachukulia hatua kama ambavyo Bodi ile imewaruhusu, wawe karibu nao, kuwapa moyo na maelekezo na kwa wale watakaoshindwa Mheshimiwa Waziri tunaomba muangalie hali zao je, ameshindwa kulipa kwamba anacho hataki kulipa au hana. Haitatupa faida kusema labda tuzuie cheti tumruhusu kama kuna nchi ataweza kwenda kupata kazi na akajua kwa muda fulani ataweza kurudisha lile deni hata kama tuwaandalie, kuwaombea kazi nje ya nchi yetu wakafanye kazi baada ya miaka fulani warudishe fedha zile, hawana uwezo kwamba akauze kilichopo nyumbani kama una elimu nzuri kuna Mataifa yanahitaji wataalam tuwapeleke wakafanye kazi baada ya muda fulani waweze kurejesha. Kwa hiyo, hili liwe ni jukumu la Mabalozi wetu walioko nje kama wanavyotangaza utalii wa nchi hii wajue katika Tanzania tuna wasomi wangapi, wa aina ngapi na kuna Mataifa gani yanahitaji watu wale kwenda kufanya kazi? Hili Mheshimiwa Waziri, naomba kama Serikali ilisimamie.

Mheshimiwa Waziri, sikuwa na nia ya kutaka kusimama lakini nilivutika na ushawishi mkubwa kusema kwamba dhana kubwa ni kuwasaidia wale ambao Serikali mliona kwamba walikosa elimu. Lingine kubwa Mheshimiwa Waziri nataka nikupongeze kwa kweli ni muda sasa hivi hakuna mgogoro katika Vyuo vyetu Vikuu. Kwa dhati kabisa nachukua nafasi hii kuwapongeza wanafunzi wetu wa Vyuo Vikuu vya Tanzania.

Kwenye miaka ya sabini wakaweza kugoma na hili nataka nilizungumze, viongozi wa Vyama vya Siasa au sisi watu wa siasa tusiwashirikishe wanafunzi katika mambo ya siasa, tuwaacheni wasome kwa faida ya Taifa hili na kwa faida yao wenyewe. Lakini leo tunasababisha mwanafunzi anagoma, anakosa elimu, tutakwenda wapi?

Inatusaidia nini? Kwa hiyo, hili nalizungumza kwa uchungu kabisa, tuwaacheni vijana wetu wajisikie na niwaonye vijana wetu walioko katika hivyo vyuo washughulikie elimu, ndiyo mtaji wao peke yake hakuna lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo namwunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ARID M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria wa Bodi ya Mkopo wa Serikali kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu wa Mwaka 2004, ambao umewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza mchango wangu na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuwapongeza Wabunge wenzetu ambao wamechaguliwa kuwa Marais Kimataifa nikianzia na Mheshimiwa Getrude Mongella, ambaye amechaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika au African Union. Mwingine ni Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, ambaye amechaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani na wa tatu ni Mheshimiwa Waziri wa Sayansi mwenyewe, Mheshimiwa Pius Ngw'andu, ambaye naye amechaguliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu katika Afrika. Nasema hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonyesha ni jinsi gani Bunge lako Tukufu limekuwa makini katika kuwateua wenzetu ambao tunawapeleka katika vyombo hivi vya Kimataifa na Kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa nianze mchango wangu kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, watendaji wote wa Wizara hii kwanza kwa kuandaa Muswada huu na vile vile kwa kuuwasilisha vizuri katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwenye kifungu cha III(9)(1) inazungumzia Bodi kukasimu madaraka kwa Kamati au mfanyakazi wa Bodi kazi zake au sehemu ya kazi zake. Ningeshauri Bodi ikasimu madaraka au kazi zake kwa Kamati peke yake lakini siyo kwa mfanyakazi mmoja na hii ni kutokana na hali halisi kuwa wapo wafanyakazi ambao kwa kweli siyo waaminifu, kwa hiyo anaweza akatekeleza kazi hizo za Bodi aidha kwa upendeleo au kwa manufaa yake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu hicho hicho cha III(9)(2) mstari wa nne kuna neno pale ofisa, nina hakika lile lingesomeka ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 11(1) inazungumzia uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji ambapo Kamati itapitia maombi yote na kupitisha maombi machache ambayo yatapelekwa mbele ya Bodi. Bodi nayo itapendekeza jina moja kwa Waziri kwa uteuzi. Naomba Bodi badala ya kupendekeza jina moja basi kungekuwa na majina zaidi ya moja na hapa ningependekeza *at least* majina matatu ambayo yangepelekwa kwa Waziri ili kumpa Waziri wigo mpana zaidi wa kufanya uteuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu cha IV(16)(2) inaeleza gharama ambazo zitapatiwa msaada. Pamoja na yote yaliyotajwa kwenye sehemu ndogo za (a), (b), (c), (d), (e), naomba kuongeza usafiri wa kwenda na kurudi kutoka chuoni na vile vile matibabu hasa ukichukulia kwa hivi sasa jinsi ambavyo gharama hizo zimepanda ingekuwa vigumu kwa wanafunzi wengi sana kuzimudu. Kwa hiyo, naomba hizi nazo zingeongezwa zika-*cover* kwenye msaada huo au mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 17(b) inaelezea umri wa mwombaji kuwa asizidi miaka 45 kwa vyuo vya kawaida na miaka 60 kwa vyuo huria. Huku ni kuwanyima haki wale wote wanaotaka kujiendeleza. Naomba umri huu uongezwe kutoka miaka 45 kwenda 50 kwa wale wa vyuo vya kawaida na miaka 60 kwenda 65 kwa wale ambao wapo kwenye vyuo huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ibara ya 17(e) ya kifungu hicho hicho cha IV kinaelezea kuwa Bodi haitasaidia wanafunzi wanaorudia masomo na wanaoanza masomo. Naomba Bodi iwasaidie vile vile wanafunzi hao kwa sababu inawezekana kukawa na sababu za msingi hadi wanafunzi hao wakarudia masomo na kwa wale ambao wanaanza hawa ndiyo wenye matatizo makubwa zaidi. Kwa hiyo, kwa kweli wanastahili kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18(2) ya kifungu cha IV inazungumzia juu ya Bodi kudai mwanafunzi kuwa na mdhamini au wadhamini ili mkopaji akishindwa kulipa mkopo basi mdhamini au wadhamini walipe. Hali hii kwa kweli itawanyima haki wanafunzi hasa wale ambao wanatoka Vijijini watakosa udhamini. Ni jinsi gani basi watoto hao wa walala hoi watasaidiwa kupata mikopo hiyo. Naomba Wizara ingetueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo Ibara ya 18(3) itakuwa kikwazo kwa wananchi wengi kujitokeza kuwadhamini wanafunzi. Naomba kazi ya mdhamini iwe ni kuisaidia Bodi kumpata mkopaji kwa kueleza yuko wapi na anafanya kazi gani lakini siyo yeye ndiye sasa alipe mkopo wakati mkopaji anapokosekana. Hapa tumeelezwa kuwa Serikali za Vijiji zitaweza kuwadhamini lakini nina hakika kwa Serikali nyingi za Vijiji hazitakuwa na uwezo wa kurudisha hiyo mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha VI (29)(1) kinazungumzia kusamehe mikopo. Pamoja na sababu zilizoelezwa kwenye (a), (b), (c) naomba iongezwe sababu mojawapo kwa kukosa ajira. Inawezekana kuna mtu kutokana na mazingira au hali yake amekosa ajira ya kufanya kwa hiyo huyu mtu naye anastahili kusamehewa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye jedwali Ibara ya 2(3) inazungumzia hatua za kufuatwa kujiuzulu kwa mjumbe wa Bodi kwa kuandika barua kwa Rais. Naona wajumbe wote huteuliwa na Waziri hivyo hakuna haja ya mjumbe anapojiuzulu kupeleka barua kwa Rais. Barua zipelekwe kwa Waziri tu aliyewateua.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya maoni na maombi yangu hayo nitamke kuwa naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. Mwisho, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii, lakini vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nami kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani na Mheshimiwa Dr. Pius Ngw'andu, kwa taarifa alizotupatia leo, ambazo kwa bahati mbaya nasikitika tulikuwa hatujazipata kwa muda mrefu kwa nafasi kubwa ambayo alipewa ya kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu ya Juu, Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba nitaunga hoja hii mkono kwa masharti. Sharti la kwanza ambalo ni la msingi kabisa ambalo nitaomba na Mheshimiwa Waziri anielewe yapo mambo mawili ambayo ni ya msingi.

La kwanza, kuna hoja ya kuanzisha Bodi ya kusaidia kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, hilo ni jambo moja. Lakini kuna jambo la pili la utaratibu tuliokubaliana mwaka 1994 kwamba *cost sharing* katika elimu ya juu itakwenda kwa awamu. Tulianza na awamu ya kwanza, tukaingia awamu ya pili na awamu ya tatu haijaanza. Sasa isije ikawa ninapounga hoja hii kupita maana yake sasa nimeunga mkono hoja moja kwa moja kuingia awamu ya tatu ya *cost sharing*. Nilipenda niliweke hili sawasawa kwa sababu ni vitu viwili tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu za *cost sharing* katika elimu ya juu na Muswada huu kwa sababu kama tukichukulia maana yake ni kwamba ni *automatic* tunaunga mkono awamu ya tatu sasa tutakuwa tumekwenda kinyume na Serikali kwa sababu tulikubaliana na Serikali wakati ule nilipokuwa nasoma na Mheshimiwa Mutungirehi na wengine tuliokuwepo kwamba hizi awamu za *cost sharing* zitakwenda taratibu.

Tutaanza na awamu ya kwanza, tuitathmini kama inakwenda sawasawa tunaingia ya pili, tutafanya tathmini kama ipo sawasawa, tunaingia awamu ya tatu. Sasa sijaona tathmini ya awamu ya pili, ndiyo maana nasema isije ikachukuliwa kwamba sasa naunga mkono utekelezaji wa awamu ya tatu. Kwa sababu awamu ya tatu ina mambo ya msingi ambayo lazima yaangaliwe kwa karibu kabla ya kuianza.

Sasa Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nilitaka niliseme ili tuelewane isije baadaye kesho kutwa Mheshimiwa Waziri akasema na Waheshimiwa Wabunge walishaamua kupitisha hoja hii kwa hiyo *automatic* walishaunga mkono awamu ya tatu. Awamu ya tatu ni nzito kwa sababu inahusu *fees* na mambo mengine mazito mazito na lazima tuyatazame kwa makini na Wizara ijiridhishe kwamba sasa ikiingia hatua hiyo hayatakuwepo matatizo mengine ambayo tutakuwa hatujayatarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kwa Muswada wenyewe, kifungu cha 3 kimetoa maana ya *accredited institution* ikaieleza pale, lakini mimi ningependa kusema kwamba, labda nikisome ili kuweka mambo sawasawa. Katika *schedule of amendments accredit institution* wametuambia *means institution which are licensed to offer courses which lead to attainment of Degrees and all Advanced Diplomas.* Sasa ambalo ningependa niliongeze hapa ni kwamba tuseme *accredited institutions means institution which are licensed by Tanzania higher education Accreditation Council* na tuendelee mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo, kwa sababu zipo *University* nyingi ambazo zipo *accredited* lakini nyingine zipo nje ya nchi. Sasa si kila *University* iliyo nje ya nchi kwa sababu ipo *accredited* na chombo kingine basi *automatic* ukienda kusoma kule upewe mkopo. Lakini ambacho ningependa kusisitiza hapa ni kwamba mimi kwa uzoefu wangu katika masuala ya elimu na katika masuala ya mikopo kwa wanafunzi mimi ningeshauri mikopo hii itolewe kwa wale wanaosomea ndani ya nchi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo sababu kwa nini nasema hivyo. Sababu ya kwanza ni kwa sababu Serikali ilishaeleza kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwamba kuanzia sasa haitaendelea kuendelea kusomesha wanafunzi katika *Degree* ya kwanza nje ya nchi kwa fedha za bajeti, ilitamkwa kwamba kwa fedha za bajeti hatutapeleka kusomesha wanafunzi nje ya nchi. Sasa kama ulishatamka hivyo kama Serikali haiwezekani leo hii tukasema sasa Bodi hii itatoa fedha za kusaidia kusomesha wanafunzi nje ya nchi. Nafikiri tutakuwa tumejichanganya labda kwanza Serikali isahihishe kauli yake iliyoitoa kwamba haitaendelea kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya kupeleka wanafunzi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hii isichanganywe na zile *scholarship* mbalimbali ambazo tunazipata. Kwa mfano, Serikali ya Urusi inaweza ikatoa *scholarship* au kuna *arrangement* mbalimbali, sio hivyo naongelea kutumia fedha za bajeti. Sasa labda Wizara isimame iseme inarekebisha kauli yake, mimi sina matatizo lakini ninachofahamu msimamo wa Wizara ni kwamba kuanzia wakati ule hakuna kupeleka wanafunzi kusoma nje ya nchi kwa fedha za bajeti kwa sababu unatumia fedha nyingi mno kusomesha mwanafunzi mmoja kwa *Degree* ya kwanza nje ya nchi kuliko ambavyo ungetumia fedha hizo ukasomesha wanafunzi wengi zaidi ndani ya nchi na mimi nilikubaliana na hoja ya Serikali kimsingi kabisa. Kwa sababu hiyo hiyo, kwa *logic* hiyo hiyo, ukiamua sasa kusema fedha hizi zianze kusaidia kusomesha hata wale wanaokwenda kusoma nje ya nchi maana yake sasa utabaki na fedha kidogo za kusaidia kukopesha wale ambao wanasoma ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja ya pili kwa nini nasema wanaokwenda nje kwa *Degree* za kwanza wajisomeshe wenyewe ni kwamba ukiwatazama hawa wana uwezo. Sasa kama tayari mtu ana uwezo na anafikiria kwamba mtoto wake asome nje ya nchi sioni sababu ya kurudi kwa fedha kidogo tunazotenga kwa ajili ya maskini ambao hawana hata ile ya kufikia kwamba aende kumsomesha mtoto wake hata Uganda kwa kutumia fedha hizo tutakuwa tunajichanganya. Kama una uwezo unaamua mtoto wako

asomee Uingereza, London au Marekani sawasawa lakini tuache fedha kidogo hizi tulizonazo kwa ajili ya kusaidia wale wanaosomea ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itaona kwamba katika *program* fulani kwa mfano *let say information technology* na nyinginezo haiwezekani tukapata wataalam kwa *Degree* ya kwanza ndani ya nchi basi kwa umuhimu huo Serikali basi itenge fedha zitumike kusomesha watu hao kwa masomo maalum ambayo tunafikiri kwamba hatuwezi kukosa wataalam hao. Hilo ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ningependa niiseme hapa ni kwamba kifungu cha 17(d) kinasema anayepaswa kupata mikopo ni yule ambaye atathibitisha kwamba hana uwezo wa kupata fedha kutoka *sources* yoyote ile, sifa mojawapo kwamba Bodi iridhike kwamba hauna uwezo wa kupata fedha kutoka sehemu yoyote ile. Sasa hii nadhani huu ni utani kwa sababu kwanza ni ngumu kuweza kutambua huyu mtu hana uwezo wa kupata *sources* eneo lingine. Lakini vile vile uzoefu wangu unaonyesha mwaka 1994 tulipokuwa tunaanza haya mambo ya mikopo nakumbuka wakati ule walisema kwamba kama mzazi wako ana uwezo wewe hutastahili kujaza zile fomu za kuomba mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukamwambia Waziri wa Sayansi na Teknolojia wa wakati ule tukasema hii si kweli kwa sababu uzoefu unaonyesha kwanza watoto wote wa Mawaziri watakuwa wa kwanza kuonekana kwamba ndiyo hawana uwezo. Tukimaliza hao watoto wa Makatibu Wakuu wote wataonekana hawana uwezo. Tukimaliza hao watoto wa Waheshimiwa Wabunge wote wataonekana hawana uwezo na huo ni ubinadamu huwezi kulaumu mtu kwamba kama kuna kitu hapa na wewe ndio unasimamia ukiwa wa kwanza basi utajitazama. Huo ndio ubinadamu sitaki kusema kwamba hivyo ndivyo nilivyo bali ndiyo ubinadamu kwamba utajitazama kwanza wewe kabla ya kutazama kule. Sasa kujaribu kuweka kipengele hapa ambacho utekelezaji wake utakuwa siyo sahihi kitaishia kuwanyima watoto wa maskini uwezo wa kupata mikopo na badala yake wale wengine ndiyo wataonekana kwamba hawana uwezo.

Kwa hiyo, ili mradi tumeshaweka sifa kwamba tunataka wale kuwasaidia kusoma basi ukipata *admission* ndani ya nchi uwe na uwezo usiwe na uwezo basi tuwaachie waweze kupata hii mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu ukweli ni kwamba hata kama wewe ni Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Mbunge wapo watu wanaweza kuwa wanafikiri kwamba Mheshimiwa Mbunge sasa huyu nadhani ndiyo ana uwezo labda mtoto wake angemsomesha. Lakini ukweli hali halisi tunafahamu sisi Waheshimiwa Wabunge wenyewe kwamba kabla hujafika nusu ya mwezi, ile pesa ya mshahara kidogo unayoipata inakuwa imeshakwisha. Sasa kama wewe Mbunge huna uwezo sasa unawekaje kipengele tena cha kusema atakayeonekana ana uwezo basi huyo asipate mkopo.

Nadhani ni kipengele ambacho hakina maana yoyote ile tukiondoe kabisa ili tuache kutengeneza mianya ya rushwa. Kwa sababu tukikiacha hapa tutakuwa

tunatengeneza mianya ya rushwa ya kumpa mtu fulani namna ya kuamua kwamba ni nani apate mkopo na nani asipate mkopo. Kwa hiyo, njia mojawapo ya kupambana na rushwa ni kutengeneza sheria ambazo haziweki mianya ya kufanya maamuzi ambayo hayaeleweki eleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende *clause ya 18* inasema kwamba *security.* Wameliongelea wengi waliotangulia lakini na mimi naomba niseme unapotaja kwamba hawa wanaoomba mikopo itabidi awe na *security* inaleta utata, ingawa Mheshimiwa Waziri kwa kutumia uzoefu wake alijua kabisa suala hili Waheshimiwa Wabunge wengi watalipinga na kwa hiyo akajaribu kuonyesha kwamba ni jambo jepesi kwamba hata Serikali za Vijiji na nani wanaweza waka-*act as a grantor,* lakini naomba niseme katika Muswada huu tunasema kwamba ile Bodi itaamua kipi kinaweza kikawa *security.* Sasa ukishaipa Bodi uwezo wa kuamua kipi kinaweza kuwa *security* huizuii Bodi ikakaa ikasema kila atakayetaka mkopo lazima awe na nyumba maana umeshaipa uwezo wa kuamua kipi kiwe *security.* Kwahiyo, ili kuondokana nautata huo sisi watunga sheria lazima tuamue kwamba ili mradi mtu amepata nafasi katika Chuo cha Elimu ya Juu, hiyo ni *security* ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo tukiipitisha kama ilivyo hivi baadaye tujiandae kuingia kwenye migogoro isiyo ya msingi ya kuanza kubeba barua kwenda kwa Waziri unajaribu kumwambia huyu hapa namfahamu ni maskini lakini amenyimwa mkopo. Sasa mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge tunazo kazi nyingi za kufanya na tungehitaji kupata hata muda mwingi wa kufikiri kwa ajili ya maendeleo kuliko kuwa tunafanya kazi hizi nyepesi nyepesi za kuzunguka na barua tukijenga hoja ambazo ni sisi wenyewe tumetengeneza sheria ambayo ina mapungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja za kwamba wale wanaotaka *Masters* na *Ph. D.* na wao wapate mikopo mimi nasema hii hakuna kabisa. Tuache watu ambao bado wanatafuta *Degree* ya kwanza hawa ndiyo tuwape mikopo. Wewe unataka *Masters* kama mwajiri wako ana uwezo akusomeshe kama hana uwezo jaribu kutumia *Degree* yako ya kwanza vizuri pata fedha kajisomeshe, wewe kama unataka *Ph. D.* unataka mkopo kwanza kama unataka *Ph.D.* na unataka mkopo haustahili hata kusoma hiyo *Ph.D.* Kwa sababu inatakiwa kwakutumia *Degree* ya kwanza uliyoisoma uweze kuitumia vizuri angalau uweze kusoma *Masters* na *Ph.D.*

Sasa wewe tumekupa Degree ya kwanza bado uwezo wako wa kufikiri ni sifuri na bado unataka sasa uendelee sasa kupewa mikopo, si kweli, si kweli hata kidogo. Tuwaachie vijana wetu wa *Degree* ya kwanza wapate mikopo wakasome. Hizi fedha ni kidogo ndiyo tuwasaidie kwa kutumia fedha hizi. Kama ni *Ph.D.* kuna njia nyingi za kuweza kusoma *Ph.D.* unaweza ukajisomesha, unaweza ukaandika *proposal* nzuri *on competitive basis,* ukitaka nenda kwenye Vyuo vya Ualimu kama umesoma vizuri na wewe ukawa *a lecturer,* kule kuna hela nyingi za kusomesha watu, siyo tena kutaka kutumia pesa hii tunayotenga kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nimalizie kwamba na mimi ni kati ya watu ambao tulichukua mkopo mwaka 1994, kwa hiyo naungana na Mheshimiwa Mutungirehi

kwamba tulikuwa wote. Lakini napenda nimsahihishe rafiki yangu Mutungirehi bahati mbaya amekimbia maana wakati ule yeye alikuwa Rais wa Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mimi nilikuwa Rais wa Wanafunzi Mzumbe. Kwa hiyo, tulikuwa sehemu ya kwanza kwa hii *cost sharing.*

Sasa mimi nakumbuka wakati ule tulisaini fomu za kuchukua mikopo kwa hiyo si sahihi kuanza sasa hivi kusema basi tusilipe, kuna haja ya kujenga hiyo tabia. Lakini ambacho ningependa nisisitize hapa hoja ya kwamba turudi mpaka nyuma mwaka 1965, sina ugomvi nayo lakini tusitumie hoja ya mwaka 1994 kwamba kwa sababu sijui nani wameambiwa walipe basi wasilipe hawa mpaka tuanzie mwaka 1965.

Sisi tulisaini fomu wakati ule, tuli-*negotiate* vizuri, tulikaa Wizarani pale, tukajadiliana fomu zikatolewa watu wakasaini. Kwa hiyo, ni vizuri kuheshimu hizi taratibu na hoja ya kwamba watu walichukua mikopo kwa sababu ya migomo si kweli kwa sababu Serikali haitishwi na migomo mimi ninavyofahamu. Serikali huwezi kuitisha kwa migomo. Serikali inaweza kuamua kuondoa wanafunzi wote kwenye vyuo vya elimu ya juu na ikaleta wengine. Kinachotakiwa ni ujengaji wa hoja. Ni kwamba Serikali wakati ule ilitambua umuhimu wa kutoa mikopo, wakajadiliana vizuri, tukapata muafaka, lakini kama Bunge hili likipitisha sheria ya kusamehe tutashukuru, hakuna anayependa kulipa madeni, lakini mkopo upo pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme kwa sharti nililolitoa, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja muhimu sana iliyo mbele yetu. Lakini kabla sijaanza mchango wangu na mimi nichukue nafasi ya kuwapongeza wafuatao: Kwanza Mama Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Nasema hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Mheshimiwa Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani, naye vile vile hongera sana. Lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Ngw'andu, nampongeza sana kwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu ya Juu katika Bara la Afrika. Hongereni sana. Mmetupa heshima kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo sasa nilenge maudhui ya Muswada huu lakini kabla sijalenga vizuri niwapongeza Mheshimiwa Ngw'andu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa kuandaa Muswada huu vizuri sana. Ameuandaa vizuri kwa sababu kafafanua upo kiuchumi Muswada huo, kijamii na vile vile kisera na pia kimaendeleo. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ndugu yangu Zabein Mhita, kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri wake mpaka wakafanikisha kuleta Muswada hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo mimi sina tatizo lolote na mapendekezo ya Sheria hii ya kuanzisha taasisi hii pamoja na kuanzisha Bodi yenyewe na nasema kwamba naunga mkono moja kwa moja kwa maana mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nataka niishauri Serikali na kuiomba ama kuitaka kwamba ili kuongeza vijana wetu na watu wetu kwenye Vyuo Vikuu mbalimbali hapa nchini lazima tuchukue hatua mbalimbali na hatua hizo mimi nimeziorodhesha ili ziweze kutumiwa na Serikali na nafikiri zikitumiwa tutaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kwanza ni kwamba Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* ambacho kipo pale Dar es Salaam, kiwe Chuo Kikuu kisheria. Ni muhimu sana kwa sababu tumefanikiwa sana katika mpango wa MMEM na inaelekea tutafanikiwa sana katika mpango wa MMES, kwa maana tutakuwa na sekondari nyingi, lakini pia lazima tuwe na Vyuo Vikuu vingi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendelea kuwa na Vyuo Vikuu vichache. Kwa hiyo, hilo ndilo pendekezo langu. Tumewahi kuelezwa kwamba ni Chuo Kikuu lakini bila sheria. Kwa hiyo, nasema kiwe Chuo Kikuu kisheria ili kiweze kusaidia kutatua matatizo katika maeneo yetu haya ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam kile ambacho kipo Chang'ombe nacho kina sifa nyingi za kutosha, kinafaa vile vile kuwa Chuo Kikuu, maana kadri tunavyoboresha huu Muswada utaboresha sana mambo mengi ya elimu. Kwa hiyo, tutazaa matatizo vile vile kwa sababu vijana wengi watahitaji kwenda Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu ndiyo hivyo vichache. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima vilevile tujiandae kuanzisha Vyuo Vikuu vingi. Kwa hiyo, mimi napendekeza Chuo hiki cha Ualimu cha Dar es Salaam vilevile tuletewe Muswada hapa tupitishe kiwe Chuo Kikuu, hatuna sababu ya kukiacha maana kina sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Chuo cha Ualimu kile cha Kleruu kule Iringa, Chuo hiki ninakifahamu sana kwa sababu nimefika kule vilevile kina sifa nzuri tu na hadhi ya kutosha kabisa na kinaweza kikachukua wanafunzi wa kutosha wa Shahada ya Kwanza na kuendelea hasa tulenge katika Shahada ya Kwanza. Halafu Shahada ya Pili na kuendelea wataenda katika Vyuo vingine ni muhimu sana. Sisi tunajua kabisa tuna upungufu kabisa wa vijana wa Shahada ya Kwanza hasa katika Shule za Sekondari zetu. Vijana wengi ni wale ambao wana *Diploma* ndiyo wanafundisha katika Shule za Sekondari zetu. Lakini ni muhimu lazima vijana wenye *Degree* ya Kwanza ndiyo wangestahili kufundisha katika Shule za Sekondari. Kwa hiyo, ni muhimu sana tufungue Vyuo vingine Vikuu tusibaki na Vyuo vile ambavyo sasa hivi ni vichache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kingine ni kile cha Marangu kule Moshi. Mimi bahati nzuri nilipitia pale wakati nasomea ualimu mwaka 1970 na 1971 kilikuwa kinachukua wanafunzi zaidi ya 1,600 na kina sifa ya kutosha tunaweza tukakifanya

vilevile kuwa Chuo Kikuu kitasaidia sana kukabili mafanikio ya Muswada huu ambao tutaupitisha kuwa Sheria. Maana tunapoandaa hivi lazima vilevile huku juu tuandae mazingira mazuri kwa vijana kupata elimu ya juu. Kwa hiyo, namwomba basi Mheshimiwa Waziri anayehusika wazungumze na Waziri wa Elimu na Utamaduni, wachukue Vyuo hivi wavikarabati ili kuviwezesha kuwa Vyuo Vikuu ili viweze kutusaidia kupata wasomi wengi wa Elimu ya Juu, kwa sababu tunao wachache kwa sababu Vyuo Vikuu ni vichache.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wenzetu wanatembelea lazima sisi tukimbie kweli kweli. Kama wenzangu walivyotoa mfano, Kenya na Uganda, hawa walitutangulia sana katika maamuzi ya namna hii hii, kwa sababu walikuwa na majengo wakaamua kuanzisha Vyuo Vikuu vingi. Kwa hiyo, wametupita kwa hatua nyingi tu. Kwa hiyo, sisi sasa lazima tukimbie tulingane nao na hata ikibidi tuwapite tuna nafasi ya kuwapita sisi, kwa sababu sisi Watanzania ni wachapa kazi kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, Chuo kingine ambacho nimeona ni muhimu vilevile, mimi nimependekeza Vyuo vitano, Chuo cha Ualimu Butimba, Mwanza kule ni kizuri vile vile kinastahili kabisa. Utafiti ukifanywa Vyuo hivi pamoja na hivi vingine vinaweza kabisa kutusaidia.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri azingatie hilo kama kweli tumedhamiria vijana tutakaowasaidia, tutakaowapa mikopo na kadhalika, watatiririka kweli kweli kutoka kwenye Shule zetu za Sekondari ambazo tumeziandaa na tunaendelea kuziandaa. Kwa hiyo, lazima wakute mahali pa kwenda na kupata elimu wanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwamba mpango huu wa MMEM umefanikisha sana, ndiyo maana hata kufaulu kwa mtihani wa darasa la saba sasa umepanda, upo katika asilimia 42 mpaka hata 43. Kwa maana hiyo sasa pale tuna vijana wengi wanatakiwa kwenda katika Shule za Sekondari. Na kwa maana hiyo tunatakiwa kuwa na Shule za Sekondari nyingi na wanaomaliza Elimu ya Sekondari nina uhakika kwa sababu ya kuboresha Shule zetu za Sekondari watafaulu vizuri sana. Sasa tutafikia wakati, mahali pa kuwapeleka hakuna kama hatukujitayarisha. Kwa hiyo, naomba basi Serikali izingatie suala la kuanzisha Vyuo Vikuu vingi ili tutatue matatizo haya kwa misingi inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie tu kwamba katika mfumo wa zamani kwa kweli watoto waliokuwa wanatoka katika familia maskini hawakupata nafasi ya kusoma. Lakini kwa mujibu wa Muswada huu ambao umeletwa mbele yetu, nina uhakika tukiwa macho vijana wanaotoka katika familia za maskini ambao wana vipaji vizuri na wapo wengi sana wenye vipaji vizuri, wasaidiwe na Serikali ili waweze kusoma kwa faida ya Taifa letu. Kwa hiyo, naomba sana Muswada huu ukipita ufanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi sikuwa na mengi, lakini nilipenda haya yazingatiwe zaidi. Kwa sababu ningezungumza mengi lakini nitakuwa

narudia rudia yaliyosemwa na wenzangu. Ndiyo maana mimi nimechagua maeneo ambayo hayakuguswa kabisa na wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nakushukuru sana, na namhimiza Mheshimiwa Waziri aweze kufanya kazi vizuri baada ya sheria hii kupitishwa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo. Kwanza, naomba na nimi nianze kwa kuwapongeza wenzetu walioshinda kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika na kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya Wanawake wa UWT wa Mkoa wa Dar es Salaam na vilevile kwa niaba ya kijana mwenzangu wa zamani ambaye ninaishi naye pongezi hizi tunazitoa kwa dhati kabisa zimfikie jirani yetu mpenzi Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika.

Pongezi nyingine pia tunazitoa kwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa. Lakini pia nataka kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu, Dr. Pius Ng'wandu, pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Zabein Mhita na wale wote katika Wizara waliofanya kazi hizi usiku na mchana kuhakikisha wanaandaa Muswada mzuri kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa wengi wamechangia mengi mimi sitaki kuyarudia. Nataka pia niende kwenye maeneo machache ambayo ninayaona yana umuhimu wake katika muswada huu. Kwanza, kabisa nimwomba Mheshimiwa Waziri Pius Ng'wandu atakapokuwa anaanza kufanya uteuzi wa Wajumbe katika Bodi hiyo afikirie sana jinsia. Sina wasiwasi hili ataliweza kutokana na kuwa pia Mheshimiwa Naibu Waziri wake mwenyewe ni wa jinsia ya kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo kidogo ninataka kugusia katika *Part four section 16(2)* katika *Financial Assistance.* Nilikuwa naomba kidogo katika kuongeza waongeze *Travel Cost* hasa kwa ajili ya wale wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi.

Sehemu nyingine kwanza niliyokuwa nikiifikiria ni *Section 17* kuhusu umri. Mimi pia ninakubaliana na Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Huduma za Jamii kuwa umri huu upandishwe mpaka miaka 60 kujua kuwa hata wazee kama sisi wa umri huo bado tuna nguvu na uwezo wa kuweza kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishangaa wiki iliyopita mpangaji mwenzangu, kijana wa zamani aliniambia jambo lilinishangaza kidogo nikashtuka. Aliposema kuwa atakapomaliza awamu yake ya kazi basi huenda akaenda kusoma. Sasa ukifikiri mtu mwenye umri wa miaka 74 anasoma, sembuse mwenye miaka 60! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nizungumzie kidogo kuhusu kuongezea katika majukumu ya Bodi. Kwanza, ninaona ingekuwa ni bora zaidi kama kungefanywa uchunguzi mzuri na wa makini ufanyike kuhusu mikopo kwa wanafunzi

hasa wale wanaokwenda nje ya nchi. Je, ni aina gani ya masomo wanafunzi hao wanakwenda kusoma nje. Ni masomo ambayo hayapo hapa nchini hilo mimi nilikuwa nafikiri kwanza Bodi ingekaa ikafikiria ni aina gani ya masomo. Ni kama Mheshimiwa Diodorus Kamala amezungumzia kidogo inafanana na hii. Ni kuwa tukikaa tunazungumzia masomo yote kuwaruhusu watu kuwapatia hizi fedha waende nje hizi fedha kwa kweli tutazipata wapi?

Lingine je, hayo masomo wanayokwenda kusoma nje yatawafikisha wapi na watakaporudi watapatiwa ajira gani? Kwa hiyo, lazima yawe masomo ya kuendana na shughuli zinazopatikana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo nilikuwa nafikiri waliangalie na kulizingatia iwapo mkopaji huyo atakwenda kusoma nje ya nchi na ikitokea kuwa anatoweka kabisa akiwa huko nje na hata kubadili jina je, mzigo huo atabebeshwa nani, watabebeshwa wazazi ambao labda hawana uwezo, watabebeshwa ma-*guidance* ambao hawana uwezo? Hili ni jambo ambalo nilikuwa nikifikiri itakuwa vizuri iwapo bado kazi itafanyika kuweza kuliweka sawa. Jambo lingine ni muhimu Bodi ihakikishe kuwa *reports* zote za maendeleo ya ulipaji wa mikopo angalau zishughulikiwe na kuratibiwa wahakikishe kuwa kila mwaka wanapata ripoti na kuhakikisha kuwa mzunguko huo unazunguka ili fedha ziweze kurudi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ingekuwa sawa kama Bodi ingehakikisha kuwa mikopo yote inayotolewa inatolewa kwa madhumuni yale tu yaliyopangiwa. Yaani madhumuni ya mafunzo na kadhalika isiwe vinginevyo, ama sivyo tutapata hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo mkopaji atakiuka masharti ninaelewa kuwa kuna hatua zinaweza zikachukuliwa kama ilivyopangwa. Lakini pia si vibaya kama Bodi itaangalia suala la kusitisha kabisa mikopo ile kwa yule mtu anayekiuka masharti hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la mkopaji la kuongezewa mkopo ni jambo ambalo ni vyema tuliangalie tukizingatia kuwa mkopaji huyu ni mwanafunzi na huenda hata alikuwa hakupata nafasi ya kufanya kazi akaweka akiba na hata kama alipata kazi alikuwa na mshahara wa kiasi gani? Kwa hiyo, unakuta mwanafunzi anachukua mkopo wa kwanza, halafu inatokea kuwa hajamaliza kulipa ule mkopo kwanza, anataka kuchukua mkopo wa pili. Suala hili nilikuwa naona kuwa tusilinyamazie inatakiwa likawekwa liwe wazi kabisa. *(Makofi)*

Kuhusu Ibara ya 16 Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akiwasilisha maoni ya Kamati ametueleza wazi kuwa Chuo Kikuu hawakupata nafasi ya kuleta maoni yao. Lakini akaongezea akasema kuwa iwapo kuna Waheshimiwa Wabunge wanataka kuchangia chochote basi wanaweza wakaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni niliyokuwa nimeyapata ni kuwa wanafunzi hawa wanajisikia kuwa wamewekwa kando kabisa na Serikali na itakuwa imejitoa kabisa

kama haikuweza kuwafanikisha na kuwasaidia wanafunzi hao katika gharama mbalimbali kama vile *tuition fees, practical training* na pia *laboratory facilities* ambao mchakato wao nimeuchukua tu kijuu juu naomba niueleze kama ulivyo. *Tuition fee* zenyewe gharama yake ni milioni moja kwa mwaka mmoja, kwa maana hiyo kama ni mwanafunzi anayechukua Afya au *Engineering* miaka minne basi zinakuwa milioni nne. *Practical training* ni 280,000/= kwa mwaka kwa miaka minne inakuwa milioni 1,120,000/=. *Laboratory facilitation* ni 100,000/= kwa hiyo inakuwa ni 400,000/= kwa miaka minne. Sasa ukichukua ukazijumlisha kwa muda ule ni kuwa mwanafunzi huyu atakuwa amelipa milioni 6,240,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia gharama hizi kwa kweli ni kubwa sana, hawa ni wanafunzi na mwanafunzi hana fedha na hutegemei kama atakuwa na fedha. Hata kama mzazi wake atamsaidia, lakini tukumbuke kuna wanafunzi wengine wanakuwa wakijitegemea wao ambapo kwa wakati huo wanapoomba mkopo utakuta mshahara wanaoupata ni kiasi kidogo tu kama cha shilingi 50,000/=. Je, Serikali inaonaje katika kuliingilia suala hili ikalichambua kuliweka wazi ili angalau ikatoa unafuu kidogo kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mimi sitakuwa na mengi ya zaidi. Kutokana na mengi kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu siwezi kuyarudia rudia. Ninaomba kuunga mkono Muswada huu mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii na pili kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamechaguliwa kushika nafasi mbalimbali katika Mashirika mbalimbali. Nikianzia na Mheshimiwa Getrude Mongella, ambaye amechaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Rais wa *UNEP* na Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kuwa Rais wa Baraza la Mawaziri wa Elimu katika Bara la Afrika.

Napata faraja kwa sababu hawa wenzangu tumekuwa pamoja katika shule. Kwa hiyo, heshima hiyo naiona kama ni heshima ya *comrades.* Lakini ni vizuri wenzetu mkaelewa kwamba ni heshima kwenu na vilevile kwa nchi yetu. Kwa hiyo, mtunze vizuri heshima hii ambayo mmepewa na wenzetu kwa niaba ya Watanzania na ni heshima kwa Tanzania. Vilevile ningependa kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu kwa wakati huu. Ni kweli Muswada huu ni mgumu na utekelezaji wake utakuwa mgumu. Lakini hakuna njia. Wataalam wanasema: *"No new idea is born perfect, give it time to mature."* Kwa hiyo, kwa kuwa hili ni wazo jipya itabidi tuvumilie na wakati mwingine itabidi lipitie kwenye majaribio mbalimbali na kurekebisha mambo, lakini hakuna njia nyingine ni lazima tuanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimehusika katika mawazo ya mwanzo ya kufikiria wazo hili la namna umma wa Watanzania unavyoweza kushiriki kuchangia gharama za elimu kwa sababu ya ugumu wa tatizo na hakuna njia ya mkato. Elimu ni

kitu cha aghali sana kama ulivyo umaskini. Mtaalam mmoja aliwahi kusema: "Kama tunadhani Elimu ni kitu cha aghali mno, basi tujaribu ujinga." Huu ndiyo mtihani wetu. Sisi ni watu maskini. Ni maskini kwa sababu ni watu maskini na tutabaki maskini kwa sababu ni maskini. Kwa sababu ni maskini hatuwezi kubaki tu bila kutafuta njia za kujitoa katika mazingira haya ya umaskini. Wenzangu wengi wametoa mawazo mazuri ya kuchangia katika Muswada huu, lakini lazima tujitahadhari na baadhi ya mawazo.

Kwa mfano, wazo kwamba tubadili taasisi nyingi tulizonazo kuwa Vyuo Vikuu, ni wazo la hatari sana. Tukibadili Chang'ombe kuwa Chuo Kikuu tunazidi kukimbia kwenye utaratibu ambao unasaidia nchi hii. Kwa mfano, kuna haja ya kudumisha uwiano wa kitaalamu. Kwa mfano, upande wa masomo ya *Engineering, Engineer* mmoja mwenye *degree* anatakiwa kuwa na wataalam watano wa *level* ya *Technical College,* na wataalam kama 36 wa ngazi ya *VETA.* Sasa mwelekeo tunaotaka kuusema sasa utapotosha huo uwiano utakuwa na *Engineer* mmoja kwa watu labda watano, *ratio* inatakiwa *one to five to thirty five.* Ni vizuri tukajenga uwiano huu na vilevile tusipoangalia kama utatumia mwalimu wa *degee* mbili, kufundisha elimu ya msingi kama nchi, elimu itakuwa ya aghali sana.

La pili, nataka nidokeze kwamba ni lazima tufikirie upya ni kweli utekelezaji utakuwa mgumu. Lakini ningependekeza kwamba badala ya kufikiria huu mchango ambao utakuwa mgumu. Sehemu kubwa ya mchango iwe ni kwa njia ya pamoja kwa njia ya kodi, hii njia itakuwa nzuri sana na nyepesi zaidi kuliko njia nyingine yoyote ile. Na kwamba kigezo kikubwa kwa mwanafunzi uwe ni uwezo wake wa kiakili na siyo vinginevyo. Utafanyaje kwa mwanafunzi mwenye akili nzuri na uwezo mzuri na hana uwezo na kwa sababu ya ugumu wetu wa kuwa wakweli kama ilivyotokea katika utaratibu wa sasa. Tuliomba viongozi wa Wilaya na nani waseme lolote juu ya mwanafunzi anayeomba kusamehewa na Serikali anayesoma Chuo Kikuu, wote wanasema hana uwezo. Pale chini tuliuliza je, baba yako analipa kodi kiasi gani kwa mwaka, anasema milioni 20, halafu unasema hana uwezo asaidiwe. Kwa hiyo, unakuta katika mazingira haya ya kwetu kuna matatizo ya kimsingi ambayo ni kikwazo katika utekelezaji wa baadhi ya mambo hayo.

Lakini ningependa kusema jambo moja, kwamba bila kuwa na mkakati wa kuwasaidia watu wenye uwezo kwenda kusoma kwa kweli tutapoteza lulu, tutapoteza watu ambao ni hazina kwa nchi hii, tutawapoteza akina marehemu Nyerere wengi. Nimesoma kwa kuelimishwa na umma. Jana Mheshimiwa Joseph Mungai akitoa mfano wa kutoa elimu katika jamii yetu, alitoa mfano wa kwangu katika kuelezea matatizo ya jamii maskini, hakupata nafasi ya kuelezea zaidi, lakini kama angepata nafasi tatizo nililokuwa naelezea ni kwamba bila kuwa na mkakati wa makusudi wa kuendeleza jamii ya watu maskini kama Wamasai, Wabarabag, basi hatutakuwa na Wabarabag katika nafasi fulani za uongozi. Elimu ina tabia ya kuambukiza kama baba na mama wamesoma na watoto watasoma na ndiyo hali hii ilivyo katika nchi hii na wajukuu watasoma. Kama baba na mama hawakusoma na watoto hawatasoma na wajukuu hawatasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo elimu tusipoangalia inaweza kuwa ni kigezo kinachotumika kujenga matabaka katika nchi, kwa sababu hawa watakaokuwa na elimu ndiyo watakuwa na nafasi ya kutawala nchi, kuchaguliwa kushika nafasi muhimu katika Mashirika ya Umma, katika uchumi na ndiyo watakaokuwa na kauli. Mtaalam mmoja wa Yugoslavia anaitwa Gelas alizungumzia juu ya *"New Class."* Kwa hiyo hapa tutazalisha matabaka mapya ya watu, siyo lazima wawe na mali, lakini watu walio na *access to property* na *influence* kubwa katika nchi na hao ndiyo watakaokuwa wanatawala nchi. Kwa mazingira ya kwetu tusipoangalia ambapo asilimia 80 ya Watanzania wapo vijijini na asilimia 20 wako Mijini na hao asilimia 20 wa Miji ndiyo wanaopata asilimia 80 ya nafasi katika Shule za Sekondari na ndiyo watakaoenda Vyuo Vikuu na ndiyo watakaokuja kutawala wale asilimia 80. Kwa hiyo, katika hali hii ya umaskini ni vizuri tukatumia kigezo cha uwezo wa elimu, kwamba yeyote aliye na uwezo atakuwa na nafasi ya kwenda ili mradi Serikali iwe na utaratibu mzuri wa kuthibitisha hivyo. Vinginevyo tutawakosa akina Marehemu Nyerere wengi na tutawakosa watu wenye uwezo wa kusaidi nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuulizane ni kweli kama alivyosema mwenzangu mmoja kwamba kama mtu anatafuta *degree* ya Pili na ya Tatu ajisomee mwenyewe. Unaweza ukazungumza hivyo kwa masomo kama *history,* ya *Economics,* ya *Practical Science,* lakini kama masomo ya Sayansi, wewe unafanya kazi Muhimbili, unahitaji kuendelezwa ili uweze kuhudumia wagonjwa wa moyo au wa akili na ni kwa faida ya nchi kama utakwenda kusoma kusudi uje ukapate utaalamu wa hali ya juu zaidi. Katika mazingira ya namna hiyo, utajiendeleza mwenyewe na gharama katika masomo kama hayo ni za juu sana utawezaje kupata masomo kama hayo?

Elimu ni haki lakini nadhani kwa nchi maskini kama sisi hatuwezi tukatoa elimu katika ngazi zote bure kwa kila mmoja. Itabidi wengine tuwapeleke mbele kwa ajili ya faida ya wengine. Itabidi elimu kwa ngazi fulani tuitazame kama ni shamba la mbegu, kwamba unataka upate mbegu bora ili uje uitumie mbegu hii kuzalisha mbegu bora zaidi kwa kusambaza kwa wakulima wengi zaidi na ndiyo ninavyoona katika masomo kama haya. Kwamba elimu fulani itabidi lazima tuvumiliane tusomeshe wachache kwa ajili ya faida ya watu walio wengi zaidi. Vinginevyo tutabaki wote pale pale. Nilisema tena elimu inaambukiza sana, kama wazazi wamesoma na watoto watasoma. Nilichokuwa nikishangaa katika kuongea na Mheshimiwa Joseph Mungai ni kwamba kama lazima usome kutoka *kindergarten,* elimu ya msingi, elimu ya *Middle School, Secoandary* ukapate chuo Kikuu ndipo uje uoe halafu umpeleka mtoto *kindergarten* ndiyo aje awe wa pili, katika eneo fulani, basi kuna matatizo. Ilani hiyo ndiyo *thrust* ya *debate* siyo kushangaa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ukitazama kama wazazi wamepata Elimu ya Juu hapa ndiyo ambao na watoto wao wanasoma na kwa baadaye kwa kutumia elimu itakuwa ni kazi ngumu sana, kwa sababu ya tabia hii ya *self perpetuation* ya ambao wamesoma na watasoma, kwa hiyo kutakuwa ni wale wale watakaokuwa na *excess* hata kwenye uongozi, kwenye Ubunge, kwenye *management,* kwenye nafasi zote katika nchi, unaondoaje tabaka kama hilo. Nilidhani hilo ndugu zangu ni maeneo ya kutazama kama Waheshimiwa Wabunge na ndiyo maana suala la kujenga shule za Sekondari Vijijini ni

suala la kupambana na hawa wachache kusudi tupeleke elimu kwa walio wengi zaidi. Tupeleke shule kwa watu na siyo kuwaleta watu kwenye shule za mijini. Nilidhani hiyo katika *revolution* ni *strategy* ya ku-*fight* na *mass.*

Kwa nini tunasoma hatusomi kwa sababu ya kupata kazi, maana kama ni hivyo, ajira hapa Tanzania kwa Serikali ni nafasi kama 300,000 au chini yake. Na sisi tuko milioni 36, na wanaosoma tayari hawa nafasi zimeishajaa. Kwa hiyo, tunasoma kwa sababu elimu ni ufunguo wa maendeleo, elimu ni nyenzo inayoongeza upeo wa wewe kuona mambo, elimu inapanua wigo wa uhuru, elimu kama walivyosema wengine ni haki ya kila Mtanzania. Hakuna kitu cha bure, *concept* ya bure nadhani nayo inapotosha kufikiri. Bure maana yake nini? Ni kwamba hakuna aliyegharamia. Nasema elimu igharamiwe na umma kwa kiwango kikubwa na tueleze vilevile kwamba tunazungumza hii maana yake nini? Ni mafunzo darasani, ni mavazi, ni chakula, ni vitabu, ni kitu gani? Tusipoelewana hapa tunaweza tukapata matatizo ya kimsingi, kwa sababu ya kuanzia mahali pasipo na maelewano vizuri zaidi. *(Makofi)*

Lakini mimi ningependa kumalizia kwa kusema kwamba katika mazingira haya ya dunia hii ya tatu, hatuwezi kutoa elimu kwa kila mtu, hasa baada ya kiwango fulani. Ndiyo maana kwa sasa hivi elimu ya lazima kwa kila Mtanzania na ambayo ni haki tumesema ni ile elimu ya msingi. Elimu ya Sekondari ndiyo maana haiwezekani, Elimu ya Chuo Kikuu tutakuwa *selective* kwa gharama za umma, kwamba ni eneo lipi na kwa faida ipi vinginevyo itabidi tuvumiliane. Lakini kusema utatoa elimu kwa wote hata nchi zilizoendelea bado zina matatizo hayo. Sasa kwa sisi kwa sababu ya umaskini kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, mimi nilikuwa napendekeza kwamba katika Mfuko huu huenda ni vizuri tukaanzia mahali, kurudi nyuma utapata matatizo zaidi.

Unataka urudi hata wakati mimi nasoma useme na mimi nianze kuchangia kwa sababu ya utaratibu. Maana hatukuwa na mkataba huo. Mimi nilisoma kwa gharama za umma chini utaratibu wa kimkataba ambao uliokuwepo wakati ule na ulikuwa mkopo. Mheshimiwa Magani alikuwa amekopa. Mimi nilikuwa na utaratibu mwingine. Sasa nasema ni lazima tuanzie ni wapi hapo Wizara lazima itaamua. Sasa mimi katika kupendekeza huu mfuko kama ninavyouona huenda hakuna aliye na *readymade formula* ya namna ya kutekeleza jambo hili. Ni kama mtoto wa jongoo alipozaliwa alimwuliza mama yake, mama nianze kutembea na mguu upi? Kwa bahati mbaya hata mama yake naye hakujua alianza na mguu upi? Kwa hiyo, akishindwa jibu la kumpa mtoto wake akamwambia tembea tu mwanangu. Alipoanza akakuta anatembea huyo jongoo na safari ilianza.

Kwa hiyo, Dr. Ng'wandu itabidi uanzie mahali. Kutakuwa na matatizo lakini hakuna *short cut*. Hayo matatizo mengine yatakusaidia kukufundisha. *There is no readymade formula.* Ukisema mazingira ya Kenya, Uganda na ya Tanzania ni tofauti. *You cannot import a revolution. You can import revolutionary ideas* lakini lazima mawazo yalingane na mazingira ya kwako, mazingira ya Tanzania. Ni kwa njia hiyo tu

tunaweza ukasonga mbele zaidi. Kwa hiyo, *seek* hii: *"The education kingdom and the rest will be harden to you"*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nikitegemea kwamba hii itakuwa ya mwisho walivyokuwa watu kila mmoja ana hamu ya kwenda kuwapongeza wenzetu zaidi huko nje. Kwa hivyo ningependa nitumie muda mchache sana wa kutoa maoni yangu kuhusiana na Muswada huu uliokuweko mbele yetu. Ili kupunguza wakati nafikiri pongezi zinakwenda moja kwa moja. Lakini kwa upendeleo maalum nimpongeze rafiki yangu Prof. Ng'wandu kwa vile leo ndio kwanza nimepata taarifa hiyo na kuweza kuelewa kwamba alikuwa ni Rais wa Wahadhiri wa Elimu ya Juu ya Tanzania. Kwa hivyo hongera sana Prof. Ng'wandu. Wengine kwa kawaida ni usiku tutazidi kupongezana huko kwenye chakula. *(Makofi/Kicheko)*

Kwanza nisije nikakosea niunge mkono moja kwa moja Muswada huu ulioletwa mbele yetu hapa. Muswada ambao kwa kweli kila nikizingatia naona ni Muswada umekuja kwa wakati kabisa. Kwa sababu kama tunavyoelewa elimu ni haki ya kila mmoja, ya msingi, kabisa ikiwa kama utakwenda shule au utasomeshwa nyumbani lakini elimu ni elimu. Lengo na madhumuni haya ya Muswada wetu huu ni kuona kwamba tunapata watalamu wa hali ya juu ili kuweza kuwaendeleza wale waliokuwa wa hali ya chini na wao waweze kuendesha maisha yao ipasavyo.

Kwa ruhusa yako ningependa nitoe historia ndogo tu ambayo imenipata mimi. Kimsingi mimi msomi ninayetokana na maisha ya kimaskini kabisa kama alivyotangulia msemaji mwenzangu. Nashukuru kwamba mpaka nimefikia taaluma niliyoipata nimesomeshwa bure. Lakini bure sio bure ya kusema haina maana, ni bure kwamba sikutoa malipo. Sikutoa malipo kulingana na hali ambayo tulikuwa nayo kwa wakati wetu. Lakini kwa kweli tukilinganisha tunakotoka na hapa tulipo tuzungumze ukweli ni watu kiasi gani sasa hivi ambao tungeshindwa kuweza kumudu angalau kidogo tu cha kuwachangia watoto wetu wakaweza kusoma kama ilivyokuwa mimi baba yangu alishindwa shilingi 15/= za kunilipia kwa mwaka kwa Shule ya Msingi. Wala hatukuwa na njia yoyote ya kuweza kukopa kwa mwingine kwa sababu na mwingine alikuwa hana vile vile. Sasa leo ikiwa kama Serikali imekuja na utaratibu huu wa kutukopesha kwa nini tuwe na vizingiti vya kuweza kujiwekea sisi wenyewe wakati njia ipo ya kutupatia elimu ipasavyo. Kwa hivyo, kwa misingi hii naunga mkono Muswada huu mia kwa mia bila ya wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa na jambo moja tu ambalo ningependa kidogo niongezee katika kutahadharisha kufuatana na masuala haya ya Miswada. Alipokuwa anazungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, alizungumza kitu kimoja kidogo kilinishtua. Alisema kwamba kuna wenzetu wadau kutoka Chuo Kikuu walichelewa kuleta maoni yao na badala yake maoni yao wakayaleta baadaye. Sasa najiuliza ilikuwa kuwaje kwamba Chuo Kikuu wakati wamepata taarifa ya kuja kuchangia leo ifike mpaka unawasilishwa Muswada hapa ndio wanaleta maoni yao. Nilikuwa na ushauri mkubwa sana kwamba wakati tunapokuwepo katika suala hili, ili kutupunguzia mzigo sisi Waheshimiwa Wabunge tuliokuwa na jukumu la kuzungumza

na wanaotuletea Miswada waweze kufika kwa mujibu wa taratibu zilivyo ili tuweze kupunguza haya matatizo.

Sasa mimi leo hapa sisemi kama sikubaliani na maelezo ambayo wameyazungumza wenzangu kutoka Chuo Kikuu. Nakubaliana sana. Kwa hivyo kutokana na misingi hiyo natumaini kwamba ripoti au mawazo yao wameyawasilisha kwa njia nyingine. Sasa tu kwa kile ambacho nimekishuhudia hasa tukizingatia kama mimi ni Mjumbe wa *Council* ya Chuo Kikuu ambavyo wenzangu hapa mlituchagua pamoja na wenzetu tungebidi nalo suala hili tulizungumzie na tuweze kuwashauri wenzetu nao walizingatie ipasavyo. Sasa ningeomba tu kwa yale, ingawa yamefika kwa wakati ambao tumeshafikia hatua hii, labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha, kama atakuwa nalo la kutuzungumza, atuambie. La kama ikiwa hana ningemwomba sana ayafikirie sana haya masuala ambayo wenzetu wameleta wakati atakapotunga sheria au kufanya marekebisho ya sheria pamoja na wakati atakapounda zile kanuni na sheria ndogo ndogo ili kuweza kuona ni kiasi gani tunawajumuisha wadau wote wanaohusika katika kutayarisha Muswada wetu huu kwa hii leo.

Kwa hivyo nafikiri hayo yalikuwa ni yangu makubwa kwasiku ya leo na zaidi kwa hivyo kuwa na dakika tano ni kwamba Muswada wetu huu yamepita mapendekezo kwamba uitwe *Higher Education Loan* badala ya *Government Loan.* Kwa hivyo ningekubaliana sana na wazo hili la kubadilisha jina la Muswada kuwa *Higher Education Loan.* Kwa sababu kama tukizungumza *Government Loan* tunasema kwamba Elimu ya Juu ni suala la Muungano ni katika shughuli za Kimuungano. Lakini sasa tukitazama vyuo hivi viko vingine ambavyo si vyuo vya Serikali, haviko katika shughuli za Kimuungano. Sasa tutakapolizingatia hili kama suala la Kimuungano. Sasa tukizungumza kama Zanzibar tuna Vyuo Vikuu vinne ambacho chuo kimoja tutasema ni cha Serikali. Tukisema cha Serikali itakuwa ni Serikali ya Muungano. Lakini vile vitatu ambavyo havipo mle tutavichukua katika sehemu gani. Kwa hivyo ningependekeza sana kwamba hii iwe ni *Higher Education Loan* kuliko kusema *Government Loan* wakati zile sekta nyingine ambazo hazimo kwenye *Higher Education* ziko chini ya Serikali zetu hizi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo maelezo machache naomba kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa shughuli za leo tumefikia hapo. Kwa wachangiaji ambao wameleta maombi hapa wamebakia watatu, nao wataendelea Siku ya Jumatatu kabla ya Mheshimiwa Waziri kumalizia hoja yake. Baada ya maelezo hayo sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.38 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 19 Aprili, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*